# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS

## MWATATE CONSTITUENCY HELD AT

## KENYATTA HIGH SCHOOL

**FRIDAY, 3rd MAY 2002**

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MWATATE CONSTITUENCY, HELD AT KENYATTA HIGH SCHOOL ON FRIDAY, 3rd May 2002.

**PRESENT**

Com. Prof. Wanjiku Kabira
Com. Keriako Tobiko

**SECRETARIAT STAFF IN ATTENDANCE**

Fatuma Jama - Program officer
Onesmus Kipchumba - Assistant Program officer
Alice Thuo - Verbatim recorder
Nancy Odipo - Sign language interpreter

**The meeting was called to order at 9.00a.m.**

**Frida Mwadime:** Wapendwa, wale ambao wameketi kule nyuma tafadhalini tungetaka tuanze pamoja. Pengine kama mngegeuka tu, tuombe halafu tuendelee. Na wale ambao walioko nje pia waweze kufika hapa karibu. Nafikiri tungesimama sote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku hii ambayo wengi tumekuwa tukitarajia kwa hamu kuu. Naam. Nafikiri nitaomba.

**Maombi:**

Baba katika jina la Yesu Kristu tunalibariki na kulitukuza na kuliinua jina lako tukijua kwamba wewe ni mweza wa yote na ni mwanzilishi wa mambo yote. Na tunaelewa ya kwamba unapoanza jambo, katika kuanza umekamilisha. Tazama umefika wakati ambapo tumekusanyika tena katika ukumbi huu ili tukaweze kutoa maoni yetu ya kuweza kurekebisha Katiba iliyoko mbeleni mwetu eeh Bwana. Tunakuomba ukapate kutuongoza, ukimpa kila mmoja wetu hekima na uwezo na mamlaka ya kuweza kuyatamka yale yote ambao umeweka mioyoni mwao ili Baba tukaweze kurekebisha Katiba itakayo saidia nchi yetu na kusaidia wananchi na wote watakao husika ili utukufu na sifa zikapate kukurudia. Nashukuru hata kwa wale wako njiani wanakuja ukawawezeshe wakapate kufika hapa na wale ambayo tutakuwa pamoja nao Bwana watakapo pokea mambo haya, wakapate kubarikiwa na yote ambayo yatakuwa yamenenwa mahali hapa. Nashukuru hata kwa ajili ya Ma-commissioners wetu kwa kazi kubwa ambao umewapatia ya kuweza kwenenda hapa na pale ili kupokea maoni kwa wananchi; Kazi yao Baba ukapate kuibariki wanapo kamilisha Katiba hii, tukapate kunena kwa hakika Wakenya tumekuwa kitu kimoja. Nashukuru nikijua kwamba umekamilisha mambo yote na ni katika jina la Yesu Kristu Mwokozi nimeomba na kuamini. Shukrani.

**Fridah Mwadime:** Kwa hivyo pengine ningependa kwa kifupi tu, kuwatambulisheni kwenu wanakamati wa sehemu hii ya uakilishi bunge ya Mwatate. Wengi wao mnawafahamu lakini kwa sababu ni muhimu niweze kufanya hivyo nitataja. Kamati hii ina wanakamati kumi, mojawepo akiwepo ni Mbunge wa mahali hapa ambaye ni Waziri Retired Major Marsden Madoka. Na aliahidi kwamba atakuwa pamoja nasi siku ya leo na nataraji labda yuko njiani anakuja.

Wa pili ni Mwenyekiti wa baraza ambaye ni Councillor David Riga, nafikiria pia yuko njiani atafika mahali hapa. Wa tatu ni mimi kama mshilikishi wa mambo ya Tume ya kurekebisha Katiba katika wilaya ya Taita Taveta, majina yangu ni Mrs. Frida Mwadime. Wengine ni wale akina mama ama wanawake watatu ambao walikuwa ni lazima wachaguliwe ili wawe katika kamati hii. Wa kwanza kabisa akiwa ni Councillor Clara Juma - Clara yuko pale. Simama tu wananchi wakuone najua wanakufahamu lakini kwa heshima yao. Anatoka sehemu ya Chavia wilaya Taita Taveta.

Na wa pili ni Elizabeth Mwabingu, anawakilisha location ya Bura. Wa tatu ni mama ambaye naona hajafika bado, yeye ni Magdalene Ngati na anawakilisha sehemu ya Mwakitau. Wale wengine wako nje kama mwandishi wetu ni Tom Mwashube, na mwenzake Alvis Ibrahim Nyambu anayesimamia ndugu zetu waislamu. Halafu tuna kijana ambaye anasimamia pia walemavu, Lloyd Mwambela - sijui kama nimesahau. Kuna mwingine nimesahau? Halafu kuna ndugu yetu ambaye ametoka sehemu za Ronye juu - kule juu kabisa, anaitwa Stephen Malanga, nafikiria yuko njiani atakuja. Kwa hivo nitarejesha kikao hiki kwa Commissioner Prof. Wanjiku Kabira aweze kutuendeleza kuanzia hapo. Nawashukuru nyote kwa kufika na nataraji kwamba tutaanza vyema na tutamaliza vyema. Asanteni sana. Kwa hivyo karibu Commissioner.

**Com. Kabira:** I would like to declare this sitting as a sitting of the Commission na nimefurahi sana kuwa hapa siku hii na tunamngojea Commissioner Tobiko anakuja. Lakini tulisema tutaanza kwa sababu tumeambiwa kutakuwa na watu wengi sana asubuhi hii. Tulitarajia kuanza kama saa tatu na ninaona saa hii ni saa tatu na dakika kumi na tano. Ili tuweze kuwapatia watu wengi nafasu waweze kutoa maoni yao, tutapatiana dakika tano kwa yule mwenye memorandum ataje yale muhimu halafu anatupatia memorandum. Lakini akiwa hana memorandum, tunampatia dakika kumi aseme yale anataka kusema. Lakini kukiwa na watu wengi twaweza kumpatia dakika kama tano au hata tatu ili kila mtu apate wakati wa kutoa maoni.

Utaratibu wetu ni kuwa tutaenda kulingana na record ile mmeandika huko nje na tutaenda according to that record lakini pengine tukifika saa nane au saa tisa, tutawapatia wale wametoka mbali na pia walemavu nafasi, ikiwa mtatupatia ili waweze kuongea na waondoke mapema. Lakini kwa leo tutaanza na yule alijiandikisha kama namba moja na nitamuuliza aje hapa mbele azungumze lakini kabla ya hapo ningeomba wale secretariat tuko nao wajitambulishe nikianza na program officer. Can you introduce yourself please?

**Fatuma Jama:** Kwa jina naitwa Fatuma Jama, I am a program officer.

**Onesmus Kipchumba:** Kwa majina naitwa Onesmus Kipchumba, Assistant Program Officer na nimefurahi kuwa hapa.

**Alice Thuo:** Kwa majina naitwa Alice Thuo, verbatim recorder.

**Nancy Odipo:** Naitwa Nancy Odipo, natafsiri lugha ya wasiosikia.

**Abraham Karanja:** Kwa jina naitwa Abraham Karanja mimi ni driver.

**Com. Kabira:** Hiyo ndiyo team tulikuja nayo na tutaanza na yule aliyejiandikisha nambari moja. Anaitwa Rebecca Chari.

**Rebecca Chari:** Kwa majina ni Rebecca Chari Mwamburi. Hii ni memorandum yangu binafsi ambayo nimeiwakilisha. Ya kwanza ni kwamba ninataka hati ya shamba iwe na majina mawili Mr. and Mrs. Kulingana na rasilimali zilizoko katika Taita Taveta, ninataka elimu iwe ya bure na madawa yasilipishwe hospitalini. Soko ziwekwe karibu na mkulima au mfugaji kwani faida yake yote inaishia kwa transport au uchukuzi na hivyo hafaidi chochote yeye kama mkulima wa nyumbani. Pesa za malipo ya soko zinaumiza yule mfanyi biashara ndogo ndogo. Kwa sababu wakati mwingine mtu ana licence, tena akiwa kwa soko anaitishwa ushuru wa sokoni.
ID card zinatumia ghalama na muda na ninaomba ziletwe kwa kiwango cha location. Chief anaelewa na watu wake. Njia nyingine ni kuwa tatizo hilo linakabili kuchangia ukahaba kwa wasichana wanaotoka mbali kwa vile hawana uwezo.Pia wengi wanapitisha muda wa kuchukua hiyo hiyo ID na inabidi walipishwe fine. Njia nyingine wengi wanapitisha muda wa kuchukua ID hiyo, inawabidi walipishwe fine.

Katika division yetu ya Mwatate, wageni wamemiliki mashamba kwa wingi, na ni uridhi wetu. Ninaomba kama ni wageni, wawe hapa kibiashara au kama waajili. Na kama wanamiliki pia kuwe na kiwango fulani; Wenye umilikaji wanafaidi. Rasilimali yetu ya Tsavo National Park, 80% iwe ni mali ya Wataita. Taita Sisal estate pia ilipie ushuru kwa Wataita kama 50%. Kutoka kwa misitu, madawa yatolewa, gum, mbao, zinatolewa na hatujafaidi chochote - na hiyo ni rasilimali na vile vile hii inaharibu chemchemi zetu.

Afisi ya madini iwekwe mahali rasilimali ya madini inatoka. Na pia wenye wanatoka mbali na wanafaidi kwa madini, lazima waache 50% ya madini, ifaidiwe na wenyeji. Mume akiweka msichana mimba, lazima aajibike na ulezi, asimwachie msichana alee peke yake. Pia tohara ya mtoto wa kike iondolewe kabisa - ikomeshwe. Mtu mmoja asirundikiwe mamlaka wakati wengine wamesoma na wana ujuzi wa shughuli hiyo. Mtu akifikisha miaka arobaini, astaafu wengine wapate nafasi ya kazi.

Polisi asinipige au kunitesa bila sababu. Kama nimekosa, mahakama inihukumu yenyewe. Na kama mtu amejisalimisha tena asipigwe. Polisi akipokea hongo aachishwe kazi. Rasilimali zinazoingiza mapato katika Kenya Ports Authority ya Coast, 70% mapato yawe kwa watu wa Coast. Na pia wageni lazima watoe heshima kwa wenyeji - mtu kama amekaribishwa mahali na anaishi asijaribu kutoa matusi. Mtu akitoa matusi arudishwe kwao. Pia naomba muda wa kurekebisha Katiba ambayo

tunaendelea nayo wakati huu, kama kuna kipengele chochote kinarekebishwa, lazima tuhusishwe kama tulivyohusishwa wakati huu. Asanteni.

**Com. Kabira:** Kabla ya kwenda Bi. Rebecca, nina swali tafadhali. Umesema mtu akifika miaka arobaini "to go on retirement?" Ni hivyo ulisema kuhusu retirement?

**Rebecca Chari:** Nimesema mwajiri ambaye amejiriwa akifikisha miaka arobaini kuliko hiyo ya hamsini au hamsini na tano, astaafu na hao watoto ambao wamemaliza shule nao wapate nafasi ya kazi.

**Com. Kabira:** Asante sana. Utajiandikisha kwa secretariat. Martin Mwande. Martin Mwande.

**Martin Mwande:** Mimi kwa jina ni Martin Mwande na niko hapa kuakilisha Kishamba location. Kuna kamati ya viongozi wa Kishamba location ambao walikutana - watu karibu mia moja ishirini na watano na wakatoa maoni yao na wakanituma nije niitoe siku ya leo. Nitaanza kwa kile kijitabu ambacho mlitupatia, "Hati za ardhi" yaani ukurasa wa kumi na nane. Anayepaswa kuwa mumiliki wa mwisho wa ardhi ni jamii ya mahali pale. Pili; Serikali iwe na uwezo lakini kuwe na makubaliano fulani baina ya Serikali na wenye ardhi. Mwenye ardhi kusiwe na lazima yaani kulazimishwa chochote na Serikali. Serikali ya mitaa iwe na uwezo wa kudhibiti uamilikaji na wakaazi wanavyotumia ardhi. Jamii ishughulikie mambo ya ugawaji wa mashamba. Mtoto akifikisha umri wa miaka kumi na nane, apatiwe shamba lake na wazee ili aweze kujiendelesha kimaisha.

Kuwe na kiwango cha juu cha ardhi inayoweza kumilikiwa na mtu binafsi. Umilikaji wa ardhi urahisishwe na kusiwe na malipo mengi katika kubadilisha title deed kutoka kwa mzee hadi mtoto. Maafikiano na mapatano yaliyokuwepo kabla ya uhuru miongoni mwa wanajamii yasiwepo na yasiwekwe siasa kwa sababu kuna ongezeko la watu.

Wanawake wawe na uwezo wa kumiliki ardhi sawa na wanaume lakini kuwe na utaratibu na makubaliano baina ya jamii. Halafu kuna kitu kimoja ambacho tulisahau ambacho nimekumbuka saa hizi - kuna kipengele kilichoko katika sheria za ardhi kinachoeleza kuwa mtu ana haki kumiliki fiti sita pekee chini ya ardhi hata kama mtu ana title deed. Hicho kifungo tunaomba kiondolewe ili kukipatikana madini, mwenye shamba amiliki - maana ndicho kinafanya wananchi hata kama shamba ni lake, hana uwezo wa kumiliki; - maana anamiliki tu fiti sita chini ya mchanga. Kwa hivyo hicho kipengele ikiwezekana kiondolewe kabisa ndio mwenye shamba atamiliki pale.

Ukurasa wa kumi na sita: "Haki za kimsingi." Masharti ya Kikatiba haki za kimsingi hayatoshi. Serikali iweze kuwasomesha watoto kwanzia shule za vidudu yaani nursery school mpaka kidato cha nne bila malipo. Hukumu ya kifo ikiwezekana iondolewe na badala yake kuwe na kifungo cha maisha. Mwananchi afundishwe na kupewa uwezo kutumia rasilimali zake. Apatiwe vifaa zinazowezesha kutumika kwa shughuli hizi. Katiba ilinde usalama, huduma ya afya, maji, elimu, makaazi, chakula na ujira. Usalama upewe muda zaidi chuoni ili wanao husika wapate elimu zaidi ya kujua sheria. Huduma ya afya iwe ya bure

kwa sababu wale ambao hawana uwezo wa kifedha wanapata shida sana.

Ukurasa wa kumi na saba: Maslahi ya wanawake hayajahakikishwa kikamilifu na Katiba. Iwapo msichana amepata mimba hatua za kisheria zichukuliwe. Pia msichana akinyanyaswa kimapenzi, mhusika achukuliwe hatua za kisheria.

Walemavu wapewe elimu ya bure kwanzia shule za vidudu hadi chuo kikuu. Wapewe vifaa vya kutumia ili kuweza kukabiliana na hali yao. Wapewe mikopo ya kuwawezesha kujiendeleza baada ya kumaliza masomo. Wapewe vifaa maalumu vya kuwawezesha kuwasiliana. Wapewe nafasi nzuri za kazi kulingana na ujuzi na elimu yao.

Katiba inaweza kulinda haki za watoto kwa kuwapatia elimu ya bure; Ofisi za kuwashughulikia watoto ziletwe katika kiwango cha kata yaani hizi shule ambazo ni za walemavu, ziletwe katika kiwango cha kata. Makundi mengine ambayo hayashughulikiwi na Katiba ni wazee, wajane, maskini na mayatima. Kwa hivyo Katiba ikiwezekana ishughulikie watu kama hao.

Katiba itoe masharti kwa vitendo, vishawishizi kwa manufaa ya wanawake na makundi mengine. Kuwe na masharti kwa vitendo, kuwe na kamati tekelezi katika viwango vya vijiji.

Ukurasa wa kumi na tisa: Katiba itambue na iendeleze lugha za kienyeji, tuwe na lugha moja ya taifa ya Kiswahili. Ili kuhakikisha umoja na usalama wa mtu binafsi na mali, ni lazima mtu aheshimu mila na tamaduni za wale wanaoishi pale yaani wenyeji. Mila na desturi lazima zihifadhiwe lakini kwa uangalifu.

Uongozi wa matumizi wa mali asili: Mamlaka ya nchi yasiendelee kuthibiti uwezo huo. Mamlaka yathibitiwe na Serikali za mitaa yaani Local Authority. Bunge isiwe na uwezo wa mamlaka ya kuamrisha ukusanyaji wa matumizi ya fedha za umma, - Serikali za mitaa zipewe uwezo huo. Msimamizi na mkaguzi wa fedha za umma, yafaa apewe ulinzi zaidi na awe akichaguliwa katika Bunge. Mkaguzi mkuu ateuliwe na bunge. Tunaweza kuwavutia wakenya walio talaamika ili waweze kufanya kazi katika mashirika ya umma kwa kuwapatia mishahara mizuri. Anaye paswa kuteua tume ya huduma za umma ni Bunge. Inatupasa kuwa na kanuni za maadili ya maofisa wote wanaohudumia umma na walazimishwe kutangaza mali yao.

Maswala ya uhifadhi wa mazingara yanayopaswa kuingizwa kwenye Katiba ni vianzo vya maji yaani water catchment areas, misitu, zichungwe kikatiba. Kamati ziundwe za kuhusika na mazingara. Matumizi ya rasilimali zipatiwe katika Serikali za mitaa. Mali sote zinapaswa kulindwa na Katiba. Mwenye jukumu la kulinda na kusimamia mali ya asili ni mwananchi kupitia kwa Serikali za mitaa. Mali ya asili, zisimamiwe na kamati ndogo ndogo kutoka mashinani.

Ukurasa wa kumi na tatu:- "Serikali za mitaa." Mayor na wenyeviti wa mabaraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Mayor na wenyeviti wawe na vipindi vya miaka mitano. Mabaraza yasiendelee kufanya kazi chini ya Serikali kuu. Kiwango cha elimu cha chini cha madiwani kiwe kidato cha nne. Mitihani inayofanywa ya lugha haitoshi. Kuwe na masharti ya kimaadili na

kitabia kwa wagombea viti vya udiwani. Wananchi wawe na haki ya kumrejesha diwani nyumbani kwa kura ya kukosa imani. Atakayekataa kauli kuhusu mishahara na marupu rupu ni tume ambayo itachaguliwa na wananchi. Ndio tuwe na madiwani walioteuliwa lakini kuwe na njia maalumu ya kuwateua. Madiwani waongozwe na masharti yafuatayo katika mfumo wenye vyama vingi: Uwazi, uajibikaji na uaminifu. Rais au Waziri za Serikali za mitaa asiwe na uwezo wa kuvunja mabaraza.

Ukurasa wa kumi na nne: "Muundo wa utaratibu wa uchaguzi." Tufuate mfumo wa kura za siri. Tuendelee kufuata mfumo ambao mwenye kura nyingi ndiye mshindi. Wanawake watengewe viti maalum hadi kiwango cha wilaya. Idadi ya chini ya mgombea kiti iwe ni asilimia hamsini na ikiwa hakutosheleza kiwango hicho katika duru ya pili, asitangazwe kuwa mshindi. Wagombea viti wanaokosa kuteuliwa na chama kimoja wako huru kuomba uteuzi kutoka vyama vingine. Kuwe na uhuru wa kuhama kutoka chama kimoja hadi kingine. Tuendelee kuwa na kanuni ya asilimia ishirini na tano ya uakilishaji katika angaa mikoa mitano katika uchaguzi wa Urais. Tuwe na viti maalum vilivyotengwa kwa makundi ya akina mama, walemavu na vijana.

Tuendelee kuwa na maeneo ya kigeographia katika uakilishi lakini yhata hivyo hatutosheki na ugawaji wa maeneo ya uakilishi wa bunge na mabaraza. Kwa mfano kama juzi kuna viti vya mabaraza vilizokusanywa vikawekwa pamoja pamoja, ile hali ambayo ilichukuliwa hatutosheki nayo, ikiwezekana ingeangaliwa kwa uzuri zaidi wananchi wakaelewa.

Tuendelee kufanya uchaguzi wa bunge na mabaraza wakati mmoja. Utaratibu wa uchaguzi urahisishwe kwa kuhesabu kura hapo hapo baada ya kumaliza kupiga kura. Tarehe ya uchaguzi itajwe kwenye Katiba. Uchaguzi wa Urais uwe na kura ya maoni na pia ufanywe moja kwa moja. Ma-commissioners wawe na sifa nzuri, uajibikaji na uwazi na wateuliwe na bunge na pia wahakikishiwe usalama wa kikazi. Kuteuliwe ma-commissioner ishirini na wawili.

Ukurasa wa saba: "Vyama vya kisiasa": Vyama vya kisiasa visitekeleze majukumu mengine. Katiba itekeleze uundaji, uongozi na tabia za vyama vya kisiasa. Kuwe na idadi maalum ya vyama vitakavyosajiriwa. Tuwe na jumla ya vyama vitatu na kila chama kiweze kujighalamia chenyewe na sio kwa fedha za umma na kuwe na uhusiano mzuri baina ya dola na vyama vya kisiasa.

Ukurasa wa nane: "Muundo wa aina za Serikali." Tusiendelee kuwa na muundo wa Serikali ya Urais. Tufuate muundo wa Serikali ya ubunge ambapo Waziri Mkuu na chama chenye uwezo zaidi bungeni ndiye atakayeunda Serikali. Rais awe na uwezo wa kuweka sahihi mijadala itakayopitishwa bungeni. Tusifuate muundo wa mseto ambapo mamlaka ya nchi yamegawanywa baina ya Rais na Waziri Mkuu. Tuendelee kufuata muundo wa Serikali moja kwa ajili ya usawa katika ugawaji wa rasilimali za wenyeji. Njia ambazo zinaweza kufuatwa ili uwezo ufike viwango vya chini vya Serikali ni kutumia Serikali za mitaa.

Maoni zaidi kutoka kwa watu mbalimbali - Yaani tulipomaliza kulikuwa na maoni tofauti tofauti. Ya kwanza, malipo ya waliostaafu yafanyiwe katika tarafa na sio kwa ofisi ya wilaya ilivyo sasa. Kiti cha Urais kiwe na vipindi viwili vya miaka mitano peke yake. Mbuga za kuhifadhi wanyama zirudishwe kwa Serikali za mitaa na pia jina "National Park", liondolewe.

Kumbuniwe tume ya kujadili mishahara ya wabunge. Ikiwa mtu aliyestaafu amefariki, yafaa mipango ifanywe ili mjane apatiwe malipo hayo bila kuchelewa. Maofisa wa utawala wawe wakichaguliwa na wananchi, yaani kama Sub-chiefs na Chiefs wawe wakichaguliwa na wananchi. Masanduku ya kupigia kura, yafaa yawe na uwazi - yaani transparent ballot boxes ili kuwezesha kuona vile idadi ya kura inaongezeka.

Waganga wa kienyeji waruhusiwe kufanya utafiti katika madawa. Mbunge akichaguliwa kwenda bungeni, abaki vilevile kama mbunge na asiteuliwe kuwa waziri kwa sababu hatawatetea waliompigia kura lakini atakuwa upande wa Serikali.

"Mtu mmoja kazi moja" - Kuwe na uhuru wa kuabudu lakini uwe na mipaka. Kuwe na klabu ya pombe ya minazi, vile watu walikuwa wanapendekeza. Wanaogombania viti vya Udiwani au Ubunge lazima wawe wazalendo wa eneo hilo. Wasiwe watu wa kutoka nje.

Walimu wawe wakipatiwa uhamisho baada ya kukaa katika shule kwa miaka mitano. Mfanyikazi wa Serikali asiruhusiwe kufanya biashara ya aina yeyote kwa maana hii huongeza ufisadi zaidi katika kupotea kwa madawa (Kitaita). Wastaafu wapewe pesa zao haraka iwezekanavyo baada ya kustaafu na isichukue muda mrefu. Kusiwe na haki ya kuuza mashamba kwa makabila mengine. Wauzaji wa jumla (wholesalers) wasiruhusiwe kuwa na biashara nyingine kado ya hiyo. Wenye biashara katika ardhi zao (plots) wawe na malipo madogo.

Umri wa wale wanaostaafu upunguzwe hadi kufikia miaka arobaini na tano. Iwapo nafasi ya kazi imetokea katika sehemu atokapo mwenyeji, basi afikiriwe kwanza, pasiwe na mtu kutoka nje kuchukua nafasi hiyo. Tender ikitolewa yafaa ichukuliwe na wenyeji wa mahali hapo isichukuliwe na mtu kutoka mahali pengine. Uteuzi wa Ma-judge uondolewe. Kuwe na kibali maalumu kwa watu wawili wanao oana kutoka kwa daktari kwa ajili ya kuzuia ukimwi.

Wanaoajiliwa katika Mahoteli ya watalii na Mbuga za kuhifadhi wanyama, idadi kubwa ya waajiliwa yafaa wawe wa kutoka sehemu hiyo hiyo yaani wenyeji. Walimu wa shule za vidudu (nursery) wawe wakilipwa na Serikali kwa kazi yao ngumu. Wale ambao wamepitiwa na umeme mashambani mwao, wapewe umeme bila masharti yeyote. Nafikiri kwa hayo machache nasema asanteni kwa kunisikiliza.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Martin. Nikuulize swali tafadhali; Ulisema- sijui kama nimesikia vizuri? That women should have a certain percentage in Parliament? What percentage?

**Martin Mwande:** Nilikuwa nasema ikiwezekana kila wilaya iwakilishwe na……

**Com. Kabira:** Kila wilaya, kila district?

**Martin Mwande:** Kila district.

**Com. Kabira:** Should have one woman representative?

**Martin Mwande:** Yes.

**Com. Kabira:** Thank you very much. The other one is on the sale of land. You are saying that one should not sell land to anybody belonging to another tribe? So you want to say that Kenyans should not have a right to live anywhere?

**Martin Mwande:** No. Haja yangu nilikuwa nasema, kwanza kuwa pale pale katika ile shamba inauzwa, kuna watu wana uwezo ambao wanaweza kununua lile shamba, wapatiwe nafasi ya kwanza.

**Com. Kabira:** Okay, wapatiwe nafasi ya kwanza?

**Martin Mwande:** Wapatiwe nafasi ya kwanza. Kama kuna kukosekana , ndio ijulikane ni kwa nini na sababu ijulikane. Lakini asiende kuchukuliwa mtu kutoka nje na kuna watu hapa wana uwezo wa kununua lile shamba.

**Com. Kabira:** Okay. Asante sana. Tutaenda kwa mtu wa tatu, Ayubu. Bwana Ayub Mjomba?

**Ayub Mjomba:** Nashukuru kupata nafasi hii, majina yangu ni Ayubu Mjomba na ninawakilisha maoni ya wanakamati wa Chavia (inaudible) land scheme pamoja na Mwachambo land scheme ambazo zina-cover locations mbili Chavia pamoja na Mwachambo. Maoni yao yanaanza na ardhi.

**Com. Kabira:** Umeandika hayo kwa hiyo karatasi?

**Ayub Mjomba:** Nimeandika.

**Com. Kabira:** Umeandika hayo maoni ni ya akina nani?

**Ayub Mjomba:** Eeh nimeandika.

**Com. Kabira:** Asante.

**Ayub Mjomba:** Kwanza wanaomba kwamba mambo yote yanayohusiana na ardhi yawe yanawakilishwa kutoka mashinani,

kutoka sub-location, location kwenda division hata ndio kufikia juu, sio kutoka kwa Commissioner of lands. Pia tunasema rasilimali zilizoko kwenye ardhi ikiwa ni misitu, minerals, maji na mengineyo yote pia ziwe zinapata idhini ya watu kutoka mashinani kama zitatumika.

Fedha zitakazopatikana kutokana na license ya kutumia rasilimali kama hizo ziwe pia zinagawanywa kwa viwango kuanzia mashinani, tumependekeza kama ishirini kwa mia kwanzia sub-location, location, division, district halafu Central Government. Ardhi lazima iwe ni ya watu wa eneo linalohusika na Serikali isiwe na ardhi- ardhi ni ya raia kutoka mashinani. Serikali isiruhusiwe kuwa na land ama ardhi lakini iwe mkononi mwa raia kutoka National Parks ziendelee kuweko na pia game reserves ikiwezekana.

Ikiwa watu wataongezeka na kuhitaji ardhi zaidi, basi kupitia mashinani, sehemu ambazo zimepewa ardhi kwa mfano, sehemu kubwa kubwa kama shamba za mikonge au ranches zikatizwe ili raia wapatiwe sehemu hizo. Jambo lingine ni kwamba Land Consolidation Act iondolewe kabisa - Isiweko. Tunakubali adjudication peke yake.

Tukiingilia upande wa tawala, tumependekeza kwamba kuanzia Sub-chief, Ma-chief wawe ni watu wa kuchaguliwa na watu, na ki-administration, tungependelea kwamba district level iwe na baraza lake - yaani utawala uanzie kutoka district level.

Tumesema kwamba Serikali kuu iwe chini ya Executive President ambaye atachaguliwa na Wakenya wote na asiwe mbunge wa sehemu yeyote na iwe ni kwa term mbili za miaka mitano peke yake – yaani jumla ya miaka kumi na asizidi hapo. President anaweza kutaja mawaziri wake kutoka kwa MPs ambao wamechaguliwa. Nominated MPs wawe wanawakilisha mahitaji maalum ya kitaifa na wasiwe washiriki wa chama chochote cha kisiasa na ni lazima wachaguliwe kulingana na maoni ya regions – yaani Ki-provinces.

President asiwe juu ya sheria - yaani above the law au hatakuwa na uwezo wa kusimamisha Bunge au kuliitisha bali Bunge lenyewe liwe na uwezo wa kufanya kazi zake kulingana na committee watakayochagua. Pia tumesema President asiwe na uwezo wa kuajili Judges, Governor wa Central Bank, Auditor General, Commissioner of police na Chief of General Staff. Hawa waachiwe Bunge.

Nyadhifa zingine za watu wa wizara mbalimbali, - zile parastatals, ziachiwe ministries zinazohusika. Tukienda sehemu ya uchaguzi tunasema kwamba, political parties ikiwezekana sizizidi tano. Na pia kukubalike independent candidates, - kama mtu atajitokeza kutaka nafasi ya President ama kiti chochote, sio lazima awe mwanachama wa chama fulani cha siasa. Jukumu la Central Government, ama Serikali Kuu, ni kwamba iweze kutoa bure elimu ya kutoka nursery mpaka form four. University ziwe zikichagua Chancellors wao wenyewe na pia Boards.

Serikali pia itoe bure madawa na aina yeyote ya matibabu au health kwani ni jukumu la Serikali ya kulinda maisha pamoja na

mali za raia. Ni jukumu la Serikali kugawa maji, power, telephone na kuleta mambo kama haya karibu na watu. Sio kwamba saa ingine watu waitishwe kutoa pesa nyingi, kuvuta kama ni moto ama maji wenyewe. Serikali kuu ilete hizi karibu na watu halafu mtu anayetaka kuweka nyumbani kwake, atoe pesa tu ya connection. Pia iwe ni jukumu la Serikali kuu kujenga barabara hizi kubwa kubwa zote na Serikali za mitaani kujenga barabara ndogo ndogo za kuingia mitaa yao.

Twataka Serikali kuu pia iwe inaheshimu raia wake bila kujali hali na mali. Kwa sababu kwa wakati huu tunaweza kuangalia kwamba mtu aliye maskini saa ingine anaweza kuteseka kwa mambo ambayo hajiwezi kwa sababu hana fedha labda za kuajili wakili ama mambo kama hayo. Kwa hivyo kuna utesi mwingi kwa raia wa kawaida - haheshimiki mbele ya mapolisi na kadhalika. Kwa hivyo tungetaka raia wa Kenya bila kujali hali na mali yake aheshimiwe kama binadamu. Vile vile hali ya utamaduni udumishwe.

Kwa hayo machache ndio hao land committees kwa niaba ya land committees kwa locations mbili nitapeana memorandum ambayo wameandika.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Mjomba na nina swali pia. Ulisema tuwe na political parties kama tano? Tutachagu aje hizo tano? Utarudi huko ujibu ili watu wasikie. Unajua leo tuna forty two yaani tuna political parties arobaini na mbili. So how do we get five?

**Ayub Mjomba:** We want five.

**Com. Kabira:** So what do we do with the others? We de-register them?

**Ayub Mjomba:** Yes.

**Com. Kabira:** How do we choose which one to de-register?

**Ayub Mjomba:** Hapo hatujapendekeza ni ipi lakini ikiwa sheria itakubalika hivyo basi……

**Com. Kabira:** Watajua vile watafanya?

**Ayub Mjomba:** Labda wananchi wenyewe wanaweza kuwa consulted kuziondoa.

**Com. Kabira:** Asante sana. Nitauliza Commissioner Tobiko ajitambue kwenu kwa nyinyi kwa sababu amekuja amechelewa.

**Com. Keriako Tobiko:** Hamjamboni nyote. Kwa jina naitwa Keriako Tobiko na mimi ni Commissioner kwa hii Tume ya

kurekebisha Katiba.

**Com. Kabira:** Okay asante Tobiko. Tutamuita mtu wa nne na huyu ni Mr. Raphael Nganyi.

**Raphael Nganyi:** Mimi ni Raphael Nganyi kutoka Bura sub-location. Tulikuwa na memorandum yetu lakini mwenzangu hajaja. Hata hivyo nitajaribu kuzungumza yale ambayo pengine walizungumza. Jambo la kwanza ni utawala: Utawala uwe wa majimbo. Tuwe na Serikali ya majimbo na katika hii Serikali tumeamua ya kwamba Bunge iwe na uzito zaidi kuliko Serikali. Na katika utawala huo huo, tukaona kwamba Chiefs na Ma-sub-chiefs wawe wakichaguliwa na wananchi ndipo waandikwe na Serikali. Wakisha andikwa na Serikali, chiefs wawe wakibadilishwa au kupewa uhamisho katika district yao. Na hao ma-chiefs, akiendelea kuwa transferred, baadaye apewe promotion awe naibu wa Mkuu wa Tarafa. Cheo hicho kiende mpaka kimalizikie kwa naibu wa District Commissioner.

Tukija katika umiliki wa rasilimali. Katika nchi yetu, tukiangalia katika ramani unakuta ya kwamba Taita Taveta district, sitini na mbili kwa mia ni mbuga za wanyama. Hizi mbuga za wanyama zipunguzwe, sehemu zingine zipewe wananchi waweze kuzitawala. Halafu zile ambazo zilikuwa zinaitwa National Parks, badala ya kuwa National Parks ziwe game reserves ili wananchi katika district hiyo waweze kufaidi kwa kile kitachopatikana kwa rasilimali hiyo.

Mashamba makubwa ya mikonge kwa mfano yale malipo yanayotoka kwa mashamba ya mikonge, yasiende kwa Serikali kuu kabla hayajapita katika Serikali ya wilaya ndiposa kile kitakachopatikana wagawanywe - 50% iende kwa Serikali kuu na 50% ibaki kwa Serikali ya wilaya. Tukija kwa upande wa ugawanyaji mamlaka. Kama wakati watu wameandikwa kazi, iangaliwe kwamba pahali kunapoandikwa kazi, 85% wawe ni wenyeji ambao wanaandikiwa kazi pale.

Tukija katika umiliki wa ardhi, tunaona ya kwamba license kwa mashamba makubwa makubwa, yanatoka kwa Serikali kuu. ………kuja ku-settle au kukaa, akipewa aje apitie kwa County Council halafu county council impe ruhusa ya kwenda kuingia pale akipewa kitu kama lease au muda wa kukaa pale.

Tukija katika upande wa elimu, Serikali iweze kuwalipia watoto karo – walisema elimu ni ya bure. Serikali iweze kuhudumia watoto kwa elimu kwanzia standard one mpaka form four level. Ni hayo tu kwa leo, mengine yalikuwa katika hiyo memorandum na pengine mwenzangu akija ataweza kuitoa. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante Bwana Raphael. Sijui kama mwenzako ako karibu. Lakini yule atafuata ni Mwatila Salim.

**Mwatila Salim:** Haya yafuatayo ni maoni yangu kuhusu urekebishaji wa Katiba ya Kenya. Katika Katiba ambayo tunaitarajia, kusiwe na mwananchi yeyote aliye juu ya sheria na kila mtu atii sheria na ahukumiwe akikosa, kusiwe na upendeleo wowote.

Rais: Rais wa Kenya awe ni Mkenya asili asiwe ni mtu aliomba uraia na atumike vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Rais asiwe mbunge na asiwe akiitwa "Mtukufu Rais" ila aitwe "Mheshimiwa Rais." Wabunge wasiwe wakichaguliwa Mawaziri ili wawe na nafasi ya kuangalia Serikali iliyoko mamlakani. Mawaziri wachaguliwe kati ya Wakenya walio na ustadi wa mambo tofauti tofauti kwa kila wizara. Lakini wawe na wakenya ambao wako na moyo wa kujenga taifa sio hao mafisadi. Rais asiwe akichagua Ma-judge ama Mkuu wa sheria. Kuwe na tume ya kuwachagua wanasheria. Kenya police iwe chini ya wizara ya mambo ya ndani pamoja na magereza.

Kuwe na ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ataongoza Serikali na atoke kwenye chama ambacho kilipata kura nyingi. Serikali za wilaya zipewe uwezo zaidi wa kupata kodi kwa ajili ya maendeleo ya ile wilaya.

Elimu: Elimu iwe ya lazima kwa kila mtoto wa Kenya- hasa elimu ya msingi, kwanzia darasa la kwanza mpaka la nane. Elimu ya Sekondari itiliwe mkazo katika sehemu zingine ambazo ziko nyuma ili Kenya isiwe na sehemu zingine zinaendelea zaidi na zingine zinakuwa nyuma kwa ajili ya elimu.

Mbuga za wanyama: Asilimia hamsini iliyolipwa kwa mbuga ibaki kwa wilaya inayohusika. Pia hapa nilikuwa nimesema kwamba kwa mfano Taita Taveta, asilimia kubwa sana ya ardhi ya Wataita imechukuliwa na National park. Hiyo haikuwa ni maoni ya Wataita bali ilikuwa ni maoni ya Wakoloni wakati ule uliopita na kwa hivyo Wataita wakawa wamenyimwa sehemu kubwa ya uzalizaji mali kwa ardhi. Kwa sababu ardhi ndio kila mmoja anatumia kuleta maendeleo. Kwa hivyo mbuga ya Taita ama ya Tsavo National park ipunguzwe sehemu moja igawie wananchi na ile itakayobaki iendelee kuwa mbuga. Tena mapato yawe yakibaki sehemu kubwa kwa ajili ya kuendeleza wilaya hii ya Taita.

Maji ya Mzima,- 'Mzima springs' yamekuwa yakienda Mombasa kwa muda wa miaka hamsini na hakuna chochote tunachopata kama Wataita. Hiyo rasilimali ambayo Mwenyezi Mungu aliweka hapa Taita haiwafaidi Wataita. Kwa sababu maji yanapita hapa inaenda mpaka Mombasa na Wataita wengi wanapata shida sana kuhusu habari ya maji. Ni jambo la kusikitisha sana.

Hakuna la muhimu kama kilimo: Kilimo kimekuwa sasa kinazorota sehemu nyingi kwa sababu Serikali haijatilia umuhimu kabisa habari ya kilimo na ili hali ndio uti wa mgongo wa nchi. Bila chakula, nchi inakuwa na shida na hapa kwetu kilimo kiko nyuma sana.

Afya: Kuwe na madawa kwa kila kituo cha afya ili wananchi wakiwa na matatizo waweze kusaidika haraka. Kila mwananchi ni haki alindwe na Katiba ya nchi.

Ufisadi: Mtu akipatikana mfisadi afungwe jela na mali aliyoipora ichukuliwe na kuwa mali ya umma. Mimi kama Mtaita Katiba initambue kama Mtaita na mila zangu vile ziko tangu zamani.

Imani ya dini: Uhuru wa kuabudu. Mimi napinga uhuru wa kuabudu kwa watu ambao wanaabudu mashetani. Hilo jambo ni jambo la kusitikisha sana, kwamba sheria ambayo iko sasa inawapa watu ruhusa waweze kuabudu hata mashetani,- ambapo ni kinyume cha sheria kabisa. Kwa hivyo mimi napingana na haya mambo kabisa.

Sheria ya Islamu: Mimi ni muislamu, waislamu waongozwe na kitabu chao kitukufu - Koran. Wasomi wakuu wakiislamu wawe wakichagua S*heikh* mkuu ama M*futi mkuu* na pia kuchagua *Ma-kadhi* kwa ajili ya kutatua matatizo mbalimbali ya waislamu. Kuwe na uhuru wa dini - badala ya uhuru wa kuabudu kuwe na uhuru wa dini.

Katiba ijayo tungependa iwe ya majimbo. Majimbo yatafanya kuwe na mashindano kwa kila jimbo kusiwe na vile mambo yalivyo sasa. Kuwe na uhuru na haki kwa kila mtu kujisikia yuko sawa katika nchi yake na kusiwe na ubaguzi wa ukabila. Hii mambo ya "lease holdings," mashamba kama haya yanapatiwa ati lease ya miaka tisaini na tisa! Sasa hiyo ni karne hiyo - hilo ni jambo la hatari sana kuwafanya watu wengine wanazidi kuwa matajiri na wengine kuwa wanyonge. Haya mambo yaondolewe.

Ajira hapa Taita ni chache sana. Tuko na sehemu chache za kuajili watu na watu wengi wana ajiliwa si wenyeji wa hapa.

Vyama vingi vya kisiasa ziendelee kuweko. Mbunge na diwani wawe wakichaguliwa bila chama - yaani kuwe na uhuru, unaweza kusimama na ukachaguliwa bila kusimama na chama chochote isipokuwa pengine Rais ambaye ni sharti awe na chama.

Chifu achaguliwe na wananchi na Katiba ijayo iwe katika mfumo wa elimu - yaani iwe ikifundishwa kwanzia shule ili kila mmoja ajue haki zake kwanzia akiwa mtoto kuendelea mpaka mbele. Yangu nafikiri ni hayo asante.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Mwatila.. Ulisema elimu ya Primary school iwe ya lazima?

**Mwatila Salim:** Elimu ya Primary school ya msingi iwe ya lazima kwa watoto wote wa Kenya.

**Com. Kabira:** Ukikosa kulipa?

**Mwatila Salim:** Kulipa? Serikali ndiyo itasimamia haya mambo.

**Com. Kabira:** Kwa hivyo unasema iwe free and compulsory. Iwe lazima na iwe free pia.

**Mwatila Salim:** Naam. Ilipwe na kodi ya wananchi.

**Com. Kabira:** Okay, asante. Bwana Morris Munyaka.

**Morris Munyaka:** Kwa majina yangu naitwa Morris munyaka nina na-present maoni ya dini ya wa Seventh Day Adventists ama ya Wasabatu. Haya ni maoni ya washiriki wa kanisa. Washiriki thelathini hivi. Tulikuwa tumeketi pamoja, tukajadiliana na tukaona ya kwamba sheria iwekwe katika Katiba ya kulinda haki ya mwenye kuabudu ama haki ya kimsingi ya kuabudu maana tunaona kwamba kuna free worship. Lakini utaona kuwa watu wengine ambao wanaabudu kwa siku ya ijumaa, wengine Jumamosi na wengine Jumapili na kwa siku hizi tatu za kuabudu ni moja tu ambayo imewekewa "priviledge"- kama hii ya jumapili. Hawa wa jumamosi na ijumaa, hawajawekewa kimsingi yeyote; akikosa kuelekea kazini anakatwa hiyo siku. anakatwa siku. Kwa hivyo tunaomba ya kwamba Katiba ijayo itulinde na ituweke uhuru kwa siku hii ambayo tunaabudia Kwa mfano utakuta kama ni mwanafunzi ambaye ako shuleni, imefikia ni siku ya jumamosi ya kwenda kufanya ibada yake kwa Mwenyezi Mungu, anakatazwa asiende katika ibada. Utakuta wazazi wengine ambao wanataka kwenda katika ibada, wameambiwa kwamba waende katika mikutano kama ya P.T.A, mikutano ya fund raising. Jumamosi imewekewa vitu vingi ambapo mwabudu wa siku ya jumamosi anashindwa atafanya nini. Kwa hivyo mambo kama hayo, tumeona ni kwamba yawalinde wale ambao wanaabudu siku ya jumamosi.

Pili, tunaona ya kwamba kiwanda kama hichi kiko hapa chini 'Sisal estate' kinalazimisha mtu kama hataenda kazini basi atakuwa nje ya *wire* - maana amefutwa kabisa. Isipokuwa amewekewa tu hiyo siku moja ya jumapili. Lakini kama Muislamu na huyu Mu-SDA hawana nafasi kabisa ya kushiriki katika ibada zao za kawaida. Kwa hivyo hapo ndipo tulikuwa tunaomba sheria pia ije imlinde isije ikabadirishwa kabisa. Sheria pia imlinde hata huyo wa jumapili na ijumaa. Hayo ndio maoni tulikuwa tumeafikiana kwa pamoja, tukayaweka katika memorandum na ndiyo hii tuliandika hapa.

**Pascal Nyambu:** Asante sana Bwana Munyaka. Mr. Pastal Nyambu. Pascal Nyambu ako? Okay.

**Pascal Nyambu:** Mimi ni Pascal Nyambu na ninawakilisha Mwatate Division of Disabled Group. Nitaanza kusoma. "Walemavu kwa jumla tumetengwa na kudharauliwa sana kwa hivyo sisi tuliketi na tukaamua kuwa kwa kila uongozi na idara nchini Kenya tupatiwe Waziri na afisi yake ili kushughulikia mipango na maswala ya kujali walemavu katika nchi nzima na hivyo mbunge wa kuchaguliwa au kuteuliwa awe ni mlemavu. Ikiwa tuwe na Mbunge awe amechaguliwa na kuteuliwa na awe ni mlemavu. Hii ni kwa ajili ya ufisadi na kudhulumiwa, sisi kama walemavu tunavyofanyiwa, - kwa mfano kutukanwa na kuitwa "wasiojiweza" na kadhalika. Simu ziwe za kiasi za kufikiwa na kila mlemavu yeyote yule. Kila tarafa iwe na shule ya kuweza kufundisha walemavu na elimu iwe ya bure kwanzia darasa la kwanza hadi vyuo vikuu.

Walemavu tupewe haki zetu. Kwa mfano, tujengewe majumba ya kuendeleza miradi yetu na tuheshimiwe sawa na wale wazima. Tusibaguliwe kikazi na tuchukuliwe sawasawa na wale wengine. Kusiwe na kukosana kati ya baba, mama na hata wale wengine juu ya ulemavu. Mzazi yeyote mwenye mtoto mlemavu anastahili kumuelimisha mtoto huyu bila ubaguzi wowote. Kusiwe na pingamizi yeyote kwa NGOs watakaojitolea kusaidia walemavu. Miradi yote ya walemavu isajiriwe na Serikali

kupitia kwa wizara itakayoteuliwa kwa maswala ya walemavu.

Tutengewe ardhi na kusajiliwa kwa walemavu kuanzia mashinani. Wakati wa kupiga kura, mlemavu apewe nafasi ya kwanza nchini Kenya. Serikali ya Kenya tunataka igeuzwe na iwe ya majimbo. Ikiwa ni Waziri Mkuu. Ardhi zirejeshewe kwa wananchi asili. Kifungu kinachosema "Mkenya anaweza kukaa mahali popote" kiondolewe na kiwe "mwananchi awe katika mahali pake pa asili." Bunge lisiwe na jukumu la kurekebisha Katiba kwa vyovyote vile, iregeshewe kwa wananchi wenyewe. Usalama wa taifa ulindwe na Katiba.

Bunge iwe na mamlaka na amri juu ya jeshi. Vyama vya kisiasa viwe vitatu nchini Kenya. Mbunge akichaguliwa awe ni mbunge pekee. Ni kwa sababu Mbunge akichaguliwa tu, hurundikiwa kazi nyingi hata akawasahau watu ambao wamemchagua na maendeleo kwa ujumla. Waziri akichaguliwa, achaguliwe kulingana na kisomo na elimu na wizara itakayomfaa. Mamlaka ya nchi iwe mikononi mwa mwananchi mwenyewe.

Mbuga za wanyama wa pori, zirejeshwe kwa Serikali za Mikoa. Mwenyekiti wa baraza, achaguliwe na wananchi wenyewe kwa kura. Kura zihesabiwe katika vituo vya kura. Kuwe na haki za kitamaduni na zilindwe na Katiba. Kusiwe na uridhi wa kupokezana vyeo vya Urais bali kupigwe kura kumchagua. Kuwe na uchaguzi tofauti wa Ubunge kado na wa Urais. Rais akiwa mwanamume, makamu wake awe mwanamke." Asanteni

**Com. Kabira:** Umemaliza? Okay asante sana.Tutamuuliza Mr. Daudi Nyamae.

**Daudi Nyamae:** Mimi kwa jina naitwa Daudi Nyamae na shida ambayo imenileta maoni yangu ni kuhusu ardhi kwa upande wa survey. Land Board imepewa jukumu kubwa sana hivi kwamba utakuta mtu anakaa Wundanyi ndiye ofisa wa land na ndiye anauza ardhi katika reserve akishirikiana na ma-chief na ma-sub-chief na wafanyi kazi wa Land Board.

Mimi nikiongea namna hiyo ni kwa sababu nilikuwa karibu kunyang'anywa shamba langu na ofisa mmoja wa mashamba. Nilipoenda kwa ofisi yake na kumuonyesha kijitabu changu cha shamba, alikipasua pasua baada ya kuniambia kuwa nimeiba hicho kijitabu. Kama sio DC wa Wundanyi aliyeingilia kati, ningepoteza hilo shamba langu. Hii ndio sababu ninalia sana kuhusu mambo ya ardhi. Kuhusu Machifu na Sub-chifu, tungetaka wachaguliwe na wananchi. Yangu ni hayo tu.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Nyamae, thank you very much, utajiandikisha huko kwa msichana yule ako nyuma yako. Asante.Mr. Kepha Nguli.

**Kepha Nguli:** Asante sana kwa nafasi hii. Kwa majina mimi ni Kepha Nguli, na memorandum yangu itafuata baadaye kwa hivyo nitaongea kwa kifupi tu – sitachukua muda. Kitu cha kwanza, naomba Tume isitilie maanani memorandum zozote ambazo zimetumwa na vyama vya kisiasa. Kwa maoni yangu tunaandika Katiba ya kutawala Wakenya na sio ya kutawala vyama. Tukitoka hapo, tunaomba Serikali iwe ya majimbo. President asiwe MP na nguvu zake ama powers ambazo President ako

nazo sasa, zipunguzwe.

Judges wachaguliwe na Parliament. AG asiwe mwanachama wa kile chama kinachotawala na ateuliwe na Parliament. Parliament ijitawale yenyewe na itengeneze utaratibu wake na fedha zake. President pia asichague Permanent Secretaries, Chief of General Staff, Commissioners of Police na hao wengine.

V.A.T. itozwe kutoka kwa factory ama kwa port of entry. Kwa sababu hii " staggering" itolewe kutoka kwa wholesalers na kwa maduka kwani inaongeza ufisadi. Statehouse Controller asitoke kwa ile kabila ambayo President anatoka. Government isifanye biashara – itawale; nikisema hivyo ninasema vitu kama Power & Lighting, Telkom, Post-Office, KPA, hizo zote ziwe ni private companies. Hapo Kenya itapata ushuru wa kutosha wa kuendeleza nchi hii. Positions zozote za kuchaguliwa - elected positions, watu wa-serve for two terms na waachie wengine. Yangu ni hayo machache memorandum nitatumana. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Kepha. Na tutamwita Elizabeth Mwabingu.

**Elizabeth Mwabingu:** Asanteni sana kwa fursa hii. Kwanza tulikuwa tunazungumzia mali ya asili. Wananchi wamelalamika sana kuhusu mali ya asili, wanataka irudishiwe mwananchi wa pale pale. Ikiwezekana percentage imfae mwananchi aliyoko mahali pale kunatoka natural resources. Iwe kunaweza kugawanywa mugawanyo mwananchi wa pale aweze kufaidika. Naja kwa political parites. Wananchi waliamua kuwa vyama vya kisiasa visajiliwe mpaka viwe vitatu ndio vipate nguvu za upinzani mkali. Uraia: Mwananchi aliye mzaliwa wa Kenya aweze kupewa uraia bila tashiwishi, bila swali - Sio leo anapelekwa kwa DO, wapi wapi wakati yeye ni mzaliwa wa pale. Hata kama mzazi mmoja ni wa nje, awe mama au baba, na apewe uraia bila swali. Pia mtoto ambaye amezaliwa na mzazi mmoja ambaye ni Mkenya na awe atarudishwa nyumbani Kenya basi awe mraia wa Kenya. Pengine kuna msichana amekwenda amezaa huko na ni wa hapa Kenya, hajaolewa, amezalishwa pengine na foreigner anastahili kupewa uraia bila swali.

Umilikaji wa ardhi: Kuwe kutaandikwa katika title deed jina la mama na la watoto wote wake. Kama vile watu wanavyoajiliwa kazini wanaandikwa "next of kin," hata hivyo pia kwa title deed kuandikwe "next of kin" kwa maana akina mama wananyanyaswa sana, mashemeji wanaobakia wanachukua ile priviledge kumpokonya yule mama mali yake.

Freedom of movement: Mwananchi awe na haki ya kuishi mahali popote Kenya. Lakini kama si mkaazi wa pale aishi kwa maelewano - waelewane ataishi kwa muda gani, - ikiwa ni kazi aweze kuishi pale.

Haki za akina mama. Tunanyanyaswa kutoka nyumbani, hata Serikali mahali inapostahili kutuona bado tunazidi kunyanyaswa. Kama mahospitali, sijui pengine nyinyi ni watu ukishapata ubunge kule, hustahili hata kufika hospitali ya Voi, Makadara ama mahali popote. Jaribu siku moja ufike kwa ward ya akina mama, hapo unakuta mama yuko pale amejifungua na ndio anaambiwa aende akachote maji – Hakuna hata nguo za kuvaa. Unakuta palepale amejifungua, amelala hapo na ameshida

hapo. Kweli huo ni usalama? Unakuta mtoto yule ni delicate na anastahili kuwa mahali pa safi. Uwe ukijifungua pengine private hospitals, mtoto yuko kado, mama yuko kado. Lakini unakuta hospitali zetu, mama yuko pale, mtoto yuko pale na uchafu wake uko pale. Nurse akiulizwa anasema 'si kazi yangu, kama hukuja na mtu ni shauri yako'. Kwa hivyo tuwe na tume za kuweza kuangalia masilahi ya hospitali - local hospitals - sio private ambao mwananchi wa kawaida ndiye anayedhurika sana katika hizi hospitali. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Elizabeth. Tutamuuliza Clara Juma.

**Clara Juma:** Kwa majina vile mumeambia mimi ni Clara Saru Juma, ni Councillor wa Chavia na pia ni mwanakamati wa Mwatate Constituency kwa hii Tume ya kurekebisha Katiba. Nitaanza na mambo ya elimu. Elimu kama vile wenzangu walivyotangulia kusema, nimeungana na wao mkono kwamba elimu iwe ya bure kwanzia nursery hadi Secondary school. Halafu hapo hapo nikaona kwamba hapa kwetu Mwatate kwa hakika tuna Secondary schools nyingi, pia kwa districts hata kwa Mkoa wa Pwani lakini mambo ya hizi shule, tuseme kama colleges na vyuo vikuu hakuna. Kwa hivyo nilikuwa na mapendekezo kwamba kwa kila district tuwe na college, iwe ni ya walimu ama ni ya department yeyote ile lakini tuwe na colleges.

Halafu tena hapo hapo tuwe na vyuo vkuu viwili, kimoja kiwe cha wasichana na kimoja kiwe cha wavulana. Kwa sababu tukiangalia hivi vyuo vikuu ambavyo viko humu nchini, tunapata vyuo vikuu viko sehemu za juu na ni mixed. Kwa hivyo vikifanyiwa utenganishaji wa wasichana na wavulana kado, basi itakuwa vizuri. Na pia sababu ya kusema hivyo kutenganisha kado kado ni kwamba, msichana anaweza kupita vizuri sana na akienda kwa hiyo shule ambayo iko mixed, hicho chuo kikuu, kuna mambo mengi hapo - Kuna ulevi mwingi na kwa yule ambaye hajazingatia hayo mambo, akienda huko anashindwa na mara kwa mara ndio tunaona hawa wasichana wetu wanasema hawapendi kuendelea na masomo. Na tunazidi kupoteza nafasi kama hiyo. Kwa hivyo ndio maana nilisema, au maoni yangu niliomba kwamba Katiba iweke mashule haya haya ya vyuo vikuu.

Nikaja pia kwa mambo ya matibabu. Matibabu ni kwamba Kenya yetu tuna huu mpango ambao unaendelea wa cost-sharing. Lakini cost-sharing kwa hakika si cost-sharing. Imekuwa ni mambo tunajituza tu. Hawa wakubwa-wakubwa ni mahali ambapo wanajipatia utajiri. Na hii cost-sharing kwa hakika unakuta madawa hayapatikani pale pale hospitalini, yanapatikana kwa private-kwa chemists. Sasa mgonjwa akienda pale hospitalini, anaandikiwa madawa aende kununua mahali. Kwa hivyo mimi naomba kwamba Katiba yenyewe, yale madawa yalikuwa yanapatikana pale hospitalini basi yaendelee kupatikana hapo hapo. Na pia nikaongezea, katika hali ya maoni yangu nikaongezea kwamba tunazo District hospitals. Na hizo District hospitals ni kwamba madaktari hawapatikani hapo hapo. Kama ni daktari, tusema kama kwa mfano kama tungekuwa na District hospital hapa Mwatate, daktari anapatikana Voi. Wakufanyia operation, wakufanyia nini! Ni Voi. Lakini within the hospital hakuna daktari yeyote. Kwa hivyo naomba kwamba popote pale District hospital ipo basi daktari wa kufanyia operation kwa akina mama, kwa mtu yeyote yule apatikane hapo hapo tusiendelee kupoteza watu kabla wakati wao haujafika.

Ardhi na rasilimali. Hapa mimi nilijumulisha mambo yote kwa ujumla. Kwamba ardhi yeyote ile, ardhi yeyote ile ambayo iko mikononi mwa Serikali irudishwe kwa mwananchi. Na ikirudishwa kwa mwananchi ni kwamba, mwananchi huyo huyo, kile kipengele ambacho kinasema kwamba kama tunataka kupata title deed na inatumika kwa mambo ya "consolidation" mashamba kulazwa, kipengele hicho cha consolidation kiondolewe - Kwa sababu kimepatia watu matatizo, kimepatia watu shida, wamepoteza mashamba, wamepoteza mali na wengine wamepoteza maisha yao, kwa sababu ya hii Land Consolidated Act.

**Clapping from the audience.**

So, hiyo Act itupiliwe mbali na ikiwezekana mwananchi mwenyewe ajiamue kwamba shamba lake angependa kulaziwa kivipi. Halafu sasa ashirikiane mwananchi na Serikali halafu ndio sasa mambo yataenda sambamba. Si kwamba Serikali iamue, - Aah aah, tunaomba ushirikiano hapo.

**Clapping from the audience.**

Pia kwa upande wa hizi rasilimali ambazo tuko nazo, ni kwamba rasilimali, kwa maoni yangu rasilimali zote ziwe chini ya County council - Ikiwa chini ya County council, mapato yote yatakuwa yakiingia kwa councils halafu sehemu ile ambayo inatakikana kwenda kwa Central Government, basi council ndio itakata percentage fulani kwa kupeleka kwa Central Government, badala ya Government or Central Government kukata pesa hapo halafu inaletea County council.

Kwa hivyo maoni yangu kwa Katiba hii ambayo tunaitengeneza sasa ni kwamba mali yote iwe chini ya County council na percentage iende Central Government. Maoni yangu nmi kuwa kwa hiyo percentage, 70% ibaki kwa County council na 30% iende kwa Central Government. Kwa sababu inaweza kutokea some other councils zitapeleka hiyo percentage fulani na Central Government itakuwa na pesa nyingi sana. Kwa hivyo 70% si pesa nyingi kwa baraza letu, na itakuwa inajaribu kuinua hali ya mwananchi kwa upande wa elimu na mambo mengine kadha wa kadha.

Jambo lingine ni juu ya mishahara ya wafanyakazi wa Serikali. Mishahara ya wafanyikazi wa kiserikali ni kwamba, maoni yangu niliona tuwe na Tume maalum, - tume ya kuangalia au ya kuchunguza mishahara ya wafanyi kazi wa kiserikali. Sana sana hawa wafanyikazi wa kiserikali unakuta hawa watu wa juu juu ndio saa zote wanajiongezea mishahara. Kesho mshahara, mwezi ujao mshahara, mwezi mwingine mpya mshahara! Sasa hawa wengine hapa chini, yeye yuko pale pale. Ndio anang'ang'ana na kazi, kazi nyingi kazi nyingi kazi nyingi lakini haonekani. Kwa hivyo Tume hiyo ambayo itachaguliwa, ni kwamba itaangalia kila wizara. Na si kwamba ni wizara moja, kila wizara, wizara ya elimu, wizara ya kilimo, na wizara zote ziangaliwe kwa mambo ya mishahara. Na kama ni kupandisha mishahara, basi unakuwa ni msimu wa kupandisha mishahara. Ili kwamba kila mtu sasa hapo anajivunia, sio mwaka huu, walimu hawajapata mishahara. Ninatoa mfano kwamba kama hawa walimu wetu, miaka sijui

ni mingapi, bado wanapiga “mark time” na mishahara yao kuongezewa. Kwa hivyo sasa Tume hii nafikiri ikiundwa itajaribu kupunguza zile strikes zinafanyika kazini, itapunguza hizi strikes zinafanyika kwingineko. Kwa hivyo maoni yangu kwa upande wa mishahara ya wafanyi kazi wa kiserikali ni hayo.

Nitaingia kwa mishahara ya wanasiasa; Pia kwa wanasiasa tuwe na Tume maalum ya kuzungumzia mambo ya mishahara ya wanasiasa. Na sote wakati tunasikiza Bunge letu la Kenya, mara kwa mara wao ndio wanajiongezea mishahara - wabunge peke yao. Mbali na Rais, mbali na diwani, kwa kisiasa ni kwamba, sababu niliyosema hivyo ni kwamba Diwani, Rais na Mbunge hao wote ikifikia ni wakati wa uchaguzi, wanapigania viti. Na ikifikia ni kuingia kwa council kwa bunge wapi, wanaingia kwa wakati mmoja. Kwa hivyo ikiingia wakati wa pesa wa mishahara, wabunge wako kando, madiwani wako kando. So, mambo ya mishahara ya wabunge ni ya wanasiasa wote kwa ujumla. Mwanasiasa yote akiingia hapo au tume hiyo ndiyo itakuwa inaangalia mambo ya mishahara ya wanasiasa. Kwa hivyo kwa upande wa mishahara ya wanasiasa, hapo niliomba kwamba tume ichaguliwe. Na tume itakayochaguliwa ni wabunge wenyewe ndio watachagua hiyo tume.

Vyama vya kisiasa: Vyama vya kisiasa kwa hakika mtindo huu tunaoendelea nao sasa - kesho sijui chama kingine kimezuka, sijui kingine hata imekuwa vyama hivi imekuwa hazina heshima. Kwa hivyo maoni yangu katika hali moja ni kwamba tuwe na vyama vitatu. Na vyama vitatu vya kisiasa ni kwamba kimoja kikiingia kwa madaraka au wakati kimeunda Serikali, hiki kingine kina-support na hiki kingine kama hakiko mahali popote, basi kitaweza kuwa kinajaribu kuona ni wapi mahali mambo yamelemaa. Na kama ni kupiga kura sababu ya kuweka vyama vitatu kwa maoni yangu, ni kwamba wakati kama ni mswada umepitishwa na kuna wengine bado hawajaufurahia, basi wakati wa kupiga kura kutakuwa na ku-balance vizuri.

Nikaendelea na kidogo kwa upande wa ubunge. Bunge letu la Kenya kwa sasa hivi, akina mama ni tisa na kwa maoni yangu mimi niliona kwamba kwa sababu akina mama huwa wamejitokeza kupigania viti vya ubunge badala ya kungoja wateuliwa, nilikuwa naona kwamba, akina mama pia tujaribu kutengewa viti kwa Bunge. Na viti hivyo, ikiwa hao wabunge wako mia mbili na ishirini na mbili, basi tungekuwa na wabunge akina mama thelathini na tano badala ya tisa.

Kwa hivyo mimi naomba Bunge lijalo akina mama hao, kama hatutazidi hamsini, kama hatutazidi sitini basi tusipungue thelathini na wa tano. Mimi ndio nilikuwa naomba na nilikuwa naona hivyo. Sababu ya kusema hivyo ni kwamba mama anapita huko na pale, pesa kidogo, huyo anatimuliwa na mzee hapa ambaye ana pesa anaondoka kwa siasa. Kwa hivyo maoni yangu ndiyo hayo.

Kwa upande wa haki za akina mama - huku kukosewa heshima. Kwa mfano mtu wanagombana na mwingine, au mwanamume kwa mwanamume au mwanamke kwa mwanaume wanagombana, lakini jambo ambalo litatumika, utasikia mtu akisema kwamba ‘wewe usinifanyie akili zako kama za mwanamke.’ Kwa hivyo sasa sisi wanawake tunaona tunatumiwa tumiwa namna hii. Mtu amekosana na mwenzake sasa anamwambia ‘wewe akili zako kama za mwanamke.’ Au mtoto amekosa ni wa kiume, ni wa kike, amekosa lakini atapatiwa kichafulia roho kwamba ‘wewe akili zako ziko kama za mama yako.’ Haambiwi akili

zako ziko “kama zangu” au “kama za ndugu yako” ni kama za mama yako. Kwa hivyo akina mama katika hali hiyo niliona kwamba tuwe na tume maalum pia ya kuangalia masilahi ya akina mama kwa upande wa kukosewa heshima, kwa upande wa hizi raping cases. Kwa hivyo nilijaribu kuona tukiwa na tume kama hiyo, itasaidia.

Na upande wa raping cases - hata kwa wanaume. Wanaume wale ambao ni vijana wadogo wanawekwa na mama mwenye umri mkubwa. Pia tume hiyo ijaribu kuangalia mambo hayo. Kama kijana ni wa miaka kumi na nane halafu mama naye ni miaka hamsini na tano. Sasa huyo ni kama amemchanganya changanya huyo kijana kabisa. Kwa hivyo niliomba kwamba tuwe na tume kama hiyo, na pia kuweko na policewomen wa kushughulikia cases kama hizo.

Mwisho ninamaliza na kusema kwamba, kuna hii mikutano ya kimataifa ya akina mama. Mara kwa mara akina mama wanapokuwa na mikutano ya kimataifa basi kuna mambo mengi, - kuna maswali mengi yanaulizwa. Akina mama wanaenda kujadiliana nini? Wanaenda kujadiliana kwamba kuja kupindua Serikali? Wanajadiliana ‘sisi wanaume watuondoe kwa viti vyetu’, ‘wanajadiliana sisi wanaume watutoroshe kwa nyumba zetu.’ Kwa hivyo hii mikutano ya akina mama hii ya kimataifa ninaomba kwamba kwa Katiba hii ijayo kusiwe na maswali mengi mengi. Mama si mwendawazimu wa kukaa na kujadili mambo machafu bali mama ni mtu mwenye heshima anajadili mambo ya kujenga nchi yetu. Kwa hayo machache, nashukuru sana. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Councillor. Nina swali. Ulisema tuwe na at least 35 women MPs.?

**Clara Juma:** Yes.

**Com. Kabira:** Na watachaguliwa kwa njia gani?

**Clara Juma:** Hawa kwa kuweka akina mama thelathini na tano ni kwamba wakati wa uchaguzi, wengine ni lazima watapigania na wataingia. Si ajabu kumi au kumi na watano au ishirini wanaweza kushida na kuingia kwa Bunge. Sasa hizo nafasi zingine ambazo zimebaki ndio watachaguliwa akina mama ambao wengine ni walemavu na pia wale ambao ni wa religious groups.

**Com. Kabira:** Kwa hivyo unazungumza juu ya affirmative action. Tuweke affirmative action tuone tuna wanawake na walemavu na other marginal groups?

**Clara Juma:** Yes.

**Com. Kabira:** Asante. Kuna Laban Lejo.

**Laban Lejo:** Kwa majina yangu ninaitwa Laban Lejo na nitatoa maoni ambayo ni ya watu wa kata ndogo ya Vuzi, - Chavia,

na nitaenda kulingana na mfuatilio ulioko kwenye kijitabu ambacho ni juu ya marekebisho ya Katiba.

Utangulizi: Tunahitaji utangulizi katika Katiba yetu ya Kenya. Utangulizi huo uhusishe kabila zote za Kenya na sababu za kuandika Katiba na mabadiliko yake.

**Com. Kabira:** Tafadhali kuja karibu na microphone.

**Laban Lejo:** Kanuni za kuiongoza sera ya dola. Tunahitaji vyama vya kisiasa visivyozidi vinne.

Ukuu wa Katiba: Tuendelee kuwa na utaratibu wa Bunge kubadirisha Katiba.

Uraia: Sheria za mwanzo kuhusu uraia zinazopatikana katika Katiba zifuatwe.

Ulinzi na usalama. Ulinzi na usalama utawaliwe na Katiba. Rais aendelee kuwa Mkuu wa majeshi yote ya Kenya. Kuhusu vita, Rais ashauriane na baraza la mawaziri. Katiba iruhusu uwezo wa kipekee na mamlaka wakati wa vita na mikasa ya kitaifa.

Vyama vya kisiasa: Katiba ielekeze uundaji, uongozi na tabia za vyama vya kisiasa. Vyama vinavyosajiliwa visipite vinne na vyote vighalamiwe na Serikali.

Miundo na aina za Serikali: Tuendelee na muundo wa Serikali wa Urais. Rais awe na uwezo wa kupitisha jambo baada ya Bunge kulikubali. Rais awe wa nchi nzima na kila mkoa uongozwe na Governor ambaye atakuwa na bunge lake ndogo.

Bunge: Tuwe na Bunge moja la kutunga sheria. Bunge lipige msafa na darubini uteuzi wa Katibu mkuu na maofisa wakuu wa mashirika ya umma. Kwanzishwe masharti ya kimaadili na kitabia yatakayotimizwa na wagombea viti vya bunge. Wananchi wawe na haki ya kumrejesha nyumbani Mbunge wao kwa kuakilisha malalamiko yao kwa Speaker wa Bunge kupitia kamati za mashinani.

Mishahara ya wabunge ijadiliwe na kamati maalum katika ofisi ya Rais. Kuwe na mwongozo wa utaratibu wa kupata mishahara na marupu rupu. Kusiwe na wabunge wateule katika bunge. Kuwe na chambers mbili za bunge. Moja isimamiwe na Speaker na nyingine isimamiwe na Governor.

Mamlaka ya nchi: Katiba ifafanue masharti ya kutimizwa na wagombea wa kiti cha Urais. Kila Mkenya awe na haki ya kugombea kiti cha Urais mradi awe ni mbunge na mzalendo halisi wa Kenya. Rais awe na kiwango cha elimu ya kidato cha nne na juu. Awe na afya nzuri na nidhamu bora. Rais awe na mamlaka kwa vipindi viwili vya miaka mitano. Majukumu ya Rais yaelezwe katika Katiba. Kwa mfano: Rais asiwe na mamlaka yote hasa ya kuwa juu ya sheria.

Katiba itoe kibali na mwongozo wa jinsi ya kumuondoa Rais mamlakani. Rais aondolewe mamlakani akitenda kitendo kisicho halali hasa kutumia mamlaka vibaya. Kwa mfano: Kuzusha vita bila kujali masilahi ya wakenya wasio na uwezo wa kimali wa kukimbilia nchi za nje, - kuweka jamii yake katika nyadhifa za kikazi nchini, kuiba pesa za nchi na kuzihamisha nchi za kigeni. Rais ni lazima awe Mbunge na akishinda Urais, mahali pake pa eneo la ubunge kuwe wazi kupiganiwa ili apatikane Mbunge wa sehemu hiyo.

Kuwe na utawala wa majimbo ambako kila jimbo litasimamiwa na Governor. Bunge la Mkoa likutane na Bunge la Kenya siku mbili za wiki. Kutengewe pesa za kumpa kila Mkenya asiye na kazi na aliye na kitambulisho cha kitaifa kama kiasi cha elfu mbili mia tano kila mwezi kughalamia mahitaji ya kila siku. Katiba iweke mwongozo wa kumshtaki Mkenya yeyote anayeiba pesa za Kenya na kuziweka kwa mabenki ya ng’ambo. Pia wale wanaovunja pesa za mashirika na kuyafirisi wachukuliwe hatua. Serikali ihakikishe hakuna mgeni anapewa kazi ambayo Mkenya anaweza kuifanya.

Mahakama: Mawakili wanaosimamia walalamishi katika mahakama wasipewe pesa za mlalamishi bali mlalamishi apewe pesa hizo kisha amlipe wakili wake. Kuwe na mahakama ya juu zaidi, na pia mahakama ya Katiba. Maofisa wa mahakama wateuliwe na Mkuu wa Sheria wa nchi. Kiwango cha elimu cha maofisa wa mahakama kiwe cha shahada ya chuo kikuu cha taaluma ya sheria.

Serikali za mitaa: Wenyeviti wa mabaraza na Mayor wasiwe madiwani bali watakao viti hivyo wafanye campaign katika ward zote ili kuvigombania. Yaani asiwe mmojawapo wa madiwani. Wenyeviti na ma-mayor wawe wanahudumu kwa kipindi cha miaka mitano. Serikali za wilaya ziwe zikishirikiana karibu karibu na wenyeviti wa mabaraza kwani wenyeviti ndio wanaoelewa shida za wananchi na mahitaji yake. Katibu wa baraza awe chini ya kamati ya baraza. Madiwani wote wawe wa kiwango cha elimu cha darasa la saba au la nane kwenda juu.

Mitihani ya madiwani iwe ya Kiingereza na Kiswahili. Mgombea kiti cha diwani ni lazima awe mzaliwa wa ward hiyo. Na kama ni mwanamke aliyeolewa katika sehemu zingine basi bwanake awe mzaliwa na mkaazi wa sehemu hiyo. Mgombeaji awe ana tabia nzuri na awe ameoa na ana mke au ana bwana. Kuwe na madiwani wateule, waziri wa Serikali za ulaya asiwe na mamlaka ya kuvunja baraza bali Katiba ieleze mwongozo wa kufanya hivyo.

Haki za kimsingi: Katiba ilinde usalama, huduma ya afya, maji, elimu, makaazi, chakula na ajila kama haki za kimsingi kwa wakenya wote. Serikali inayotawala ihakikishwe kwamba Wakenya wote wanafurahia haki zote za kimsingi. Katiba ilinde haki ya mwananchi kupata elimu ya lazima kuanzia shule za msingi hadi kidato cha nne. Pia wasomi wote wa vyuo vikuu wawe wakipewa mikopo na Serikali ya kusoma hadi kumaliza masomo yao.

Huduma za afya ziwe za bure katika hospitali zote za Serikali. Katiba ilinde maadili ya kibinadamu. Uhai wa mwanadamu

usitolewe na mtu yeyote bali Mungu pekee. Kwa hivyo kusiwe na hukumu ya kifo. Serikali ilinde usalama wa raia wote wa Kenya pamoja na mali yao.

**Com. Kabira:** Bwana Laban, uko karibu kumaliza? Kwa sababu utatupatia memorandum, usisome kila sentence.

**Laban Lejo**: Haki ya makundi yanayoweza kudhuriwa. Walemavu walindwe na Katiba na wapewe jukumu sawa na watu wengine wasio na kasoro. Haki za wanajamii na tofauti za kitamaduni, kabila na kieneo zilindwe kwa vile huchangia kwa kiasi kubwa katika ujenzi wa utamaduni wa kitaifa.

Uongozi na matumizi ya mali asili: Rasilimali na mapato yanayotokana na mali asili ya wilaya hiyo, asilimia sabini ya mapato hayo yasaidie maendeleo ya sehemu hiyo na asilimia thelathini iende kwa Serikali kuu.

Haki za ardhi na mali: Sheria zote zinazohusu ardhi zivunjwe kisha watu wa sehemu mbalimbali za Kenya wahesabiwe na kugawanyia ardhi chini ya ulinzi wa Serikali za mitaa. Mazingira na mali asili: Maswala ya uhifadhi ya mazingira yanayopaswa kuingizwa katika Katiba ni; maji na vilivyomo, misitu, mbuga, madini , na wanyama wa pori.

Muundo wa utaratibu wa uchaguzi: Kubuniwe eneo moja la bunge la Kenya. Kenya Constituency ambalo wagombaji wa kiti cha Urais watagombania baada ya kushinda viti vya maeneo yao ya ubunge. Asanteni sana. Ni hayo.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Laban na utajiandikisha. Sasa nitauliza watu wachukue dakika chache. Ukiwa una memorandum na unatupatia, utaje machache ili tuwe na wakati wa kupatia kila mtu azungumze. Kwa sababu leo ninaona tuna list ya watu sabini na tumefikia watu kumi na mmoja. Kwa hivyo tukitumia dakika ile kumi, hatuwezi kumaliza watu wote. Kwa hivyo nitauliza mtaje machache ukiwa una memorandum kwa sababu hiyo ingine tutasoma. Asanteni. Now, Henrita Shali? Ako karibu? Ni wewe. Okay asante.

**Henrita Shali:** Kwa majina yangu ni Henrita Shali na tuko na memo yetu ya 'Zingira na majengo'. Memo ya kwanza ni juu ya shamba la makonge. Lease tumeikataa kwa sababu hii lease imetunyanyasa kwa muda mrefu sasa tunaitwa ma-squatters na tunahamishwa wakati wowote. Tunataka shamba hili lirudishwe kwa Wataita wa Mwatate. Shamba hili halitufaidi kwa rasilimali. Hizo pesa mahali zinalipiwa hatujui. Ramani ya kwanza la shamba la Taita Estate Mwatate, kikao cha kwanza kilifungwa December 1954 hadi February 1955. Mkao wa pili ulikuwa 1957 February to March. Mkao wa tatu shamba ilirudishwa 1962 ambapo plot number yake ni number AG 75893/2/85 (D). Kwa muda huu wote survey ilikuwa inafanywa na nchi ya nje na hakukuweko tofauti yeyote. Tofauti zimetokea kwanzia 1991 na ndio maana tunasema hiyo lease hatuitaki kabisa – tumeikataa. Hatuwezi hata kujenga shule, makanisa, hata nyumba ya mtu ikianguka hatuwezi kuirekebisha. Wale waliohudhuria mkao huo wakati shamba hilo lilikuwa linafanyiwa survey walikuwa ni marehemu Danson Mwanyumba na marehemu Mengo ambao walikuwa ni viongozi wetu wa kisiasa. Marehemu Mwanyumba alikuwa mbunge wa Wundanyi na Mengo alikuwa ni mjumbe

kutoka enzi za zamani.

Rasilimali za mbuga ya wanyama wa pori: Mbuga hizi ambazo zinaitwa National parks, tunaikataa. Iwe game reserve ya Wataita. Kwa sababu hii Park hata imechukua sehemu kubwa kuliko makazi ya binadamu na hatufaidi chochote kutokana na hizo mbuga - Maanake hizo pesa huwa zinalipiwa Nairobi. Madini: Wale wote wageni wanaochimba hayo mawe watoke, wabaki Wataita pekee. Hao nao watoke wakati wowote kuanzia sasa. Tunataka tumiliki sisi wenyewe kwa sababu hatufaidi chochote. Nikisema hivyo hatufaidi chochote, ni kwa sababu kuna wageni wameingia mahali pale kwa madini na wakati Wataita wanaenda kuchimba, wanatolewa ramani ambayo imechorwa Nairobi, hata Mtaita mwenyewe hajui hiyo ramani imetoka wapi.

Maji: Kwa mfano maji ya Mzima springs inatoka Taita Taveta lakini hatufaidi chochote. Kwa hivyo tunataka tuisimamie sisi wenyewe. Hata kama ni kilimo tutafanya kwa urahisi.

Uongozi wa utawala: Tunataka nguvu za Rais zipunguzwe, kuwe na Mkuu wa Majeshi na kuwe na Mkuu wa fedha. Rais asiwe Mkuu wa majeshi tena mkuu wa fedha. Pili, wabunge wachaguliwe kwa kura za siri na Mbunge asiwe Waziri. Waziri pia achaguliwe na wananchi. Ikiwa kunatakikana Waziri basi achaguliwe na wananchi. Councillor achaguliwe kwa kura za siri. Mwenyekiti pia wa County Council achaguliwe kwa kura za siri - Asiwe Councillor pia awe mwenyekiti.

Uteuzi: Wananchi wamekataa mambo ya uteuzi wa siri. Madiwani wachaguliwe kwa kura za siri na wananchi wenyewe. Na pia Councillor akisha kuchaguliwa asiwe na cheo chochote. Anayehitaji kuchaguliwa Diwani awe amesoma hadi form four. Vile vile tunaomba kiwango cha pesa za kujiandikisha kugombea kiti cha udiwani zipunguzwe. Wagombeaji wa udiwani wawe wanapewa mitihani ya lugha ya Kiswahili na Kizungu.

Wagombea viti vya udiwani wawe na mila za kitaifa. Madiwani wakipatikana na kosa waondolewe na wananchi na kuondolewa kwa kura za siri. Na Diwani pia akiwa anachaguliwa, awe ni mtu wa miaka ishirini na tano na kuendelea. Hata Rais ni hivyo.

Wanawake: Wanawake wapewe nafasi za uongozi. Wanawake wakitaka kugombea kiti kama wanao elimu ya kutosha form four yaani kidato cha nne na kuendelea wachaguliwe bila kupingwa.

Afya: Wananchi wanataka Serikali isimamie mambo ya kulipa pesa za hospitali kama ilivyokuwa zamani.

Karo: Wananchi wanakataa mambo ya karo za shule kwanzia nursery……

**Com. Kabira:** Bi. Henrita uko karibu?

**Henrita Shali:** Ndiyo. Kwanzia nursery hadi University. Kila mtoto akienda University apewe marupu rupu kama zamani.

Ushuru wa sokoni. Wananchi wanakataa ushuru wa sokoni maana unanyanyasa.

Walemavu: Walemavu wahesabiwe wakati Serikali inafanya budget kama mradi wao na binadamu kama wengine. Kwa hivyo wapatiwe haki zao. Nimemaliza hapo.

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Henrita. Thank you very much. Na tunauliza Gerald Nzano. Gerald yuko? Hayuko. Tutaenda kwa Victor Maningi.

**Victor Maningi:** Kwa majina naitwa Victor Maningi nimetoka Godoma Mtau sub-location na nawakilisha vijana. Naanza kwa kusema hivi. Elimu ya msingi iwekwe bure na kwa shule ya upili, Serikali itoe nusu ya pesa. Wanafunzi walemavu wapatiwe elimu ya bure kwanzia darasa la kwanza hadi shule za upili. Wapatiwe elimu ya bure.

Nitaenda mambo ya afya. Madawa yapatianwe bure. Nikaja kilimo. Serikali na vijana wanaweza shirikiana na watoe ma-tractors ili kufanya kilimo ambacho kinatakikana hapa Taita Taveta. Katika mambo ya mashamba. Naomba Serikali katika mashamba yote yaliyonyakuliwa yarejeshwe kwa wananchi wa division ile wanaokaa. Hapa katika Bura lodge kuna hii mineral, lakini hiyo mineral, wananchi haiwafaidi. Sasa tunataka Serikali ichukue jukumu ya kuchimba hiyo mineral halafu itoe misaada kwa wananchi wanaokaa hapa. Nitaenda katika ajira za kazi. Siku hizi watu wanaandikwa kazi kulingana na mtu aliyeko mbele ama unayemjua. Lakini sasa tunataka Serikali iandike mtu kazi, - kulingana na level na capacity na standard ya mtu.

Ufisadi: Mwizi, tunataka kama mtu amepatikana na wizi katika Kenya………

**Com. Kabira:** Tafadhali tumia microphone kwa sababu tuna-record. Uje karibu na microphone.

**Victor Maningi:** Akipatikana na makosa, mtu huyo atolewe kwa wananchi halafu achomwe mbele ya wananchi.

**Laughter from the audience.**

Kuna hao wasichana wanavaa nguo karibu na uchi. Na hiyo ndiyo inasababisha zaidi wanaume wanawa-rape. Sasa tunataka mwanamke yeyote atakaye shikwa amevaa nguo fupi, ashikwe na Serikali na afungwe miezi sita.

**Clapping from the audience.**

Kuna hii raping (kunajisiwa sasa). Wacha nizungumzie kunajisiwa hasili. Mtu yeyote atakayeshikwa na kosa la kunajisi lazima apelekwe kwanza apimwe. Kama amepatikana na viini huyo mtu muachilieni lakini mupatieni mtu wa kum-advise. Na kama hana viini kama hana viini, mtu huyo anatakikana afungwe miaka miwili ama mitano.

**Laughter from the audience.**
Namaliza na uongozi. Tungeonelea Rais awe ni kijana, makamu wake awe ni mzee. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Victor kwa hayo maoni na tutamuuliza Matasa Mwazuti. Ako?

**Matasa Mwazuti:** Kwa majina yangu naitwa Matasa Mwazuti. Jambo ambalo napendelea kupendekeza ni kwamba Tume hii itusaidie kwa ajili ya upande wa mashamba. Nikizungumza kwa upande wa mashamba ni kwamba sisi wananchi wa Mwatate ambao tulizaliwa hapa hapa Taita, tumekuwa tukinyanyaswa kwa upande wa mashamba. Kama kwa mfano, baba yangu ama mama yangu na nyanya zetu ni watu waliozaliwa hapa Taita lakini utakuta ya kwamba leo hii sisi ambao tuliobaki, wazazi wetu walitangulia wakaenda mbinguni basi leo hii unakuta kwamba tunaambiwa sisi ni ma-squatter. Hatuna sehemu ya kuweza kumiliki katika sehemu hizi za Mwatate.

Basi ningependa kusema kwamba Tume hii iweze kutusaidia kwa ajili ya kwamba tukaweze kuwa na vibali vyetu vya mashamba yetu ya hapa Taita Taveta. Kwa hivyo napenda kusema ya kwamba ni watu wengi wamezidi kunyanyaswa sana hasa kwa upande wa machifu - wamekuwa wakitunyanyasa sana kwa sababu wao ni watu wame elimika na wakawa na elimu ya juu. Sasa utakuta wazazi wetu wengine hawakuwa na elimu.

Mambo yanaenda yatengenezewa huko sehemu nje na unakuja unakuta kwamba wewe ambaye mzazi wako hakuwa na elimu yeyote, unakuta ukiambiwa kwamba 'hapa huna nafasi yeyote kwa hivyo wewe uondoke maana wewe ni squatter'. Hilo jambo limetuudhi sana katika upande huu wa Taita Taveta. Kwa sababu ni wengi sana wamepata kunyanyaswa kwa njia ya hali hizo. Kwa hivyo tungependa Tume hii ya kurekebisha vile watu wanatakikana wakae, ningeomba itusaidie kwa ajili ya upande wa mashamba yetu.

Na kwa upande wa hizi mahospitali, tumekuwa sanasana tukipoteza watu wengi kwa ajili ya matibabu ya hospitali. Maana utakuta mtu amepeleka mgojwa wake pale hospitali lakini utakuta kwamba ameambiwa kiwango cha pesa ambapo ukiangalia hana hicho kiwango. Tungependelea kwamba kiwango hicho cha pesa kiondolewe na matibabu yetu yarudi kama zamani vile tulikuwa tunaendelea kutibiwa kwa matibabu ya bure. Hilo ni ombi langu ningelikuwa ninaomba, hospitali zirudishwe kama zamani.

Jambo lingine ni kwamba kuna rasilimali zetu ambazo ziko katika hii wilaya ya Taita Taveta, ambazo ni madini. Watu wengi wametoka sehemu za nje na unakuta kwamba vyeti vya kumiliki zile rasilimali zinatolewa sehemu za nje na unakuta mwananchi

wa hapa hapa Taita anajaribu ili aweze kupata hizo rasilimali zao, lakini utakuta kwamba wamekanyangiwa na watu ambao wametoka nje. Kwa hivyo tungelipendelea kwamba, wananchi wa hapa Mwatate, wapewe rasilimali zao na wapewe vibali za kumiliki katika upande wa madini – Maana ni wengi wanatoka na vibali kutoka huko sehemu za nje, unakuta mtu ametoka Nairobi anakuja na kibali chake anakwambia 'hapa kwa huu mgodi nilipewa mimi. Na yule yule ambaye mwenye kuhusika na huo mgodi ataambiwa kwamba hana nafasi yeyote. Kwa hivyo ningelipenda kusema kwamba, tujaribu kusaidiwa kwa sababu sisi ni wazaliwa wa hapa hapa. Tuweze kuwa na vibali vyetu hapa hapa na tuweze kuwa na ofisi za kuweza kuuzia rasilimali za upande wa madini hapa katika wilaya ya Taita Taveta. Kwa hivyo yangu ni hayo na Mungu awabariki.

**Clapping from the audience.**

**Com. Kabira:** Asante sana Mr. Mwazuti. Na Eunice Mwola.

**Eunice Mwola:** Kwa majina ni Eunice Mwola nawakilisha Kishamba location. Na nitaenda kuzungumza ama kusisitiza yale mwenzangu amekwisha zungumzia hapo mbeleni. Mjane ambaye ameachwa, awe akiendelea kupewa ama kulipwa pesa za mumewe kwa maisha yake. Sio kwa miaka mitano kama ilivyo sasa. Unaona ya kwamba mzee amefariki halafu yule bibi wake ama watoto wake ambao wamebaki, anapewa miaka mitano pekee ya kulipwa. Ingewezekana aendelee kupewa maisha yake yote. Pia kuwe na uhuru wa kuabudu lakini kuwe na mipaka. Kwa sababu tukiangalia maisha ya sasa, tunaona watu wengi wameendelea kuabudu vitu ambavyo hazifai ama kama kimashetani. Lakini ingefanya vyema kuwe na mipaka ya kuabudu.

Mtu mmoja awe na kazi moja. Tukiangalia watu wengi wanakuwa na kazi nyingi ili hali kuna wengine wanakosa kazi. Wanaoajiriwa katika mahoteli ya watalii na mbuga za kuhifadhi wanyama wengi wao wawe ni wenyeji wa mahali pale. Hatutosheki pia na ugawanyaji wa Ward kwa upande wa uakilishi wa wabunge na mabaraza. Ukiangalia kama upande wetu wa Kishamba, utaona ya kwamba Kishamba inataka kuunganishwa na Chavia, hii inamaanisha ya kwamba yule mtu atakuwa anawakilisha pale hataweza kujua wale walio mbali pale na hataweza kutimiza yale mahitaji ya wale wakaao pale. Yangu ni hayo. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana.  Eliud Muchalo**.** Eliud, hajarudi? Richard Mwangeka. Tuko na wewe tena mzee wangu hapa. Fanya kwa ufupi sana.

**Richard Mwangeka:** Basi Commissioners, mabibi na mabwana, mimi nimekuja kuakilisha chama cha Shirikisho Party of Kenya. Maoni ni kwamba tunataka Serikali ya *majimbo*. Jimbo ambalo litasimamia rasilimali zake lenyewe kama maji, madini, hata na mbuga za wanyama. Vile vile tungependa Commission hii, Katiba tunayoiandika mpya kwa sababu tutakuwa na *majimbo*, tunaondoa utawala wa mikoa. Tunawaondoa. Kwa sababu tuna Governor, huku chini tutakuwa na mtu wetu - DO hatakuwako, na Machifu hatakuwako. Huku hivi tumepata shida na hawa watu. Tumeona ya kwamba plot nyingi zinazungumzia Wundanyi, zinagawanyiwa huko, huku ni kupeana vijiti tu " fanyeni hivyo". Ndio mzee huyu mmoja amepiga kelele sana hapa

amekosa shamba. Twataka Katiba hii ambayo tunaiandika mpya kila Mkoa uwe na University tatu, uwe na college za walimu tano na kila District iwe na viwanda ili wananchi wapate kazi. Tunataka pia Katiba hii mpya tunayoandika tuone kwamba imerudisha 'Vagrants Act.' Kuna watu tunaishi nao hapa, wamekosa kwao wako hapa - wamejaa Mwatate sana. Hujui ana tabia gani.

**Clapping from the audience.**

Tunataka Katiba tunayoiandika kila hospitali iwe na madaktari watatu, zahanati iwe na daktari mmoja. Kama vile Dispensary Mwatate hapa iwe na daktari – Mara hakuna daktari, kwingine ni mmoja. Ndugu zangu tunataka Katiba ambayo tunaiandika mpya, zile tenders ambazo zinapewa ndugu zetu za barabara za kupeleka vyakula, tenders hizo zipewe the locals watu wa hapa hapa.

**Clapping from the audience.**

Ni barabara imetengenezwa na "*Kaluwanga*." *Kaluwanga* ni wa wapi? Hakuna *Mwadime*? Tunataka Katiba tunayotengeza ndugu zangu iwapo mtu yeyote - hata kama ni President asipeleke pesa nje ya nchi ya Kenya.

**Clapping from the audience.**

Tunaomba pesa IMF, World Bank na pesa ziko nje tele kabisa, zimepelekwa na jamaa zetu. Hawataki sisi tuendelee vizuri. Twataka Katiba tunayoiandika hizi National parks tunazozungumzia, wananchi wapewe ten kilometers ili waweze kutengeza game reserves zao. Kwanza wapite kwetu, ndio waende zalini ndani kule. Tukisema tupewe zote, "aah" tumeomba sana, tunataka Katiba tunayoandika tupewe ten - kama vile Masai Mara wako na game reserve, ndio wako na pesa nyingi. Kwa hivyo tupewe mraba ten kilometers ndani.

Uraia: Uraia upewe Mkenya anayezaliwa pale pale na baba na mama. Ikiwa ni baba wa nje pia mtoto yule apewe. Isiwe ungumu kupigwa madarubini sijui "vetting" sijui "huyu jamaa vile ana hiyo akili alitoka wapi?" Wasomali wanapata vitambulisho Taveta free, sisi twapata shida mpaka tupigwe vetting na uko kwenu hapa Chavia. Hayo ni makosa. Katiba mpya iondoe mambo hayo.

Ukulima: Kuwe na kipengele katika Katiba, kuwa "lazima watu wawe wakilima hata vipi." Kwa sababu mambo haya yameletwa na free-chakula cha msaada ndio kimeharibu hii na watu wakawa wavivu. Katiba hii inayoandikwa kuwe ni lazima watu wawe wakilima - Kama vile ndugu zangu Watanzania, "kilimo cha kufa na kupona." Tulinde haya mahindi ya msaada inayokuja. Ndugu zangu Katiba tutakayoandika tungeona ya kwamba hii mambo ya lease, ninety nine, 999 "nine mara tatu" iondolewe. Imetuadhiri sana. Shida iko hapa ya sisal estate mwaijua.

Vile vile tunataka Katiba itakayoandikwa mpya, Electoral Commission of Kenya wawe wakitembelea kuchukua maoni kwa wananchi jinsi ya kubadirisha mipaka. Sio wakae Nairobi waseme tu, "Tumevunja Kishamba, tunaweka yote iwe ni Chavia location". Si ndiyo ilivyo namna hii sasa? Waliuliza nani? Hawakuuliza mtu! Kwa hivyo Katiba inayotengezwa tuone kwamba Commission ile ambayo ni ya uchaguzi, wawe wakizunguka kuchukua maoni. Kama vile hii maoni, Commissioners mnachukua leo.

Katiba tunayoandika iwe "one man one job." Tumeumia sana watu wa pwani. Katiba tunayoandika mpya tungependa wazee ambao wamezidi miaka sitini na tano wawe wakilipiwa na Serikali ili kuendesha maisha yao. Wawe wakilipiwa na Serikali - sixty-five na kuendelea. Ndugu zangu Katiba tunayoandika tuone ya kwamba, kunakuwa na leaders meeting katika kila district. Leaders meeting ya district mzima, iandikwe hiyo Katiba, lazima kuwe na leaders meeting every quarterly. Tuwe tukijua shida zetu za district hiyo. Hapa tuko "Fua"- tangu tupige uchaguzi mpaka leo hakuna leaders meeting, shida zimejaa tele.

**Com. Keriako Tobiko:** Malizia, malizia ndugu yangu.

**Richard Mwangeka:** Namalizia kwa kusema ya kwamba, Commission hii imeomba kuongezewa muda miezi minane, watumie 0.5 billion - na hiyo ni kodi ya wananchi. Mimi nasema hivi; Commission hawa ni watu waliosoma, kuna Professor Ghai, tuna Professor Wanjiku, kuna watu wote wanajua historia ya Kenya. They simply adapt *majimbo* Constitution. Maanake ilikuwako.

**Clapping from the audience.**

Ilikuwako kwa hivyo hizo pesa zipewe walimu ambao wanalia mishahara.

**Clapping from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Eunice Nyasi.

**Eunice Nyasi:** Kwa jina naitwa Eunice Nyasi. Walemavu tumewachwa nyuma sana na katika maoni yetu, tunaomba Tume ibadirishe katika mambo ya simu. Simu zirejeshwe ambapo walemavu wanaweza kufikia hata mlemavu akitaka kupiga simu, kuna wale wanatambaa chini, afikie apige simu yake mwenyewe. Pia kwa vyoo - hivi vyoo vya public, inatakikana ziwekwe ambapo mlemavu anaweza kujisaidia bila kushika uchafu wowote. Lingine naongezea, wazazi walio na watoto walemavu, tafadhalini mjaribu kuwapeleka katika vituo hivi vya walemavu ambapo wanapata course zao za kujifundisha kama mfano; kushona nguo, kufundishwa kama weaving na kazi kadhalika kadhalika.

Kisha katika Mkoa wa Pwani tuwe na wada la walemavu ambako walemavu wanaweza kuajiriwa kazi. Kwa mfano

wakifungua kama tuseme ni kiwanda cha kazi ambapo walemavu watakuwa wakiajiriwa wakitoka katika hiyo course yao ambayo wamesomea, wataletwa hapo kwa hicho kiwanda chao na wataajiliwa wafanye kazi zao yaani watumie rasilimali za wenyewe kwa ile hali waliyo nayo. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Mama jiandikishe hapo. Ephraim Mwang'ombe. Ndio wewe? Tafadhali usisome hiyo karatasi, fanya hivi, just highlight. Taja zile mambo muhimu kwa ufupi.

**Ephraim Mwang'ombe:** Asante sana. Jina langu ni Ephraim Mwang'ombe na mimi ni diwani wa Kishamba. Kwanza ningeanza na uwezo wa Katiba. Uwezo wa mwisho wa kubadirisha Katiba uwe wa wananchi kupitia kwa national referendum. Yaani wakati Bunge inapofikiria kubadirisha Katiba, waende wapewe uwezo na wananchi kuliko kupitia national referendum.

Pili usalama wa nchi. Vyombo vya usalama vihakikishe usalama wa wananchi wote. Nasema hivyo kwamba training ya ma-askari polisi ambao ndio wanakaa sana na wananchi iwe extended kufikia mwaka mmoja na nusu ili waweze kufundishwa public relations, sheria kidogo isiwe tu kazi yao ni ku-harass wananchi. Iwapo kutatokea hali yeyote ya kutangaza hali ya hatari, basi Bunge liwe na uwezo wa kuidhinisha kutangaza hali hiyo ya hatari.

Namba tatu tuwe na vyama vitatu tu vya kisiasa. Kuwe na mvumo wa majimbo. Kuwe na nyumba mbili za uakilishi yaani Lower House na Upper House. Haki za kumiliki ardhi zibaki kwa mwananchi kupitia trustee ambayo ni baraza la wilaya ama County Council. National park ibadilishwe na iitwe game reserve na chini ya wananchi kupitia kwa trustee wao County Council. Mawaziri wateuliwe kutokana na wataalamu na wabunge wabakie na kazi ya kuakilisha wananchi peke yake.

Rais asiwe mbunge awe ni mkuu wa dola na kuwe na Waziri Mkuu ambaye ataunda Serikali. Iwapo mtu atasimama Urais, basi tena akishindwa abakie tu mwananchi wa kawaida ama kiongozi wa chama chochote kile. Na kuhusu uchaguzi, ni wenyeji tu - wale tunaita indigenous people ndio wachaguliwe kisiasa kuwakilisha wananchi. Nasema hivi: Sio mtu atoke Western Kenya aje kupigania uchaguzi hapa Mwatate ama kwingineko. Wabunge na madiwani maalum wateuliwe kuakilisha masilahi maalum.

Elimu iwe bure na ya lazima kwanzia nursery mpaka University. Huduma ya kiafya iwe bure na pia ya lazima maanake kuna madhehebu mengine yanasema mtu asiende hospitali. Kwa hivyo iwe ni lazima, tena ni ya bure. Kila mkoa uwe na Chuo kikuu. Rasilimali zisimamiwe na mabaraza ya wilaya. Mabaraza ya wilaya yawe huru kujisimamia bila kusimamiwa na waziri wa mamlaka ya wilaya. Mamlaka ya kupambana na ufisadi iwepo na kutambulia kwa Katiba ya sasa.

Wahudumu wa afya wasiwe na biashara inayohusu taaluma yao. Yaani kama wewe ni daktari, usiwe tena una clinic pale ama chemist. Maanake tunaona ndio wanaibia Serikali kupitia hivyo. Mipaka ya mikoa iliyokuweko mwaka wa 1963 ihifadhiwe ili kuweka usalama. Nasema hivyo kwa sababu kuna mikoa ambayo inazozana, inasukuma mipaka ya mikoa ingine na pia wilaya zingine zinasukuma mipaka ya wilaya zingine. Nasema hivyo nikitaja sana Taita, imesukumwa sana upande wa Mtito Andei na

pia imesukumwa sana upande wa Mcnan Road. Mipaka ile ya zamani irudiwe.

Kamati za maendeleo wilayani zisimamiwe na wenyeji. Nasema hizi DDC kama zitaendelea kuwepo, basi zisimamiwe na wenyeji hata kama ni mwenyekiti wa baraza la wilaya asimamie kamati hizo maanake kwa sasa zinasimamiwa na wageni na masilahi ya wananchi hayaangaliwi vyema. Haki za kuakilisha katika mahakama ziweko….

**Com. Keriako Tobiko:** Ndugu yangu umalizie.

**Ephraim Mwang'ombe:** Asante. Haki za kuakilisha katika mahakama ziwepo kwa kesi za mashamba kwa mwananchi ambaye ni maskini. Maanake tunaona mwananchi anasukumwa na kesi ya mashamba na tajiri kwa sababu hana uwezo wa kupata utaalamu wa kisheria basi anashindwa. Hati za kusafiria zisiwe na vizuizi vyovyote. Mtu akitaka hati ya kusafiri apate. Bunge liwe na kuidhinisha uteuzi wa Mabalozi. Mawakili wanaoibia wateja waondolewe katika orodha ya mawakili. Makabila madogo yalindwe Kikatiba, tunaona makabila mengine madogo yananyanyaswa kama akina Ndorobo na wengineo na hata Wataita.

Waganga wa tiba ya kienyeji, watambuliwe kikatiba na wanapogundua tiba fulani basi watambulike na kupata haki miliki. Tunaona kwamba pengine wanagundua kitu na inafinywa na wale wengine. Na pia ikiwezekana waganga wa kienyeji hata wawe wakipewa honour degrees ama shahada za u-professor kama Prof. Wanjiku hapa. Asanteni kwa kunisikiza.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante. Jiandikishe pale mwenzangu. Jiandikishe. Mwabuduwa Mwakalo.

**Mwabuduwa Mwakalo:** Mimi ningetaka kusema mawili au moja. Iko kijana tuliuziana shamba. Tulipouziana shamba………

**Com. Keriako Tobiko:** Taja jina lako.

**Mwabuduwa Mwakalo:** Mwabuduwa. Ama wataka jina la baba? Sasa tulipouziana na huyo kijana hilo shamba, basi tukaendelea tukaendelea ……….

**Laughter from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Tafadhali tumsikize, tumsikize.

**Mwabuduwa Mwakalo:** Halafu tulipoendelea kama kiasi ya miaki miwili mitatu hivi, alipokuja kwa mastabadhi ya mashamba, akaona "basi nishapata bahati." Akaanza nini? - Kunitongoza sasa. Wasikia akaanza kunitongoza, akanisongezaaa. Nikamwambia, "sasa wewe mzee sasa mbona unafanya namna hii." 'Wewe tulia tu, we tulia tu'. "Nitulie kivipi na wewe

unakuja kunitafuta sasa?" Basi kwa hivi ndio nina bahati nikaona sasa mumefika nyinyi hapa, nijaribu kufika kwenu ili mjaribu kuniongoza. Mjaribu kuniongoza.

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa tunaweza kukusaidia namna gani?

**Mwabuduwa Mwakalo:** Kunisaidia kwa mafikira.

**Com. Keriako Tobiko:** Kwa mafikira?

**Mwabuduwa Mwakalo:** Yes.

**Com. Keriako Tobiko:** I see. Sawasawa. Tukimaliza hii, unione nje. Mimi ni wakili nitakwambia vile unaweza kufanya.

**Mwabuduwa Mwakalo:** Kweli. Sawa.

**Clapping from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Mukala Mwakalo. Mukala Mwakalo.

**Mukala Makalo:** Kwa majina mimi naitwa Mukala Mwakalo, na kitu kimenileta hapa ni kuhusu mashamba. Mashamba imelazwa, imepimwa vizuri lakini wakati wa kulazwa ililazwa, na ufisadi umekuja sasa. Tumeibiwa pesa na pesa zikaenda na mashamba yakauzwa. Kwa kuwa Katiba leo imesimama, imefika hapa tuna maoni yetu ya kusema Katiba itusaidie na Serikali. Itusaidie. Tumepata taabu na hizi vituko nje, tuna watoto lakini hatujui kama watajenga wapi. Na hii yote imeletwa na watu wa mashamba-ni wafisadi hawa wametuletea taabu kweli. Na watoto hapa Kitivo hawana mahali pa kukaa. Na ni sababu ya watu wa kulaza mashamba hawa, wanaiba. Basi kwa hivyo tunaomba Serikali itusaidie tuna taabu, Katiba hiyo itusaidie irekebishe maneno yote na kutakuwa usalama. Maanake sisi wenyeji tuko hapa na tumezaliwa hapa na mababa zetu wamezaliwa hapa hapa, hatuna mahali pa kukaa. Watoto wetu watajenga wapi? Kwa hivyo tunaomba Katiba imekuja hapa itusaidie kwa njia hiyo. Na wanyama hao wanyama, hatujaona wanyama wakichanganyikana na watu pamoja. Lakini leo tunalazimishwa tuwe na wanyama karibu na wanyama. Wanyama wanakuja wanakula vyakula vyetu. Tuna faida gani sisi watu wa Pwani ndani ya Kenya hii? Basi kwa hivyo tunaomba Katiba itusaidie. Sina mengi yangu ni mawili tu.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mzee wangu. Jiandikishe hapo kwa register. Jiandikishe. Paul Oringa.

**Paul Oringa:** Kwa waliofika hapa, mimi nina machache tu. Katika Katiba mpya ambayo tunatarajia kuwa nayo labda mwakani ama mwanzo wa mwaka ujao, nina maoni machache. Ya kwanza ni kuhusu vijana na wanawake. Inasemekana kwamba vijana

ndio zaidi ya asilimia sitini ya watu wote nchini Kenya. Lakini kama kuna tabaka la watu ambalo limedharauliwa na kufinyiliwa kabisa basi ni vijana. Nitazungumza kama kijana na ni kwamba, kwanza tunataka kutambuliwa katika hali yetu ya uongozi. Sisi vijana si wajinga na tunaweza kushika nafasi ya uongozi.

Na pili ni kwamba hatuwezi kushindana na wale wazee ambao walioko sasa kwa hivyo tunataka Katiba ambayo itatenga viti ambavyo vitashikwa na vijana katika Bunge letu, na pia katika mabaraza yetu ambayo tunataka kuyaongezea nguvu kwa hivi sasa kwa Katiba mpya ambayo tunaitaka.

Na la muhimu pia ni kwamba katika hali hii ya kutenga viti maalum kwa vijana, pia Katiba ihakikishe kuwa viti maalum pia vimetengwa kwa akina mama na pia walemavu vile baadhi yao walivyosema hapa. Na ili iwe katika Bunge letu, asilimia ya viti vilivyotengwa kwa vijana, akina mama na walemavu ichukue zaidi ya asilimia hamsini na tano. Kwa sababu akina mama ni wengi, vijana ni wengi basi tukijumuisha na ndugu zetu wengine walemavu basi wachukue zaidi ya viti asilimia hamsini na tano katika Bunge lote. Yangu ni hayo tu. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe. Eliud Muchalo.

**Eliud Muchalo:** Asante sana. Kwanza nitaanza kwa kusema kwamba Katiba yetu mpya iweze ku-define sawasawa mipaka ya Kenya na kila wilaya mipaka yao iwe defined - Itambulike kamili kwa sababu Katiba ya sasa haitambui mipaka. Na hii ndiyo sababu wengine wetu wameeleza kwamba mipaka ya Taita huko upande wa Mcnan Road upande wa Mtito Andei imevurugwa vurugwa sana. Kwa hivyo Katiba kila wilaya ieleze mipaka yake.

Pili Katiba ieleze kwamba Kenya ina kabila hili, na hili katika appendix yake - Kama vile Katiba zingine yalivyo. Katiba yetu haielezi namna hiyo. Na hii nchi ni nchi ambayo ina makabila. Yalikuwa forty two lakini yako mengine yanazuka sana. Na kila kabila lazima litambulike katika Katiba. Na mimi nataka kusema hivi katika utawala ama katika muundo wa utawala - structure of Government, District - ambayo ni wilaya ni lazima ipewe nafasi kubwa sana. Na kama inapewa nafasi kubwa sana, hii ni kusema uwezo mkubwa kutoka Central Government uwe devolved kwa district. Na mapendekezo yangu ni kwamba district iwe a “jimbo.” Taita tunataka jimbo la Taita ambalo …

**Clapping from the audience.**

Linaongozwa na Governor ambaye amechaguliwa na watu pamoja na Deputy Governor wake wachaguliwe na tikiti kimoja. Na huyo Governor aunde Serikali yake ambayo inasimamia mambo kadha wa kadha. Na Heads of department vile vile wawe ni watu ambao wana uwezo, tuwe kama ni…..kuna jambo hapa ambalo linakera sana Wataita, - ni jambo la ardhi. Kama tuna Secretary for land, tuwe na District Commissioner of land hapa Taita Taveta.

Yule mtu wa Nairobi ambaye anaitwa Land Commissioner, uwezo wake umalizike. Kazi iwe inafanywa hapa. Na huyu Land Commissioner atafanya kazi kupitia kwa District Land Control Board ambayo inasimamiwa na Serikali ya Governor. Vile vile tutakuwa na District Legislative Council, - Bunge la District ambalo linachaguliwa sawasawa. Na hii maneno ya Local Government, kama vile tulivyo na Taveta Town Council ambayo inasimamia division yote. Division ya Mwatate iwe na Divisional Council, ya Voi vile vile na Wundanyi vile vile. Yaani division isiwe division tu lakini iwe na uwezo wa kuangalia mambo ya utawala, mambo ya ardhi, mambo ya security.

**Clapping from the audience.**

Mambo ya ardhi nikiingia zaidi Bwana Chairman ama Madam Chairlady ni kwamba, vile tulivyosema District Commissioner of land aangalie hayo maneno na District Land Board. Hii ni kuonyesha kwamba hakuna mtu Nairobi anaweza kuingilia mambo ya ardhi ya wilaya kabla ya Serikali ya wilaya kusema "ndiyo."

**Clapping from the audience.**

Mtu, - Mtaita au mwingine yeyote kutoka wilaya ingine akipewa ardhi,- Mwananchi - citizen apewe freehold. Hapana ile lease ya miaka tisaini na tisa. Ni freehold - ni land yake. Lakini mzungu, - investor ambaye ametoka huko mbali, awe na leasehold ya kama two generations -fifty years hiyo inatosha, hapana miaka tisaini na tisa ama mia tisa tisaini na tisa. Hiyo ni maneno ya kikoloni.

**Clapping from the audience.**

Hiyo two generations miaka hamsini kama amei-develop vizuri na wenyeji hawana haja na ile ardhi wakati lease imemalizika, anaweza ku-apply kwa District. Na mambo mengine nataka kusema ni haya: Wakati tunakuwa na jimbo la Taita na jimbo la wilaya ingine, tuwe na Katiba yetu ya District ambayo inaidhinishwa na Parliament huko Nairobi. Kwa hivyo tutakuwa na sheria hapa ambazo zinatawala ardhi. Bwana Chairman, Madam Chairlady, jambo moja ambalo limeharibu, limeleta taabu katika Kenya hata ethnic clashes, limeondoa amani katika Kenya ni kule kutojali masilahi ya wenyeji.

Ile sheria katika Katiba ya sasa ambayo imetajwa tajwa sana kwamba Mkenya yeyote yuko uhuru kuishi mahali popote Kenya, na yuko huru kuwa na property (mali) katika mahali popote Kenya (ndio), - lakini with a question mark with a "provider" - Provided local authority ya sehemu ile imezungumza jambo hilo wakakubali. Maanake Commissioner of Land Nairobi, ana tabia mbaya sana ya kutuma mtu sijui kutoka wapi-----

**Clapping from the audience.**

Anampa letter of allotment ya one hundred acres katika Mwatate area. Letter of allotment ya quarter of an acre. Watu ambao hawajulikani kabisa huko Voi wanapata ardhi, wanamiliki ardhi. Madaraka ya huyo mzee huko Nairobi ondoa tafadhali.

**Clapping from the audience.**

Kwa hivyo muundo wa kisiasa ama wa utawala wa ki-district, na nina emphasize district, - hapana Mkoa. Kwa sababu kabla hata mkoloni hajaja, na wakati mkoloni amekuja, district ilikuwa ndio "unit of development." Na Katiba ya sasa tunataka i-speed up, i-accelerate development. Kwa hivyo uwezo wa kisiasa na uwezo wa kiuchumi katika Kenya uletwe katika wilaya.

**Clapping from the audience.**

Hapo utaona sasa vijana watakuwa busy maanake sasa mapato kutoka kwa rasilimali ya Taita. Na nikisema rasilimali ya Taita hata ile 62 % ya national park ya Tsavo ambayo iko katika wilaya ya Taita Taveta, itakuwa ni mali ya District ya Taita. Hapana National park ya Nairobi, - - in this district.

**Clapping from the audience.**

Mapato yote yatakuwa hapa, Kenya Wildlife Services watakuwa wanaendesha na ku-manage hii park na wale waliosema isiitwe National park iitwe Taita game reserve are right. Wawe na game reserve yao.

**Clapping from the audience.**

Maanake kila game reserve kama vile Narok, huko tuna Mara, Transmara or something game reserve. Wanapata mali na kama ile pesa inatumiwa vizuri na Narok County Council, - na nafikiri inatumiwa vizuri, hii yetu tukiitumia vizuri hata Chairman wa County Council hapa, ataunga mkono aseme 'Yes Sir, hii ni sawasawa'. Kwa hivyo tunataka hii inakuwa Taita taveta game reserve.

**Clapping from the audience.**

Halafu kodi zote zile za kutoka land, agricultural establishment, industrial estates zilizoko katika hasa wilaya hii, zote zinaingia katika mfuko wa District Government ya Taita Taveta.

Tukiwa na bunge hapa na Serikali ya wilaya, huko katika Nairobi tutakuwa na Federal Government bwana Chairman. Na Federal Government hiyo itaendeshwa na Rais na Makamu wake ambao wamechaguliwa na tikiti moja (running mate) na huyo President ambaye ni mkuu wa nchi atateua kutoka kwa zile Parliamentary parties. Prime Minister ambaye ataunda na kuendesha Serikali ya jamhuri ya Kenya na wao watakuwa responsible kwa yale mambo ya muhimu ambayo ni ya National

defence na mambo ya Internal, External Affairs na External Relations, mambo ya Immigration na mambo ya National Transport and Communication - hayo ndiyo mambo ya kupelekwa huko Nairobi. Lakini hapa Education hapa hapa, Land hapa hapa, Health hapa hapa, agriculture, Livestock Development hapa hapa. Mambo ya Madini yote hapa hapa. By the District Governer.

**Clapping from the audience.**

Ikifanywa namna hiyo hata bwana Chairman, wale ambao wanazoza wenzao kutoka nje na kupigana kupigana, itakuwa hakuna mambo ya namna hiyo. Tutakaribishana tu-maanake shida moja ya Kenya ni kwamba wananchi kutoka mahali kwingine wanakuja hapa wanasema 'This is Kenya'. Na wamesema "Taita ni milimani huko juu." So, unajua nyanda za chini ambazo ndizo mingi zinaitwa si za Wataita ni za Kenya. Sasa hii is a Constitutional matter, - Irekebishwe wakitoka huku tuseme Central, ama Rift Valley ama popote watambue haki za Wataita hapa. Na lile jimbo nasema ni umbrella, ni mwavuli wa kufunika haki za Wataita, mtu yeyote atakayekuja hapa tuseme 'wewe ni jirani yetu, wewe ni Mkenya tuzungumze.' Haya ndiyo ambayo ninasema.

Halafu wakati wa kuimarisha hayo maneno, Legislature kuwe na Bunge - House of Representative na vile vile tusisahau ile iyokuwako wakati wa independent Constitution bicameralism the Senate. Introduce Senate maanake Senators ni wale wazee ambao wanasaidiana na House of Representative kuangalia kwamba haki za kila wilaya, kila jimbo, haki za walioko na zitengenezwe sawasawa.

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa ndugu yangu, malizia sasa. Just wind up.

**Eliud Muchalo:** Kwa hivyo hayo ndiyo yangu bwana Chairman, nina mengi sana ya kusema lakini nafikiri kwa sababu umeniambia nimalizie, nitaachia hapo.

**Com. Keriako Tobiko:** Your ideas are very creative and innovative, uko na memorandum?

**Eliud Muchalo:** Yes. Iko hapa.

**Com. Keriako Tobiko:** Tafadhali tupatie.

**Eliud Muchalo:** Asante sana.

**Clapping from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Jeremiah Chelezuga.

**Jeremiah Chelezuga:** Basi mimi niko na memorandum hapa. Kwa majina yangu Jeremiah Chelezuga. Niko na memorandum hapa ya watu wa Kitivo lakini nimedokoa dokoa zile main points. Kwa hivyo nitachukua kama dakika tatu kwa haraka. Tunaanza hivi: Katika Katiba ijayo tunataka kila tasishi ya utawala iwe huru. Serikali kuu isiingilie Bunge, Bunge isiingilie Serikali kuu. Zote ziwe independent.

Kitu cha pili kila wilaya iwe na uwezo wa kutumia na kumiliki rasilimali zote zilizoko mahali hapo. Maji, Madini, Ardhi, Wanyama pori, Misitu na kadhalika. Kufafanua ni kwamba kodi yote inayotozwa maji ilipiwe katika baraza la wilaya ya Taita Taveta. Vibali, kodi ya madini, baraza ya wilaya ihusike sio Serikali kuu. Kodi zote zinazokusanywa katika mbuga za wanyama, ilipiwe katika baraza ya wilaya ya Taita Taveta. Ardhi yote iliyopeanwa katika enzi ya ukoloni na baada ya uhuru irudishwe kwa wenyeji wa mahali hapo. La sivyo, County Council iwe automatic shareholders wa mashamba hayo makubwa makubwa.

Nikimaliza hapo kuna kipengele kingine hapa. “Kusiwe na mapinduzi yeyote ya kijeshi katika nchi”.

Ngazi za utawala: Tumependekeza ya kwamba tuwe na ngazi tatu za utawala katika kila wilaya. Ngazi ya kwanza, tuwe na mzee wa kijiji. Ngazi ya pili, Chifu. Ngazi ya tatu, District Commissioner ambaye ni mwenyeji wa mahali hapo na wote hawa watachaguliwa na wananchi moja kwa moja.

Watumishi wa umma: Watumishi wote wa umma wasifungamane na siasa za upande wowote na wasifungamane na siasa za chama chochote cha kisiasa. Watumishi wote wa umma walipwe vizuri na wasihusike na kazi yeyote ya kando. Kwa mfano vile tumesikia private clinics ama kazi za binafsi. Kama unataka ufanye kazi ya kibinafsi, basi uache hii ya Serikali. Watumishi wote wa umma waajiliwe na kufutwa katika ngazi ya wilaya. Rais asiwe Mbunge, Waziri asiwe Mbunge.

Uchaguzi: Mgombea viti wa Ubunge na Udiwani wawe wenyeji wa mahali hapo. Kura zihesabiwe katika kituo cha upigaji kura. Masanduku ya kura yawe transparent - yawe yaani tunaona vile kura inavyoshuka.

Usawa wa jinsia: Katiba ihakikishe usawa wa jinsia. Mwanaume yeyote atakaye mpachika msichana mimba alazimishwe na Katiba kumlea mtoto huyo hadi umri wa miaka kumi na minane.

**Clapping from the audience.**

Kulingana na pendekezo ya watu wa Kitivo wakasema hivi; Pombe ya kienyeji ihalalishwe na County Council ya mahali hapo isimamie unywaji huo vilivyo. Afisi ya mkuu wa sheria na ile ya Mwendesha mashtaka zitenganishwe na kila moja iwe huru.

Mkuu wa sheria asitatize mashtaka yanayoendeshwa na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali kwa kutumia neno sijui la ki-latin linaitwa "nolle prosequi"

Ufisadi: Wafisadi wote watambuliwe tangu wakati wa uhuru na washitakiwe katika mahakama. Kuwe na uhuru wa kuabudu Mungu peke yake. Kuwe na vyuo vikuu katika kila mkoa. Kuna mengine hapa lakini sasa kwa sababu tuko na memorandum, tunakomboa wakati nasema asante.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Walter Madedu.

**Walter Madedu:** Kwa Commissioners na watu wa Mwatate, kwa majina naitwa Walter Madedu. Mimi niko na points chache ambazo nitazisema in summary form. Naunga mkono yule Chairman alikuja hapa wa Chavia Mwachavu kwa upande wa mashamba kwa sababu mimi ni mmoja wa hapo hapo. Lakini nilikuwa na point ambayo nataka kuikaza. Pointi ya kwanza ni kwamba tuwe na mfumo wa majimbo. Machifu kutoka Assistant Chiefs, Chiefs hata DO wachaguliwe na wananchi. Wachaguliwe na wananchi na tena wawe wananchi wa hapa. Kwa mfano kama ni DO lazima awe DO wa hapa wilaya hii - Mwananchi wa wilaya hii.

**Clapping from the audience.**

Na wilaya zozote pale wafanye hivyo. Na watakuwa na uwezo wa kuchaguliwa tena baada ya miaka mitano. Lakini akishindwa baada ya miaka mitano kama hatachaguliwa, basi apatiwe marupurupu. Chairman wa County Council achaguliwe moja kwa moja na wananchi na asiwe na kiti, awe Executive chairman. Ma-councillors wake watoke katika kila location na tuwe na locational council, - hata zamani zilikuweko lakini tunataka zirudishwe. Ili katika kila location wawe na committee. Councillor na kikundi chake, iwe itamiliki utawala wa location. Mgeni yeyote ambaye atakuja lazima apitie kwa hiyo committee na ajulikane madhumuni yake ni nini. Kama ni watu wa kuchimba madini, lazima wapitie kwa hiyo committee na lazima waungane na wananchi wa pale ili rasilimali ya pale wananchi wafaidi nayo.

Kwa upande wa elimu, natilia mkazo kwamba elimu iwe ya bure. Kutoka elimu ya vidudu yaani nursery mpaka elimu ya University. Kwa sababu utakuta watoto wengine wako very bright lakini anashindwa kulipa karo ya University - National Universities. Zile ambazo ni private watajihudumia wenyewe. Na hii karo ya shule itapatikana namna hii. Ile rasilimali yote ambayo itaingia kwa County council ambayo itamilikiwa na hiloo baraza la county council italeta pesa za kutosha kwa elimu ya hawa watoto. Ile kidogo inayobaki kutoka kwa hiyo budget itapelekwa kwa katika Central Government. Lakini lazima wafanye budget yao, wa-include education, wa-include health, na mambo mengine.

Kwa upande wa wabunge, mimi naonelea kwamba wabunge wawe ni watu ambao wamefika University, tusipate tu wabunge ambao tu ni watu wa hivi hivi. Watu wawe wamefika University na….. haya ni maoni yangu wananchi. Sio yenu.

**Com. Keriako Tobiko:** Tafadhali tafadhali. Hayo ni maoni yake. Wewe unaweza kuwa na zako tofauti na unangojea mpaka upate nafasi.

**Walter Madedu:** Ma-Councillors pia wawe ni watu ambao wamefika form four. Lakini wale ambao wanakaa sasa - sitting Councillors wawe wamefika at least class eight kama wanataka ku-contest. Rais awe anachaguliwa na wananchi wote kwa ujumla awe ni Executive President, na yeye awe ana-consult wabunge ambao wamechaguliwa na wananchi, awe na haki ya kuchagua Ministers ambao hawa pia ata-consult wabunge – sio kuwachagua hivi hivi. Mawaziri wawe ni watu ambao wako na sifa fulani katika kila wizara. Kwa mfano kama ni Waziri wa elimu, lazima ajulikane kwamba yuko educated.

**Com. Keriako Tobiko:** Tunaelewa hiyo. Kwenda kwa pointi ingine sasa. Go to the next point. We understand that.

**Walter Madedu:** The next point. Nafikiri hata hivyo naendelea kumaliza na nilikuwa nasema kama ni mawaziri wasiwe wengi, - wawe between fifteen and twenty. Nafikiri namalizia hapo. Asanteni sana kwa kunisikiza.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante. Jiandikishe hapo. Michael Mwangemi

**Michael Mwangemi:** Mimi natoka Kishamba na sina mengi yangu ni kama kutilia mkazo yale yamesemwa. Nitaanzia na haya mambo ya kushikwa. In case umefanya kosa hatua ichukuliwe haraka. Mshitaki achukue hatua haraka kwa yule mtu ambaye amemshitaki, asizidi kukaa pale ndani. Na kama atakaa pale ndani, yule aliyeshtaki achukuliwe hatua kama amefariki yule mtu kwa sababu yeye ni binadamu. Halafu kwa upande wa mtu akifariki kule ndani, iwe ni hatua ya kuchukuliwa kwa yule mshtaki au kwa Serikali kwa sababu tunapoteza watu wengi, tunasikia mtu amekufa na hakuhukumiwa; - Amekufa tu hapo ndani.

Pili ni mambo ya mashamba - hii madini. Unaweza kuwa unachimba madini, lakini ile pesa hufaidiki nayo, - sisi Wataita hapa hatufaidi kwa hiyo pesa. Tunaumia bure na ukiangalia ni kabila tofauti za kutoka nje ndio zinashughulikia hayo mambo. Kwa hivyo tunaomba sana hayo mambo yarejeshewe raia wa hapa hapa. Nafikiri kwa hayo mimi sina mengi nikiongezea hapo hapo ndani, Wizara ya Afya "inasleki" sana, imerudi nyuma. Kwa sababu unaona ni mtu ndio, ukitembea waweza enda kuangalia mtu wako mahali fulani kama ameshtakiwa nini lakini mahali anakaa hachukuliwi kama binadamu-------

**Com. Keriako Tobiko:** Kwa hivyo pendekezo lako ni gani kwa hili?

Pendekezo ni kwamba, Wizara ya Afya iangalie kuwa yule mtu mahali anapoishi, pale amepelekwa amehukumiwa anakaa, - huwezi kukaa unakula hapo na choo iko hapo hapo. Wizara ya Afya iangalie haya maneno. Binadamu hawezi kukaa na choo ndani ya nyumba. Kwa hayo mimi sina mengi nasaidia mkazo hapo.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo. Boniface Mwang'ombe.

**Boniface Mwang'ombe:** Mimi ni Boniface Mwang'ombe kwa majina na ninashirikisha kikundi cha Ilole sub-location na kwa maoni yangu kwa sababu nimeona vipengele kadha wa kadha vimechangiwa, nitafupisha. Katika kipengele cha ukatibu mkuu kuna hii wanasema kwamba asilimia sitini na tano ya kura zote za wabunge inaweza ikapitishwa, ningeomba kama haitaathiri mwananchi wa kawaida, moja kwa moja inaweza kupitishwa. Halafu kuna hizi sehemu ambazo Bunge inaweza ikageuza. Kuna sehemu ambazo ziko tatu, kuna hii sehemu ya muundo na aina ya Serikali, Bunge isipewe hiyo mamlaka. Halafu kuna mamlaka ya nchi, pia hiyo sehemu iangaliwe Bunge isiwe na mamlaka. Kuna hii haki ya uraia, mtu yeyote ana haki ya kuwa raia ikiwa ni mzaliwa wa hapa ama mzazi wake mmoja ni raia wa Kenya.

Vyama vya kisiasa. Katika kikundi cha Ilole walipendekeza vyama vya kisiasa viwe vitatu na visiwe zaidi ya hiyo ili kuweka upinzani zaidi. Na wakati wanaposhughulika na mambo ya uchaguzi ama siasa, kila chama kijighalamie chenyewe na kisighalamiwe na Serikali. Pesa ya umma isitumike ovyo ovyo.

Serikali ya mitaa. Serikali ya mitaa iwe kama ndio mkaguzi ama msimamizi wa rasilimali zote za wilayani. Na katika Ma-mayors, wawe wakichaguliwa na wananchi na sio wakichaguana katika baraza. Na awe na kiwango cha elimu kufikia kidato cha nne na kuendelea. Na pia kusiwe na madiwani wateuzi.

Bunge: Bunge liwe likidumu kwa miongo miwili. Halafu nikifika katika kipengele cha rasilimali. Tukiangalia sana wilaya yetu ya Taita Taveta, asilimia sitini na mbili ni mbuga ya wanyama wa pori. Kwa hivyo wananchi waliomba hiyo asilimia sitini na mbili ipunguzwe hadi nusu ambako mwananchi wa kawaida anaweza kunufaika hapo. Pia kuna hizi rasilimali kama madini ama tusema huu utaratibu wa utalii. Wananchi wangeomba asilimia arobaini ibaki wilayani na sio ipelekwe katika Serikali kuu.

Pia kwa upande wa ufanyi kazi, kuna hizi kazi (unskilled jobs) na sio professionals, at least 65% ya wafanyi kazi wawe wametoka mahali hapo na sio kwingine. Kwa hayo asanteni ili tuokoe wakati.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo ndugu yangu. Lloyd Mwambela.

**Lloyd Mwambela:** Kwa majina ni Lloyd Mwambela Mwavasi na kulingana na mapendekezo yangu juu ya Katiba ni:

Katiba isibadirishwe na Bunge ama mtu yeyote bali wananchi kupitia kwa kura ya maoni. Tume iliyoko sasa ya Katiba iendelee ili kuhakikisha Katiba inafuatiliwa vilivyo na hakuna mtu anayeiharibu.

Kusimamia maswala ya kikatiba: Wabunge wawe na sheria ya kuwalinda nje na ndani ya Bunge. Wafanye kazi wakati wote sio kwa masaa. Washughulike kwa ajili ya umma sio Serikali - yaani they should be public centered and not leader centered.

Wananchi wawe na haki ya kuwarudisha nyumbani. Elimu ya wabunge iwe ya kidato cha nne na kuendelea. Ardhi itawaliwe na wenyeji wa mahali pale na sio mtu kutoka nje. Hakuna haki ya mtu kuishi mahali popote. Kila mwanakenya ana haki ya kuwa na ardhi isiyozidi acres hamsini na sio futi tatu kwa undani kama vile ilivyo Katiba ya sasa. Ni kuanzia juu na hata undani wake iwe inamilikiwa na mwenyeji wa mahali pale.

**Clapping from the audience.**

Rasilimali zote zimilikiwe na Local Authority ama Serikali za mitaa la eneo lile. Ugawaji wa mapato ni kwa mwenyeji, jamii ya mahali pale halafu ndio twende kwa Serikali kuu. Mkenya ni lazima apate haki ya kimsingi, afya, elimu, ardhi, maji, chakula, usalama na mengineyo ni lazima yapatikane kwa Mwanakenya. Vyombo vya habari, magazeti, redio, T.V. na kadhalika viwe na uwezo ama uhuru wa kutangaza na kutoa habari. Kusiwe na vizuizi vya aina yeyote vile. Mfanyikazi yeyote akihusika katika kashfa ya ufisadi afutwe kazi mara moja bila kujali yeye ni nani. Viongozi wa utawala wawe wakichaguliwa na wananchi. Mamlaka ya wilaya yawachiwe mabaraza na sio Ma-DC ama Ma-DO kwani wao ni watu wa kutoka nje.

Mayor na wenyeviti wa mabaraza wachaguliwe moja kwa moja. Kura zote ziwe za siri na zihesabiwe kwa kituo. Box liwe transparent. Asilimia sabini na tano ya nafasi za kazi zipewe wenyeji wa mahali pale. Sio watu wengine kutoka nje. 25% ipewe wataalamu - ama kazi zile zitahitaji utaalamu ziwe ni asilimia ishirini na tano. Kodi zote ziwe zikiingia katika hazina ya Local Authority.

Kuwe na tume ya huduma za umma za kusimamia majukumu na mahitaji yote ya wafanyikazi wa Serikali na wabunge. Hakuna ulinzi wa kutosha hivyo walinda usalama, wahudumie wananchi kikamilifu na pasipo mambo ya kitu kidogo. Tuwe na utawala wa majimbo ukigawanywa kimkoa na kiwilaya. Wapwani ni wanajamii waliobaguliwa na kuonewa na kudharauliwa - kwa ajili ya mila na desturi zao ni wakarimu, na wapenda amani na hivyo kuingiliwa na makabila mengine na mali yao kunyakuliwa. Hivyo Katiba ambayo tunayoitunga sasa ihakikishe ……….

**Com. Keriako Tobiko:** Ndugu yangu fanya namna hivi; just summarise maanake tutajisomea hiyo memorandum.

**Lloyd Mwambela:** Okay. Ihakikishe ulinzi wao. Elimu ya bure hadi kidato cha nne na mishahara ya walimu wa nursery isimamiwe na Local Authority. Nadhani kulingana na hali nitakomea hapo kwa sababu nina mengi. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana jiandikishe hapo. Vitalis Mungo. Obedi Omide.

**Obedi Omide:** Mimi kwa jina langu naitwa Obedi Omide na mimi ni mkaazi wa hapa Mwatate. Nimekulia hapa Mwatate. Naomba kwa marekebisho haya ambayo yatakayokuja, tunahitaji Serikali ambayo itahakikisha kila Mwanakenya ana sehemu ya ardhi ya kuishi. Tunaomba Serikali itakayokuja, ijali sana masilahi ya mwananchi ambaye aliyoko ngazi ya chini. Isiwe ni

Serikali ambayo inamlika wale ambao wana mapato makubwa na kunyanyasa wale ambao hawana.

Pili, tunaomba marekebisho yaweko kwa Serikali hiyo itakayokuja kuzuia ufisadi hasa kortini; Wakati umedhulumiwa, wanaweza kuwa na akili kwa upande mwingine ukasema wacha nitafute advocate ama wakili wa kuweza kunitetea. Wakili huyo akikuta wewe ni mnyonge unapata shida sana kwa sababu anakula pande zote mbili. Akishakutafuna na kujua kwamba ashakumaliza, basi anakupa ghalama yake anaachana na wewe.

Kwa hivyo tunaomba Serikali itakayokuja iwe ni Serikali ya kuheshimiwa na iwe ni Serikali ambayo inaweza kuogopewa. Utakuta mwananchi wa kawaida ananyanyaswa bila sababu. Nikisema hivyo sisemi kwamba nikwa kutukana ama nini, la. Kwa mfano Serikali imezuilia hizi pombe za kienyeji na Serikali ilipozuilia ndio hatutakai, wengine wanaibia Serikali. Wakati mwingine unakuta raia wa kawaida hana hatia------

**Com. Keriako Tobiko:** Kwa hivyo pombe ya kienyeji unataka ifanywe namna gani?

**Obedi Omide:** Tunaomba Serikali ikiwezekana iangalie masilahi kwa sababu hawa wananchi ambao wamezuiliwa pombe za kienyeji, tupewe klabu.Ihalalishwe. Tupewe klabu.

**Jeering/shouts from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Sawasawa endelea.

**Obedi Omide:** Halafu hawa watu wanaitwa wafisadi walionyakua pesa kwa Serikali wamesababisha mwananchi wa kawaida wa Kenya kubaki maskini. Wapigwe darubini na Serikali ijayo ikiwezekana hiyo mali irudi kwa mikono ya Serikali. Mwisho Mwanakenya yeyote awe na uhuru kuishi pahali popote nchini Kenya.

**Jeering from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Maoni yake hayo. Heshimu maoni yake.

**Obedi Omide:Maoni yangu.** Mimi nikisema hivyo nasema nikimaanisha sasa wakenya wanaoana, si tunaoana? Wakati tunapo oana, huenda baba mkwe wangu mimi, baba mkwe ameridhika na mimi kumchukua yule binti, na amenipa shamba amenioza. Pasiwe na mwenyeji wa kutaka kujua kwamba mimi, baba mkwe yule wa kwangu amenipaje lile shamba. Niwe na mimi pia nina haki na Mkenya yeyote aruhusiwe anaweza kununua ka-plot pahali popote anapoishi. Yangu ni hayo. Asante.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante. Jiandikishe pale. Violet Nyambu.

**Violet Nyambu: Haya maoni juu ya m**arekebisho ya Katiba yameletwa na viongozi wa kata ya mwanabogo wakiwa ni wananchi arobaini ambao walikadiria matarajio hayo. Jambo la kwanza, Katiba ambayo iliyoko sasa haikuandikwa Kiswahili, iliandikwa Kizungu. Kwa hivyo tunataka Katiba ya lugha ambayo inaeleweka - iandikwe Kiswahili. Serikali iliyoko sasa si nzuri juu ilikalia wananchi sana tunataka Serikali ambayo ni ya *majimbo* - ya kiuchumi ya wilayani.

National parks: National parks isiitwe "National park" igeuzwe "Game reserve", ili wananchi walioko hapo waliotoa mashamba yao yakawa yatumiwa na game reserve wafaidike.

Ardhi: Ardhi iliyoko hapa Taita Taveta itumiwe na Wataita wenyewe na wapatiwe madaraka wilayani kwa kujigawanyia wananchi wenyewe. Hapa hii shamba ya mikonge, sehemu kubwa na ambayo ni nzuri imechukuliwa na mikonge. Hiyo lease yake iondolewe, wananchi wapewe sehemu ingine na waitawale. Shamba ya mkonge imekuwa inapatianwa kwa lease kinyume cha Wataita. Kwa hivyo lease tumeomba iondolewe.

Ranches: Kusiwe na makabila mengine kama Wasomali - tumeona wameingia hapo na watu wengine ambao wanachunga hapo katika ranches za Wataita. Ranches za Wataita wazitawale na waweke ng'ombe zao wao wenyewe.

Maji ya 'mzima springs': Maji ya mzima springs, sehemu ingine igawanywe iingie Taita Taveta hasa Mwatate. Tutumie kwa irrigation.

Nguvu za Rais: Nguvu za Rais zipunguzwe na awe ni mtawala wa kawaida na awekewe Waziri Mkuu ambaye ndiye ataangalia Serikali. Utawala wa mikoa uondolewe tuwe na utawala wa wilaya. Machifu na maofisa wao na akina "*mwalugongo*" wachaguliwe na wakishachaguliwa wapewe two terms - mihula miwili. Si kwamba ati akichaguliwa anakuwa permanent. Wapewe mihula miwili ili wawapishe wenzao nao wafanye kazi. Hiyo mihula miwili iwe ni jumla ya miaka kumi.

Kuridhi ardhi ama mali yeyote: Wakati mtu anapewa kuridhi mali, mtu wake amemuondokea, ni mama ameondoka, bwana anataka kuridhi, mtoto anataka kuridhi, ama ni bwana ameondoka, mama anataka kuridhi, mtoto anataka kuridhi, kusiwe na malipo yeyote ofisini. Mtu aende ahudumiwe bila kulipa na aridhishwe hicho kitu. Na watu wa mtaa ule wapewe uwezo kuangalia vile atakavyoridhi. Kusiwe na vikwazo vikwazo ndani ya Serikali na kudodoa dodoa yule mtu anataka haki yake.

Mahakama na Ma-judges: Mahakama na ma-judge, wasiteuliwe na Rais. Waajiriwe kazi kulingana na elimu yao na wawe wakiamua wasiwe wakiingiliwa ingiliwa, wawe wakiamua kesi kulingana na uwezo wao waliofundishwa. Katiba hii ambayo tunaendelea kutengeneza sasa isiwe ni Katiba ya kumaliza pesa na kumaliza wakati na wananchi kuhudhuria na kuleta mapendekezo yao yasitekelezwe. Tunaomba hii Katiba inayotengenezwa sasa itekelezwe na iwe ni jambo la kweli linafanyika, na iwe na malengo ya mbeleni - Iendelee kurekebisha tu, ipatiwe uwezo iendelee kurekebisha.

Kuwe na kifungu cha kumuondoa Mbunge, ama Rais ama Diwani akikosea Katiba kabla ya miaka mitano. Kabla ya muhula wa kwanza kuisha. Ikiwa Rais amekosea wananchi, ama Mbunge ama Diwani kuwe na kifungu cha kuweza kumuondoa kabla hajamaliza hiyo miaka mitano.

Afya: Matibabu yawe ya bure - irudi ya bure. Wakati tulipata uhru ilikuwa ni kuondoa ujinga, umaskini na kupatiana elimu. Lakini sasa imekuwa elimu haipatikani. Imekuwa ni nguvu. Kwa hivyo afya ikae ya bure na madawa ipatikane mahospitalini.

Kuondoa umaskini: Tumeomba viwanda vifunguliwe kila wilaya na hasa kiwanda chetu cha Ramisi kilichokufa ikiwezekana hicho kiwanda kifunguliwe. Co-operatives zianzwe na ile kodi ya County Council tafadhali hii iingie kwa Katiba, kuwa kodi inayotuzwa mtu anayeleta vitu vidogo vidogo isiwe sawa na ya yule anayeleta nguo ama magunia ya mahindi. Hili jambo limeleta umaskini sana. Pale kurekebishwe kuwekwe kiwango. Kama watu wa mashambani watalipa kodi namna gani? Sio kama watu wa town. Watu wa sokoni walipishwe kulingana na zile vitu wameleta. Mtu wa nguo asifanane na yule ameleta mnavu.

Uchaguzi: Kuwe na kiwango cha kura ambacho kiongozi atahitajika kuwa nacho ndio awe mshindi.

Maana watu wanaweza kupata mwingine 50, mwingine 65, mwingine 68, mwingine 70, lakini yule amepata 70 na mwenzake amemshinda na mbili tu, inakuwa yeye ni mshindi. Ikiwa wale wamefuatana fuatana, kuangaliwe ile percentage, wawili warudishwe na wapiganie ili kuonekane mshindi. Kura za mlolongo ziondolewe na kuwe na kura za siri na masanduku yawe transparent. - yawe yanaonyesha karatasi imeingia namna gani. Sio sanduku tupu inaletwa na hakuna makaratasi.

Rais: Rais asichaguliwe pamoja na wabunge wala madiwani. Rais akae na siku yake maalum ya kuchaguliwa. Baada ya kuchagua wabunge na madiwani kuwe na siku ya Rais peke yake ambayo anapigiwa kura. Maana kunaingia udanganyifu mwingine, wabunge wengine wanatumia ile sifa ya Rais na wanapita kwa sababu ya sifa ya Rais na alama kwa sababu zimefanana. Na pia Rais asiwe chini ya miaka arobaini na tano na asitawale kama ni zaidi ya miaka sitini. Hii ni kwa sababu akifika miaka sitini, ameanza kupungua akili kwa hivyo hataki watu ambao wameanza kuumba akili.

Wabunge wakichaguliwa, wamechaguliwa na wananchi wametumwa wawe wajumbe. Wafanyie wananchi kazi sio waende wawe Mawaziri. Wakiwa Mawaziri wanafanyia Rais kazi basi mwananchi hatamwona hata hatamfaidi.

**Com.Keriako Tobiko:** Hiyo pointi tumeelewa mama, sasa next na ujaribu kumalizia sasa.

**Violet Nyambu:** Sawa. Kura zikipigwa zihesabiwe pale pale kwa polling station. Zizibebwe ziende kuhesabiwa mahali. Zihesabiwe pale pale zionekane kweli yule mtu alishindwa pale ama hakushindwa. Elimu: Elimu tokea nursery mpaka na kuendelea ikae ya bure mpaka eight. Mipaka (boundary) Mtito-andei, Taru, irekebishwe mpaka irudi kama zamani.

Haki za watoto na walemavu. Walemavu wapelekwe shule, watoto wapelekwe shule, kuwekwe kifungu ikiwa mtu ana mlemavu wake halafu anamficha ama ana mtoto wake anaranda randa haendi shule, huyo mzazi achukuliwe hatua. Kuwe kifungu cha kuangalia hayo mambo. Maana kuna walemavu wengi, watu wanaficha watoto wao.

Haki za wanawake: Wanawake waandikwe kazi sawa na wanaume kulingana na kiwango kile wamefika. Sio mwanamke anapewa kazi ile rahisi rahisi kwa sababu ati yeye ni mwanamke. Pia wanawake…….

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa mama the last one. We will read your memorandum.

**Violet Nyambu:** Sasa wacha niseme moja tu.

**Com. Keriako Tobiko:** Sema moja halafu….

Pombe ya kienyeji: Pombe ya kienyeji tumeomba ihalalishwe na vilabu virudi kwa sababu watu wanaendelea kupatia Polisi na Machifu nguvu kupewa pewa hongo wakati ameshikwa na pombe vichakani. Kwa hivyo ikihalalishwa itakuwa wazi na hakuna mtu atashika mtu. Kwa hivyo wanaume wetu watakuwa wakinywa pombe zao hadharani - ama wale wanawake wanakunywa itakuwa imehalalishwa na anaenda kwa klabu bila kuogopa ogopa.

**Com.Keriako Tobiko:** Okay sawasawa mama.

**Violet Nyambu:** Wazee wa *mwalugongo* na wa vijiji, wawe wakipewa kitu wanafanya kazi kubwa sana vijijini. Ndio wanataarisha Serikali kabla haijafika kwa Chief ama kwa DO kwa hivyo ninaomba wapewe kitu chochote cha kuwasaidia.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mama. Jiandikishe hapo na upeane memorandum yako. Fredrick Mwachofi. No, sorry kabla yako? …. ushafika. Unaweza tafadhali kutupatia nafasi kuna walemavu kutoka Bura Rehabilitation tunaweza kuwapatia nafasi kidogo kabla ya………..Joseph Mwangeka Simusi.

**Joseph Mwangeka Simusi:** Kwa majina naitwa Joseph Mwangeka Simusi. Mapendekezo ya walemavu wa Bura Rehabilitation kwa kamati ya marekebisho ya Katiba ya Kenya. Wakenya wawe na kitambulisho kama ushahidi wa uraia na

walemavu wapewe kikao mbele kuepukana na kusimama katika milolongo mirefu ya kuomba vitambulisho. Vyama vya kisiasa nchini viwe vitatu vyenye nguvu. Kazi ya wabunge iwe ya kila siku kwanzia jumatatu hadi ijumaa masaa ya kawaida ya kazi. Kuwe na hatua maalum za kuongeza kushiriki kwa walemavu, wanaume na wanawake bungeni. Kama mbunge hatekelezi maendeleo katika eneo lake basi wananchi wamrejeshe nyumbani baada ya miaka miwili na uchaguzi ufanywe upya. Wananchi wawe wakiamua mishahara ya wabunge.

Wagombea viti vya ubunge wawe na miaka na ishirini na tano kwenda bungeni. Kuongezwe wakalimani wa sign language katika mahakama na runinga za kitaifa. Mayor na wenyeviti wa mabaraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Madiwani wawe na elimu ya kidato cha nne kwenda juu. Madiwani wateule wawe walemavu. Wakati wa uchaguzi, walemavu wapewe kikao mbele kutokana na hali yao ya ulemavu wa viungo. Elimu iwe ya bure kufikia kidato cha nne. Vituo vya elimu vya walemavu, visambazwe kote nchini.

Walemavu wasibaguliwe ki-elimu na elimu kwa walemavu iwe ya lazima. Huduma za afya hata kwa walemavu ziwe za bure. Maji masafi ya mifereji yasambazwe kote nchini. Walemavu wahusishwe katika vyama vya wafanyakazi. Katika vituo vya ki-elimu vya walemavu, walimu wote wawe walemavu na walipwe vizuri. Mahitaji mengine kwa walemavu ni kama ifuatavyo:

Simu za umma ziwekwe chini zaidi na pawekwe kiti cha kukalia. Mabasi yaweze kupandwa na walemavu bila matatizo. Nyumba za ghorofa ambazo hazina lifts ziwekwe njia za wheelchairs. National fund for the disabled itambaze huduma zake katika pembe zote na walemavu binafsi wapewe hiyo misaada. Walemavu wagawiwe mashamba sawasawa na wale wengine. Utaratibu wa kubadirisha umilikaji mashamba urahisishwe. Lugha za taifa ziwe mbili - Kiswahili na Kingereza.

Kuwe na tume ya kushughulikia masilahi ya walemavu. Walemavu waajiriwe katika Civil Service. Walemavu wahusishwe katika pande zote za uongozi. Vocational Rehabilitation division ambayo iko katika idara ya huduma za jamii ibadirishwe cheo na kuwa idara kamili. Huduma za afya ziwekwe mahali popote ambapo kuna kituo chochote cha walemavu." Kwa hayo asanteni na Tume iendelee na kazi yake hadi mwisho wenye mafanikio mema.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe pale na upatiane memorandum yako. Fredrick Mwachofi. Nafasi ni yako.

**Fredrick Mwachofi:** Kwa jina naitwa Fredrick Mwachofi na nimetoka Chaviateri kijiji cha Teri. Haya ni baadhi ya Wateri waliyoandika. "Katiba isiwe ikibadirishwa na asilimia yeyote ile. Iwe ikipatikana na makosa irudishwe kwa wananchi.

Muundo wa Serikali: Serikali tunataka muundo wa majimbo na majimbo yawe katika wilaya.
Elimu: Kwa upande wa elimu tunataka elimu ya bure kwanzia nursery hadi vyuo vikuu. Walimu wawe wakilipwa na Serikali kwanzia nursery na kuendelea. Na tunataka Katiba ieleze kwamba kila mkoa uwe na University yake moja.

Upande wa ajira: Ajira ya watoto wadogo ifutiliwe mbali kabisa. Atakaye andika mtoto afungwe miaka kumi bila fine. Katiba itambue chama cha wasio na kazi.
Mahakama: Mahakama kuamua haki kwa mujibu wa sheria za umma bila kupendelea tajiri ama maskini. Mahakama iwe na uwezo wa kupeleka Bunge ama Serikali mahakamani endapo zimeenda kinyume cha Katiba. Mahakama isiwe chini ya Serikali na ihakikishe kwamba umma unatawaliwa kulingana na sheria zilizoko na zingine kutoka vijijini. Mahakama iwe katika kila tarafa kupitia kwa mahakama kuu.

Serikali za mitaa: Mayor ama mwenyekiti wa baraza achaguliwe na wananchi na waajibike kutembelea kila mahali katika baraza lake. Diwani ama Councillor kama haajibiki, Katiba ieleze wazi wananchi wako na uhuru wa kupiga kura ya kutokuwa na imani na yeye. Serikali ya mitaa ikishirikiana na kamati za wananchi ndio itakuwa na njia nzuri ya kusimamia rasilimali za wananchi.

Serikali: Kutekeleza kauli za umma, Serikali isiwe na uadui na raia. Kwa mfano mtu ameumizwa akienda polisi anaulizwa atoe kitu kidogo. Kuhakikisha kwamba raia na mali zake ziko katika hali ya usalama. Machifu na manaibu wao wawe wakipigiwa kura. Kama Serikali inamhitaji kama mfanyikazi wao, awe akipigwa transfer huko na kwenda mahali pengine. Mbunge achaguliwe na wananchi lakini mawaziri wachaguliwe na tume.

**Com. Keriako Tobiko:** Mwachofi, hilo liwe la mwisho maanake tutajisomea hiyo karatasi.

**Fredrick Mwachofi:** Sawa. Kwa rasilimali: Rasilimali zote zitambuliwe na baraza la wilaya. Na kuna hili neno linatumiwa "lease," lifutiliwe mbali na Katiba hii kwanzia leo hadi kuendelea kwa sababu lease ya miaka zote hizo inatunyanyasa na inatuumiza. Na kwa upande wa wanyama pori nataka Katiba ieleze wazi, - Wanyama pori wanakufa kwa ukame na hawa wanyama pori ndio wanaleta mali nyingi. Hawatambuliwi na tena ndio wanaleta faida kubwa. Kwa hivyo wawe wakihudumiwa kwa sababu wao ndio wanaleta faida kubwa katika jamii. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu. Benjamin Mwasi.

**Benjamin Mwasi:** Kwa majina najulikana kama Benjamin Mwasi kutoka Ndebwa. Yangu ni mafupi tu kwa sababu mengi ambayo yameongewa nafikiri tuko pamoja. Mimi nawakilisha Vagosi va Isanga. Katiba ya sasa iangalie wazee wa *walugongo* na wazee wa mtaa kwa sababu wao ndio kitindamimba kwa Serikali. Wapate chochote kile kwa huduma zao bora.

Mazingira: Katiba ya sasa irudishe ile sheria ya "Chief's order", ya ukataji wa miti, uchomaji misitu na kutolima kando kando ya mito. Katiba ya sasa iangalie uridhi - hasa wa ardhi. Ardhi iliyotengwa kwa manufaa ya vizazi vijazo kwa wakati huu kuna upatikanaji wa mimba kwa wasichana. Kwa hivyo kutengwe kama scheme ambapo hawa hawa watoto ambao hupatikana kwa nje ya ndoa wangeweza kupatiwa ardhi hizo. Katiba ya sasa iruhusu pombe ya kienyeji na kurudishiwa vilabu kwa kila location.

Katiba ya sasa ipunguze kiwango cha kodi ya mapato kwa mwananchi. Kuwe na ulinzi wa umma – "ombudsman" katika Katiba ya sasa. Katiba ya sasa itambue tamaduni zetu kuhusiana na mipaka hadi na kaya zetu kwa ajili ya manufaa ya vizazi vijazo. Katiba ya sasa irudishe kipengele ambacho hatuna sasa, bunge liongee Kiswahili moja kwa moja redioni badala ya kusomewa taarifa kama ilivyo wakati huu.

**Com. Keriako Tobiko:** Na la mwisho.

**Benjamin Mwasi:** Ndilo la mwisho. Katiba ya sasa iangalie walemavu wawe wakilipwa chochote kile kwa ajili ya uwezo wao. Asante. Hayo ni yangu ya mwisho.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Evans Ongongwo. Ametoka? Fegras Mwalenge.George Mwajala.

**George Mwajala:** Asante kwa nafasi hii na kwa jina ni George Mwajala nikiwa mwakilishi wa kanisa la kianglikana nchini Kenya. Katiba ijayo kwanza ningalipenda ikaweze kukutana na mahitaji ya kila Mkenya. Ikiwa kwanza elimu ya bure kwa wote. Madawa yawe kwa wote bure, maji yakaweze kumfikia kila mtu bure na hata yale maji yaliyoko katika nchi yetu na sehemu yetu ya Taita kama Chala, Jipe na Mzima springs yakaweze kutumika vyema kwa ajili ya kunyunyiza mashamba yetu na tukaweze kufaidika.

Nguvu za watu wengine zikaweze kupunguzwa kwa mfano zile za Rais ambapo anaweza ku-hire na ku-fire wakati wake apendapo.

Wananchi wawe na uwezo wa kutawala na kujiongoza juu ya hali za rasilimali zao. Judiciary ikaweze kuwa independent. Parliament ikaweze kuwa independent na supreme. Na equal sharing of the national cake ikaweze kupatikana kwa wote. Kuwe na sheria hasa sasa kwa upande wa dini. Uhusiano wa dini hasa kwa upande wa kuomba kwa sababu tuna uhuru wa kuabudu wengine wanaomba usiku hata kupiga kelele pasipo kujali wengine.

Kwa hivyo kuwe na uhusiano katika hali hiyo wa kuheshimu dini zingine. Na kama nitasimama kama mhubiri, basi mhubiri mwingine akiondokea asiweze kuanza kupiga dini ingine vita. Kwa hivyo tukaweze kuwa na uhusiano juu ya jambo hilo la kuomba.

Box la kupigia kura likaweze kuwa transparent na ile alama ya kupiga kura kwa sababu kutoka kule tunakoanzia elimu, ile alama ya upigaji kura ikawezwe kubadirishwa. Kwa sababu sote tunatambua alama hii ni ya (inaudible). Kwa hivyo alama hiyo ikaweze kubadirishwa. Kuara ziwe sikihesabiwa katika kituo na matokeo kutongazwa.

Mashamba yaliyonyakuliwa yakaweze kurudishiwa wenyewe kwa wakati wake. Mambo ya lease ikaweze kuondolewa, na National park ambayo katika Taita Taveta inachukua 62% ikaweze kupunguzwa mpaka kufikia 30% na ikaweze kutawaliwa na wananchi wa Taita. Kuwe na ulinzi wa jamii, barabara zilizoko zikaweze kuimarishwa vyema na watu walio na ulemavu wakaweze kutambuliwa vyema na wakaweze pia kupewa nafasi katika Serikali yetu.

Serikali tungalipendekeza ikaweze kuwa ya *majimbo* na waakilishi bungeni wakaweze kuwa sawa kwa sawa. Hawa wanaoitwa Provincial Administration waweze kuondolewa na waliostaafu katika Serikali wasiweze kupewa nafasi zozote za uongozi tena.

Uraia: Ule uraia wa kuzaliwa hapa kwa hapa utambulikane na uraia hata kama mzazi ni mmoja na yule ambaye ana-apply kuwa citizen akaweze kuwa paper citizen katika hali hiyo. Kwa sababu kuna wengine wamekuja na wameomba uraia wa Kenya na wamepewa. Basi waendelee kuwa paper citizens.

Mwisho, umri ikiwezekana kwa uongozi, kama tunavyojua katika Biblia takatifu katika Hesabu 8: 23-26, watu wanaombwa ikiwezekana miaka ishirini na mitano na akifika hamsini na tano, basi awe ameacha mambo ya uongozi awe ni mshauri tu. Kwa hivyo tunaomba hilo likaweze kuangaliwa. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Ferdinand Mwamburi.

**Ferdinand Mwamburi:** Kwa majina ni Ferdinand Mwamburi. Wana-commissioners tungeomba tuwe na Serikali ya majimbo kama ilivyopendekezwa na wengi na Rais asiwe juu ya sheria kama ilivyo Katiba ya sasa. Katiba vile vile ieleze majukumu muhimu ya Rais ambaye atakuwa mtawala wa nchi hii. Kuwe na utaratibu mzuri wa kupitisha jambo katika Bunge. Yaani wataalamu wa nyaja mbalimbali wawe wakihusishwa wakati mijadala fulani inapoendelea bungeni. Kubuniwe pia vikundi huru vya kutetea wananchi wanaonyanyaswa na watu hasa watawala ambao wanaomba omba kitu kidogo katika mashirika ya umma.

Kuhusu magendo. Katiba iangalie jambo hilo na ihakikishe kwamba imeweka vifungu ambavyo ni vizito kwa wale ambao wanafanya magendo na kuharibu uchumi wa nchi hii. Pombe ni jambo la jadi, na si la rahisi kuachwa. Mimi mwenyewe sikunywi pombe lakini naomba ikiwezekana ihalalishwe kwa maana mara nyingi polisi, - wale wanaolipwa na Serikali ndio wenyewe tena wanarudi wanapata mapato mawili - mengine kutoka kwa wananchi wale wanaouza pombe na kwa hivyo kuwanyanyasa. Pesa hizo kama zingelipwa kwa county council ..

**Com. Keriako Tobiko:** Ingekuwa nafuu. Sawa.

**Ferdinand Mwamburi:** La mwisho labda ni kuhusu maoni ya wananchi. Maoni ya wananchi tafadhali yaheshimiwe na mtakaporudi tena kutusomea maoni haya yawe ni hasa ni yale yale wananchi waliyoyatoa na isiwe kwamba yametoka katika sehemu fulani ya Rift Valley.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Juma Mwalimo.

**Juma Mwalimo:** Madam Commissioner na wote mliofika hapa ningependa tu kutoa maoni ya kwamba katika muundo wa Serikali iwe ni ya *majimbo* na pia ningependa kupendekeza ya kwamba mamlaka ya Rais yapunguzwe na huyu mhasibu mkuu awe independent. Tunaona wakati mwingine anatumiwa na katika hali ile ya kutumiwa ndiyo imefanya Kenya iwe vile ilivyo sasa. Na ningependa pia kusema ya kwamba bunge liwe independent yaani liamue mambo na lisitumiwe na Rais. Pia mahakama yawe independent.

Kwa upande mwingine, haki za wanaume. Nimeona kwamba kumekuwa na haki za watoto na za wanawake lakini pia haki za wanaume ni haki zilindwe. Wakati mwingine, wanaume wanasababishwa kufanya jambo - wale ambao wako low-minded. Unakuta kwa mfano katika upande wa mavazi, kuwe na kipengele ama sheria maalum ya kufanya kuwe na mavazi fulani.

Mwanamke anapo onekana na mavazi yasio stahili ikiwezekana achukuliwe sheria. Kwa sababu kuna nguo kama zile ziko transparent. Folders zinafanya tu mwili unaji……unaona. Sasa hapo unakuta wakati kitendo kama hicho kinachotokea mwanaume hatapewa jukumu la kuweza kusikizwa vile yalivyokuwa. Kwa hivyo ningependa kusema pia haki za wanaume ziweze kulindwa.

**Com. Keriako Tobiko:** Haki zipi hizo? Kama gani?

**Juma Mwalimo:** Kwa mfano kwa wakati huu unaweza ona kwamba kama mahakamani. Mambo yametokea na kwamba ni mwanaume ame…….labda vile mimi nimeoa .Unakuta ya kwamba badala jukumu pia la kusikizwa yale ambayo yametokea ndani ya nyumba yangu, sasa kwa sababu kumekuwa tu wimbo ni kwamba ni "haki za wamama," "haki za wamama," itakuwa ya kwamba sitapewa wakati wa kuweza kusikizwa kulitokea vipi mpaka kukawa vile. Kwa hivyo ningependa ya kwamba haki za wanaume ziweze kuangaliwa.

Kwa upande pia wa kuabudu, ningependa kwamba uhuru wa kuabudu uendelee kuwepo. Pasiwe na mipaka ila ijulikane kwamba ni Mungu watu wanaabudu. Na kwa upande mwingine ni kwamba kwa upande wa ardhi. Inaonekana kwamba mahali nilipo labda pametokea rasilimali fulani labda ingeweza kusaidia nchi ya Kenya, na inakuwa kuwa sitashauriwa tuwe na mapatano fulani - bali kwa sababu inasemekana kwamba fiti tatu ndizo zangu, basi kwanzia hapo chini kunatawaliwa na Serikali kwa hivyo unakuta naweza tu ondolewa pale bila haki zangu zenyewe kulindwa.

Kwa hivyo ningependa kusema ya kwamba ikiwezekana kuwe anayemiliki pale, amiliki mpaka pale mwisho kabisa. Ya kwamba chochote kilichoko pale chini ni yeye mwenyewe na ni mali yake. Pasiwe na vikwazo na pia hii Katiba ambayo itabuniwa ni kwamba kwa upande wa kwa mfano hii Taita Taveta tunaona asilimia sitini na mbili imemilikiwa na mbuga za wanyama. Kwa hivyo ningependa ya kwamba, na nafikiri itakuwa hivyo ya kwamba hiyo mbuga za wanyama ziwe mikononi mwa mwananchi. Sio eti asilimia fulani ipunguzwe bali iwe mikononi mwa mwananchi. Ikiwezekana labda sisi wananchi tuamue labda kupeleka sehemu fulani ndogo katika hiyo Central Government.

Kwa upande wa ufisadi, ningependa kusema ya kwamba mfisadi yeyote ambaye anaweza kupatikana ama ameendelea kupatikana maana ni wengi wamepatikana lakini kwa sababu mahakama haiko huru, wengi wameendelea kukaliwa, kufichwa na naweza nikasema ya kwamba; sitaona aibu kusema hivyo, wengi wameendelea kufichwa na mamlaka yaliyopo. Yaani Rais ameendelea kuficha wengine kuwaweka mfukoni wakati mwananchi anataka amtoe kwa mfano ningeweza kama wakati wa Kasarani---

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa ndugu, tuachane na mifano. Kwenda kwa pendekezo.

**Juma Mwalimo:** Ningesema ya kwamba wafisadi wote wasiendelee kuwekwa Serikalini. Ikiwa wananchi wamesema huyu ni mfisadi, basi asipatiwe nyadhifa yeyote. Na kwa upande mwingine wa tume zinazoteuliwa. Kwa upande unakuta kama ni tume ya Poverty Eradication. Unakuta wale wenyewe ambao ndio wameshiba - wajua mtu aliye shiba hata mjua mwenye njaa. Ningependa kusema ya kwamba wale ambao ni maskini wawe katika ile tume maana wao ndio wanaelewa shida ya umaskini.

Nitaongea juu ya ile inaitwa Regional Council. Kuwe na Regional Council na kuwe na County Council ili ya kwamba katika hizo mbili kutakuwa na uwezo wa kuweza kusimamia masilahi ya mkaaji wa pale kisawasawa. Kwa hayo machache ningependa kusema ya kwamba wakati wa maoni basi niyaone pale isiwe ni mambo tu ya kutufunga macho.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe pale. Crispus Colamodo. Ameshapeana? Crispin Mwakweda.

**Crispin Mwakweda:** Okay kwa Ma-commissioners na wananchi wote. Hamjambo? Kwa majina mimi naitwa Crispin Mwakweda na niko hapa kuakilisha wanao ugua maradhi ya ukimwi. Na jambo la kwanza kabisa ambalo linatukera sana ni kubaguliwa. Na nikisema kubaguliwa tunabaguliwa katika sehemu nyingi. Hata naweza sema sehemu zote.

Tunabaguliwa hata si kutegemea kuwa hata kama pia Katiba hii hii ambayo inashughulikia mambo ya kuigeuza hiyo Katiba ambayo imetuchokesha tayari ishatubagua. Ki vipi? - Mimi nilikuwa natarajia, au sisi tulikuwa tunatarajia labda tungepewa nafasi kando kabisa ya kuweza kujipangia mambo yetu na pawe na kikundi maalum cha kutuelimisha. Hiyo haikufanyika na kama mjuavyo wengi hatuwezi kuongea kama vile ninavyoongea hapa. Wengi hatuwezi kujitokeza kama vile nilivyojitokeza. Je maoni haya Commissioners wetu, mlikuwa mnafikiria tungeyaleta kivipi? Mshatubagua na nyinyi pia.

**Com. Keriako Tobiko:** Ndugu yangu wataka nikujibu saa hii ama namna gani?

**Crispin Mwakweda:** Nijibu.

**Com. Keriako Tobiko:** Tuna uwezo kama unasikia kuna kitu huwezi kuzungumzia kwa public, na imefanyika nafikiri kama umesoma gazeti ilifanyika Mombasa jana. Akina mama walikuwa hawakutaka kuongea mambo mengine, wakapelekwa room ingine yao tofauti. Kama kuna kikundi au mtu ambaye anasikia kuna kitu ambacho anataka kutuambia na hawezi kusema kwa public, unaweza kutuomba tuweze kuwa na kikao. Tunasema 'proceedings in camera'. Okay? Kama wewe na wenzako wanataka tufanye namna hiyo, tunaweza kufanya mipango hiyo. Lakini kama unaweza ongea vile, sawasawa tu lakini kuna hiyo procedure.

**Crispin Mwakweda:** Kwangu mimi sina shida. Nimezoea hivyo. Isipokuwa ni kwa wenzangu wale ambao tuliketi tukaongea. Pale tuliketi tunajua pahali tuliketi lakini haingekuwa hivyo kama tungepata msaada fulani, tukaelimishwa kado, tungekuwa huru zaidi. Lakini ilinigharimu hasa mimi kutembea na kupata hawa ndugu zangu. Ilinigharimu mimi binafsi ambapo haingekuwa ghalama yangu kufanya hivyo ndio maana nasema hivyo. Lakini mimi sina shida.

Sasa nasema hivi, hapo kwanza tumeelewana ya kwamba tumetengwa. Tumetengwa hata pia katika hizi mikao au ………..kuna kamati ambazo zinahusika na mambo hayo. Kamati hizo zinaanzia kwanzia national, hatujahusishwa na kama tumehusishwa, hatujafahamishwa. Wenzetu hatuwajui. Hawajawahi kufika kwetu tukawa tunaweza kuasilisha shida zetu. Kwa hivyo tunasema hatujawakilishwa. Unajua wengine labda watanipinga waseme 'wako wapi?' Lakini kama wako, wametoka wapi? Walichaguliwa na nani? Jukumu gani wanafanya? Hatujui.

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa wacha nikuulize hivi. Wacha nikuulize. Ni pendekezo gani uko nazo unataka tuingize kwa Katiba mpya. Tafadhali.

**Crispin Mwakweda:** Naja naja. Sasa basi kwa sababu ya shida kama hizo tunapendekeza hivi, - katika lile baraza kuu hatuna haja na ma-professor pale juu. Tupeni daktari mmoja, tupeni mtu shupavu zaidi ambaye anahusika na fedha, na tupatieni waakilishi. Mmoja kutoka kila mkoa awe katika lile baraza. Mwakilishi huyo asiwe kwa mfano Pwani tupate Omondi anawakilisha, au Kamau anawakilisha. Kamau hajui mila za Mkoa wa Pwani, Omondi hajui, Muli hajui. Tunataka kama ni Mwadime, tunajua yeye Mtaita. Tunajua kama ni Mnene, tunajua ni Taveta. Mambo kama hayo. Watuakilishe pale. Tukija kwa mkoa hivyo hivyo. Mkoa ile kamati ya mkoa tuakilishwe na tuakilishwe vivyo hivyo. Mtaita awe pale.

**Com. Keriako Tobiko:** Haya hiyo tumeandika.

**Crispin Mwakweda:** Ukija kwa location, tuwe katika kila kata.

**Com. Keriako Tobiko:** Pendekezo lingine?

**Crispin Mwakweda:** Pendekezo lingine ni kwamba jamaa zangu hawa ambao wana shida hiyo wana shida ya kuelimisha watoto wao, - hafanyi kazi. Wale walikuwa wanafanya kazi washafutwa tena katika hali ambayo si nzuri. Bursary maalum zitengwe kutokana na mfuko huo, hawa jamaa zangu wapawe. Na kamati za kata ambazo zinahusika na mambo ya ukimwi zihusishwe katika hizo bursary. Nafikiri haya yote yakitekelezwa, mambo yataenda vizuri. Isipokuwa naomba hivi, mimi nina haki kama binadamu mwingine hivyo nilikuwa naonelea nina haki pia ya kuongezea mawili matatu.

Nasema hivi: Mengi tumeongea kuhusu Katiba, lakini kuna kitu kidogo kinanikera. Kuna kitu mbeleni kabisa hata saa ile nikiwa mtoto kilikuwa kinaitwa "Vagrants" na nina pendekeza hiyo irudi. Kwa sababu gani? Kuna watu wametoka mikoa mingine au districts zingine wamekuja kujificha Mwatate eti wamekuja kutafuta mawe, eti wamekuja kutafuta ardhi na ni waalifu walipotoka. Wanafanya makosa, anapotea miezi miwili mitatu, anarudi - Vagrants irudi. Kama ulipewa Vagrants huko kwenu hata kama imekwisha, ibaki huko huko ukija ukipatikana na kosa upewe Vagrants, Chifu ajue, DO ajue, DC ajue - uchanganye.

Umekuja labda unataka mambo ya ardhi, unataka ardhi, au unakuja kufanya kazi, kwanza una-report kwa District. Unakuja u-report kwa Division, nenda kwa Chief ajue. Utaweza kaa sub-location gani, Assistant Chief ajue na *mwalugongo* atajua - ukifanya kosa, juu yako ni barabara unaonyeshwa. Vagrants tunasema irudishwe.

**Com. Keriako Tobiko:** Hiyo tumeandika.

**Crispin Mwakweda:** Nafikiri kwa hayo machache wacha nikwamie hapo.

**Com. Keriako Tobiko:** Okay sawasawa ndugu. Joan Muhaya. Hayuko? Abdullah Muhammed.

**Abdullah Muhammed:** Kwa majina mimi ni Abdullah Muhammed Mwashi. Maoni yangu kuhusu Katiba ni kwamba, kwanza Katiba iweke kifungu cha sheria ihalalishe mahakama ya kiislamu. Yaani Katiba ya Kenya iwe pia ina mahakama ya Kiislamu. Halafu mahakama yenyewe imhukumu muislamu akimfanyia kosa muislamu mwingine, au muislamu kumfanyia kosa asiyekuwa muislamu, au asiyekuwa muislamu kumfanyia kosa aliye muislamu.

Kuwe na *Chief Kadhi* pamoja na *Makadhi* wake wasiopungua wanne na huyu *Chief Kadhi* na wafanyi kazi wake wasiopungua wanne, kazi yake iwe ni kuhusiana na ndoa na uridhi peke yake. Kuwe na baraza kuu la Kiislamu kama vile ilivyo sasa ili tuzidi kupata nguvu. Waislamu wawe na haki sawa Serikalini na mtu ambaye si muislamu. Kwenye Msikiti karibu

kusiruhusiwe kujengwa bar kwa undani wa metre mia tano. Polisi wa Kenya wasimfuate mtu mhalifu mpaka ndani ya msikiti kwa sababu hata msikiti wenyewe pia haukubali kuweka mhalifu.

Kuwe na Rais wa Kenya nzima halafu kuwe na Serikali ya majimbo na itawaliwe na Rais wa kijimbo. Kuwe na kitambulisho cha kitaifa na kuwe na kitambulisho cha jimbo ili ujulikane kwamba wewe ni Mkenya lakini ulitoka jimbo gani na gani. Kuhusu passports, mtu akitaka passport, basi apewe passport ile bila masharti yeyote. Kwa mfano kama vile birth certificate au barua ya pahali ambapo anataka kwenda ni wapi. Kwa sababu wewe kitambo utoe kitambulisho, kitambulisho huwezi kupata bila kupata birth certificate. Serikali itangazie wananchi kodi yote ile ambayo inakusanya katika Kenya kwamba imepata kodi ya pesa ngapi katika mwaka huu halafu ndio itangaze Budget yake ya mwezi au ya mwaka.

Kuhusu kupandisha bei ya vitu: Serikali isipandishe bei za vitu hivi hivi kabla haijapandisha mishahara ya wafanyikazi na mapato mengine yoyote ya mwananchi wa Kenya. Kuhusu maandishi kwenye ofisi za umma, ziwe kwa lugha mbili, - iwe na kizungu na iandikwe kwa Kiswahili. Kiswahili ni utamaduni wetu wa mwafrika hapa Kenya. Tukiangalia nchi zingine kama vile Ujeremani wao wanatumia Kijeremani. Mwenye kufanya kazi za mkono ofisini asiwe na lazima kuwa awe amesoma. Hata mtu ambaye hajasoma anafikia mahali anajua kupika chai na ofisi yenu yahitaji mtu wa kupika chai, basi yeye ajiriwe kazi bali na masomo.

**Laughter from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa chukua zile muhimu sana, mbili halafu umalize. Kwa sababu tuko na watu mia mbili thelathini na moja.

**Abdullah Muhammed:** Muhimu mbili ni kwamba: Kuhusu wanawake haki zao sawa. Mimi nachangia kwamba mwanamke ambaye ameolewa haki sawa ameipata kwenye cheti chake cha ndoa. Kwa hivyo ukijua wewe umeolewa, haki yako iko kwa bwanako. Na kama bwanako atakuwa amevunja haki sasa wewe pahali ulipoozwa sheria zote ziko pale, utakwenda patanishiwa pale ama utakwenda achanishwa pale. Kwa hivyo usifanyie bwanako kosa ukijua kwamba mimi nikipigwa basi nitakwenda mshitaki. Utazabwa bwana.

**Clapping from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** La mwisho.

**Abdullah Muhammed:** La mwisho ni kwamba nazungumzia kuhusu afya na elimu. Afya na elimu, Serikali sasa haina lengo la kuua raia wake lakini inaua kimakusudi. Kwa sababu sasa imekuwa matibabu ni ya matajiri. Kwa mfano mimi nimetoka ndani ndani, bibi yangu anataka kuzaa, niende nikodi gari maanake hospitali haina ambulance tena ile hospitali pia nikalipe zaidi ya elfu moja. Nitazitoa wapi sina kazi? Kwa hivyo sekta ya afya iwe bure na sekta ya elimu iwe bure. Hayo mengine yote yako kwa

memorandum.

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa wacha niseme hivi. Kama kuna wale ambao wako na memorandum na hawataki kuongea, wanaweza ku-file na ku-register badala ya kukaa hapa na kungoja uitwe. Unaweza tu kwanza kwenda ku-file na u-register na uende. Wale ambao wako na memorandum na hawataki kuongea. Tumesikizana? Okay. Rashid Mwamburi. You have a question?

**Speaker:** Naona kama wale wameongea wanasoma kutoka kwa memorandum.

**Com. Keriako Tobiko:** No, everybody else is only highlighting nobody is allowed to read the memorandum. So, I am talking of those who have memorandum and they do not want to even highlight. So you can just present the memorandum, sign and you go. Rashid Mwamburi. Yes, ndugu yangu. Ndiyo yupi? Rashid Mwamburi. Ameenda. Joseph Ngalu. Nathan Msongoli. Jacob Ngomo. Daniel Mwang'ombe. Stephen Kileta. Jared Babu. They are all there. Okay, wanapeana.

**Jared Babu:** Asante sana. Maoni yangu mengi yamesemwa na haja yangu tu ni…..

**Com. Keriako Tobiko:** Taja jina lako kwanza.

**Jared Babu:** Jina langu naitwa Jared Babu nimetoka katika tarafa hii ya Mwatate, location ya Kilayangerenyi. Ningetaka ku-recommend kwamba tuwe na Serikali ambayo itatuletea umoja, amani na upendo na wala si corruption na dictatorship na mambo mengine kama hayo. Isiwe ni Serikali ya kutumia mabafu, iwe ni Serikali ambayo inaangalia haki za watu. Pia tuwe na uchaguzi ambao utakuwa free and fair. Na National wealth iwe inaweza kutawalwa na County Council. Twataka pia kuwe na checks and balances between the three arms of Government.

Powers of Parliament: Iwe wanaweza ku-vet and approve the Executives' public appointments. Parliament iwe pia inaweza ku-summon na ku-censor Ministers. Parliament iwe pia na power ya ku-impeach the President. Parliament pia iwe na power ya kuweza ku-create na dissolve ministries. Parliament pia iwe na uwezo wa ku-summon na ku-censor constitutional officers. Parliament must approve all Government expenditures. Parliament must determine its own calendar. Parliament to enact laws. Parliament to have power to set up Commissions to discuss matters of national importance.

National resources: The Constitution should entrust all national resources in the people and not in the Government of Kenya.

Form of Government: We recommend a system that would give the regions a lot more saying in how the taxes they pay are used for their own good and what proportion of that should be surrendered to the Central Government. Functions mainly related to national security, foreign policies and participation of regional and local affairs which can best be handled by larger

entity should be left to the Central Government.

Land tenure: We recommend Constitution to contain economical land distribution seeking for the prosperity of the Taita's future economy.

Land in mining: We recommend that mining prospecting rights iwe inatawalwa na Local Authority.

**Com. Keriako Tobiko:** Mzee Babu.

**Jared Babu:** Sir.

**Com. Keriako Tobiko:** Taja la mwisho sasa. La muhimu kabisa. Hilo lingine tutajisomea kwa memorandum.

**Jared Babu:** Group ranches: Tunaomba hizi zikatwe, zipewe wananchi katika sehemu za ten acres. Na pia hii mambo ya settlement, hatutaki iendelee kwa sababu inafanya wageni kutoka nje kuja kutawala, kuchukua nchi hapa. Na hiyo naishia hapo.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mzee wangu. Gerald Nzano. Donald Mbongosa. He is gone. Venant Mjomba.

**Venant Mjomba:** Bwana Mheshimiwa mimi kwa jina ni Venant Mjomba, Councillor wa Mwachabo ward. Mengi yametajwa lakini nimeona wakati walipokuwa wakitaja tena ulikuwa unaandika. Kitu cha kwanza: Lease. Lease mtu akipewa shamba lease ninety nine years huwa umempatia forever and ever. Hiyo lease iondolewe. Lease iwe pengine forty five au hata twenty five years. Tosha kazi.

Ya pili, Taita Taveta ndiyo ya kwanza kuwa tajiri lakini ndio ya mwisho kwa umaskini. Kwa sababu mashamba yetu yamechukuliwa na mbuga za wanyama. Kwa hivyo mbuga za wanyama zirudi kwa wananchi wenyewe. Badala ya kuwa na national park tuwe na game reserve ambapo itakuwa Taita Taveta Game Reserve.

Bwana Mheshimiwa, wewe umetoka kwa mwalimu, mimi nimetoka kwa mwalimu. Kwa hivyo walimu wanastahili kupewa mshahara wa hali ya juu kuliko watu wengine zaidi. Ya pili Bwana mwenyekiti, tuko hapa kwa sababu ya usalama. Kama usalama haungekuwako hatungekuwa hapa. Watu ambao wangefuatilia ni watu wa usalama pia ni watu wa kuangaliwa mishahara ya hali ya maana zaidi ili waweze kutulinda vizuri zaidi. Ningetaka kwamba Minister, awe ni Minister na Mbunge awe ni Mbunge.

Siku hizi tunasema kwamba tu-create jobs kwa wale wengine. Lakini utakuta mtu kama mimi Councillor, utakuta nina cheo

kingine, nimepewa kazi, cheo kingine nimepewa kazi na watoto wangu watatu, wanne wako nyumbani hawana kazi. Kwa hivyo kazi moja mtu mmoja. Bwana mheshimiwa, mambo ya shamba, tangu zamani babu zetu na babu zetu walikuwa wana mashamba ambayo hii inaitwa Land Adjudication, - yaani mashamba yao yanabaki vipande vipande vile ilivyo. Sasa sisi tumeambiwa Land consolidation kwa hivyo hii "Land Consolidation" imepatia watu wengine zaidi kutuibia mashamba yetu. Tunataka mashamba yabaki vile babu zetu walivyokuwa na kama ni title deed itatolewa kupatana na vile vipande vilivyo.

**Clapping from the audience.**

Land settlement. Settlement imefanya kwamba mtu anatoka mahali hatujui ametoka wapi anakuja kuja ku-settle mahali ambapo si kwake. Mambo ya settlement iondolewe mbali, shamba iwe ni mahali watu walio pale pale ndio shamba zao hizo.

Haki: Utakuta mtu ambaye hana pesa ameshitakiwa mahakamani, mtu aliye na pesa anaandika wakili. Sasa huyu ambaye hana pesa ananyanyaswa kwa sababu hana wakili. Lakini yule ana pesa, atanyang'anya yule mtu ambaye hana pesa kwa sababu anatumia wakili. Mawakili wawe wa watu ambao wasiojiweza katika mahakama.

**Clapping from the audience.**

Kwa mfano, Chief, Assistant Chief, DO akikosa, utakuta pengine akipelekwa mahakamani utakuta yule mtu wa Serikali ana wakili anamtetea. Lakini utakuta huyu kwa sababu yeye ametoka mahali ambapo si pa sawasawa hana wakili. Kwa hivyo tunaomba wakili awe wa watu wasiojiweza.

**Com. Keriako Tobiko:** Tumeandika hiyo.

**Venant Mjomba:** Mwisho naomba hii Katiba vile tunavyoenda, mwishoni tupate yote ambayo tumeyazungumza na tuweze kuyasoma, tuone ni yale ambayo tulipendekeza. Asante sana, Mungu awabariki.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Kimunga Shuke.

**Kimunga Shuke:** Asante chairman kwa kupata nafasi hii ya kuzungumza na yote yalizungumzwa na wenzangu, nimekubaliana nayo. Lakini mimi kitu kinachoniumiza na kitu ambacho kinaudhi watu wa Taita hapa ni mashamba. Kitivo kila mtu anakupenda na kuna wenyewe asili yao walizaliwa pale. Na wakija watu kutoka huko, wanaletwa na wanasema "hapa hapa." Wewe mwenyeji wa pale ulizaliwa pale unaondolewa. Unapelekwa pahali pengine, yule mgeni anawekwa pale.

Pengine wewe baba yako alikuwa na mashamba mengi makubwa sasa leo mengine unapokonywa. Ni wale wale watu wa ardhi kushirikiana na watu wa Serikali, wanasema "huyu hana uwezo, huyu hajiwezi tumnyanyase." Basi yule mwenye pesa

amenyang'anywa. Wengine hata hawakupima hayo mashamba walinyang'anywa. Akijaribu kwenda hivi, anaendewa hivi, akijaribu kwenda hivi, anaambiwa hivi. Kwa sababu nini? Hana chochote. Yule mwenye pesa ndiye anufaika. Kwa hivyo naomba Serikali na Katiba ya sasa iondoe hiyo consolidation. Watu warudishiwe mashamba yao. Na wale wasiopima wapime mashamba yao. Sina mengi mimi.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mzee. Jiandikishe hapo Mzee wangu. Pascal Kilimo. George Ngwayi. George Ngwayi alikuwa ameongea. George Ngwayi had spoken. Ni wewe?

**George Ngwayi:** Nawasalimieni nyote, niko hapa kwa ajili ya marekebisho ya Katiba. Kwanza ni mashamba. Katiba irekebishe mambo kuhusiana na kugawa ardhi. Mamlaka ambayo ilikuwa ikitumika na wazee ya kugawa ardhi irudishwe. Tunajua kwa mfano ya kwamba mimi niko na wazazi na wazazi hao ndio wanaotumika kunionyesha shamba langu mahali itapitia. Lakini si mtu kutoka nje aje kunirekebishia shamba ama aje kunigawia shamba hiyo. Kwa sababu sisi tuko katika hali ya kimbari. Na mbari tunajua mbari yetu imeshikana namna gani. Kwa hivyo Mzee anayesimamia mbari yangu ndiye anayeweza kunigawia mahali itapitia. Kwa hivyo mamlaka yale tulikuwako na wazee wa mbari, hao wazee wa mbari ambao walikuwa wakigawa mashamba hayo warejeshewe mamlaka hayo kwa sababu wanajua mipaka za ardhi zetu.

Tukirudi kwa mambo ya pori ya wanyama. Pori ya wanyama vile nionavyo hazitufaidi chochote kwa maana tukiangalia hapa tunalalamika maji, tunalalamika barabara. Pesa hizo ingelikuwa heri kuingiza maji katika mashamba ambayo tunatumia kwa wakati huu na ikaweze kutusaidia. Na tena zitumike kwa kuingiza barabara. Tukiendelea pia na shamba la mkonge, sioni kama linatufaidi chochote. Ni heri lile shamba la mkonge lingeondolewa lingeuzwa kwa njia ya kusaidia wananchi.

Mgeni yeyote asigombee kiti katika mahali pa mwenyeji bali akae asikize vile atakavyotawaliwa na mwenyeji. Tena mgeni asiishi ndani ya mwenyeji ikiwa amekuja kibiashara basi kuna mahali kwa biashara. Lakini asiingie ndani akianza kutawala nchi vile ilivyo kwa sababu ninajua ukiona chakula chako ghalani, mtu akianza kula chakula hicho, itabidi uweke dawa ya panya.

Kwa sababu inakufanya uanze kula chakula kile kwa haraka na utakimaliza mwishowe utaanza kutafuta chakula kwingine. Kwa hivyo ni chakula ambacho ni cha Mtaita kinastahili kile chakula Mtaita akule kwa polepole. Asijiharakishe kwa sababu kama panya zimekuja kuharakisha chakula kile, basi itabidi panya zile ziwekewe dawa ya panya kama sivyo kama ni za mtu, ziondolewe zile panya na zirejeshwe mahali inapotakikana.

**Clapping from the audience.**

**Com. Keriako Tobiko:** Okay sawa sawa. Hiyo tumeelewa.

**George Ngwayi:** Tukirudi kwa upande wa mavazi. Mimi najua labda nina dada zangu ama nina wazazi. Lakini siwezi kutoka

kwa nyumba nikiwa nimevaa sawa na dada yangu. Ikiwa tutavaa sawa na dada yangu, haitajulikana dada ni nani na kaka ni nani. Kwa hivyo lazima turekebishe mavazi hayo. Ama kama utapatikana nguo ambayo haina heshima, basi kama Serikali haitarekebisha mambo hayo basi ruhusa iwe mwanamke akipatikana amevaa vazi la jinsi hiyo ambalo linaweza kufanya mtu asiishi kwa amani, lishikwe likatwe mbele ya watu. Na atembee uchi maanake anafanya kutembea uchi – Maanake anapenda kutembea uchi. Yangu ni hayo.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante, jiandikishe hapo. You are not amused? Nicholas Kalela.

**Nicholas Kalela:** Asanteni. Mambo ya Constitution mimi naelewa kwamba ni chombo cha kuelekeza wananchi wote vile watakavyoishi kwa miaka mingi ijayo. Na kwa hivyo ikiwa tutakubaliana hivyo ni kwamba kuendelea kujigawanya kwa vipengele vipengele haitakuwa ni sawa. Maana Constitution hii ni ya miaka milele na milele. Kwa hivyo mimi ningefikiria kwamba Constitution hii itazingatia hali ya kurekebisha uchumi. Hali ya kuhakikisha kwamba mwananchi yeyote yule wa kawaida anapata chakula chake, anapata elimu na anapata security ya kutosha.

Lakini security lazima iwe na mahali pa kutoka. Kutoka kwa security hatuwezi sote ku-manage. Lazima tuwe na Serikali ambaye inachukua jukumu. Jukumu hilo ni la defence ya nje, kuzuia vita na ndani pia kuzuia criminals ambao wanaweza kuletea watu shida. Hii ina maana kwamba tunastahili tuwe na mwongozo. There must be guidance, vision and quality ambayo inatokana na Constitution.

Jambo lingine ni mambo ya citizenship ambapo kweli katika Katiba iliyoko, wakati mwingine inakuwa vigumu kujua ni nani atakayeitwa mzalendo, ni nani atakayeitwa mwananchi, na katika kuandikishwa kunakuwa shida. Lakini naamini hivi; wengine wamesema lakini la mwisho kabisa ni kwamba wengine wanasema kuwe na watu ambao wanaweza kuwa na dual citizenship. Mimi sioni kama ni sawa. Kama ni mwananchi awe ni yule yule mwananchi na tunayemtambua na kitambulisho kiwe ni ile ile national identity card.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya nomination of MPs. Hili ni jambo ambalo lisingekuwako. Na mimi nilikuwa nafikiria kwamba pia wanawake kwa vile ni wengi waweze kupambania viti kama ilivyostahili au inavyostahili.

**Clapping from the audience.**

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya mishahara. Ni wazi kwamba kama nchi haitakuwa na mwelekeo wa kusema watu watalipwa vipi katika kila section, basi hapo tunapotea. Tumeona katika muda uliopita kila mtu anaamka anasema “mimi nataka kulipwa hivi, mimi nataka kulipwa hivi.” Kwa hivyo Katiba itoe mwelekeo wa kusema kwamba sheria ya kujua watu watalipwa vipi ni Wabunge, ni Madiwani - katika national level, ni Walimu, ni Madaktari ili ukiwa mahali pengine ama katika sekta ingine ujue mtu wako ambaye mnalingana ni nani. This is what I think should be able to happen.

Kuna jambo la Rais awe amesoma akafika wapi. Kulingana na mahali tumefikia, inastahili kwamba Rais wa nchi awe amefika kiwango cha University. Kuna mambo ya uchaguzi wa madiwani. Nomination isingekuwako lakini kama itakuwako iwe ni kwa option. Kwamba watafute wataalamu ambao wanahitajika na baraza lile la sehemu ile liweze kuchagua ama ku-nominate wale ma-councillors wanao hitajika.

Jambo lingine ni kuhusu mambo ya ardhi. Wananchi wa Mkoa kwa jumla wamepata shida sana kwa wakati uliopita kwamba mashamba yao yamegawanywa bila wao kujua. Na yalipogawanywa bila kujua, kunakunjwa watu wengine wanaitwa ma-squatters na wameishi hapo jadi. Wazee wamekaa wakaachia watoto wao na sasa ni majukuu na wajukuu wanaitwa squatters. Hili ni jambo ambalo linastahili kurekebishwa na likisharekebishwa amani itaingia.

Jambo lingine ni kuhusu mashamba lakini ningetaka kulisema hivi; Kwamba nchi inastahili kutayarisha chakula chake na ardhi ndio mahali ambapo chakula kinapotoka na yale mambo ambayo yako sasa katika Constitution ya sasa ni kwamba kila mtu anastahili kuchukua ardhi na afanye vile anavyotaka katika ardhi. Ningeona kwamba kutengwe sehemu ambayo itakuwa ni ya kutoa chakula. Sehemu hii iwe inamilikiwa kwa muda – kuwe na lease za wakati mchache, ikiwa yule ambaye anaendesha katika ardhi hiyo, tuseme ni one thousand acres, isiwe ni yake. Iwe mtu mwingine yaani huyo akimaliza kushughulikia hiyo ardhi, basi mwingine aweze kupewa na aendelee kutoa chakula kile kile kwa ajili ya nchi. Tumeona katika sub-division ambazo zinaendelea, watu wameenda mpaka wamebaki na visehemu vidogo ambavyo 'they are no longer productive'. Na umaskini unaingia. Hiyo ina maana kwamba tunaweza kutayarisha….

**Com. Keriako Tobiko:** Maliza.

Tunaweza kutayarisha makao ambayo yanastahili watu wote kuishi.

Jambo lingine ni mambo ya sheria ambazo ziko. Tunaomba Constitution irekebishe, ipee mwelekeo wa kurekebisha zile sheria ambazo zimedumu mpaka sasa, hasa katika Mining Act ambayo inazuia wakazi kama wa Taita Taveta ambapo madini nyingi inatoka lakini hawana uhuru wa kuyatumia vile inavyostahili.

Misitu na mahali pa chemichemi na kwote ambako kuna national resources kuweze kulindwa bila kupunguzwa kwa wakati wowote. Jambo la mwisho ni kwamba tunaweza kutengeneza Constitution nzuri kabisa lakini ikiwa sisi wananchi hatutakuwa na morals ambazo ni za sawa, hatuwezi kuwa tunafaidi kitu.

Tunatakiwa Constitution hii ielekeze watu kuondoa mambo ya corruption, kuondoa mambo ya grabbing of land na kadhalika. Hii imeleta shida na ndio maana sasa wakati huu inaonekana kwamba tunataka sheria. Lakini sheria ni sisi wenyewe tubadirishe nia na tuweze kujua huyu ni ndugu yangu na huyu ni baba yangu na huyu ni mfanyikazi wa Serikali. Inakuwa vigumu kueleweka

kwamba tunaweza kuendelea kuishi vile watu wengine wanasema ati tuishi tukisema tutaishi “haphazardly”. Haiwezekani. Thank you.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe na uwache memorandum yako hapo. Councillor Juma Sese.

**Councillor Juma Sese:** Okay. Asante sana Commissioners. Naona mengi yamezungumzwa na kama vile tunaanza kwa kurejelea majina mimi ni Councillor Joseph Juma Sese wa Bura ward na labda ndio katika kama bahati ni kama kijana ambaye yuko kwa uongozi. Kwa hivyo utaniruhusu kidogo nikiwa naongea nitakuwa upande mwingine nasisitiza kueleza maana vijana ndio tunatarajia maisha ya baadaye tuwe.

Mimi langu la kwanza ninaanza na hii Presidential seat. Mimi maoni yangu na vijana wengine na kama kiongozi, hii Presidential seat tunaomba iwe rotative. Kumaanisha kwamba toka tupate uhuru Mkikuyu ameongoza Kenya, Mkalenjin akaongoza. Na kama saa hii inafuata ni two term, wakiwa wanasimama kwa President tusione Mkikuyu tusione Mkalenjin. Awe amesimama kabila nyingine hata kama ni Mtaita anaruhusiwa. Na ikitoka ile kabila ambayo imefuata kama Mkikuyu na Mkalenjin aliongoza, basi waziregelee moja kwa moja kupite atleast ten years - Hapo ndio tutazuia samaki wandogo kumeza wakubwa. Maana kuna makabila hayawezi kulinganishwa na vingine. Na tumeona mfano mzuri hapa hapa Tanzania kwa majirani. Na hiyo hiyo imeenda mpaka kwa vyama. Kwa mfano mfumo huu unaokuja wa kura, chama cha Kanu kiwe kimekuja kulikuwa na Mkalenjin na Mkikuyu kwa hivyo wasi-nominate Mkalenjin ama Mkikuyu. Chama cha DP hivo hivyo, Ford People hivyo hivyo.Hawa makabila wengine na wenyewe wapate nafasi ya kuongoza.

Jambo la pili ni katika mambo ya doctors kuimarisha mambo ya medicals. Iwekwe sheria katika hizi professions ambazo courses ziko katika University. Especially kama Medicine Veterinary aviation, iwe kwamba mtu yeyote anaye-graduate kwa medicine, for the first five years katika hizi public universities, he or she should not be allowed to fly out of the country or to work in a private sector. Iwe ni lazima miaka ya kwanza mitano yule amehitimu katika University, amechukua medicine, lazima awe kwenye Government. Hivyo tutapunguza tatizo la madaktari.

Nikiiruka ya tatu haraka haraka katika upande wa elimu. Kusaidia elimu baadaye iendelee, iwe kwamba mtu anayeongoza kwa chuo labda ni mwalimu mkuu Secondary ama Primary na wewe kwa miaka mitatu matokeo yamekuwa yakitokea mabaya, basi automatic sio kwamba umepata demotion ya kuondolewa head teacher, lakini pia salary scale iteremshwe.

Katika upande wa education nikaona kutoka nursery mpaka Secondary, ikiwezekana iwe free. Katika post ya DDC tutaomba iwe ni post inaweza ikashikiliwa na Mtaita. Sio mtu atoke labda ni Kisumu, ni Ubaniani wapi ndio chairman halafu anakuja kutuambia vile tutafanya mambo hayo. Chairman wa DDC asiwe District Commissioner. Katika Councillors, hata wenzangu walikuwa wanaomba ikiwezekana form four lakini tunasomesha watoto. Hata ingewezekana badala ya kuanzia form four and above, hata ianzie diploma and above.

Halafu kuna jambo hili la State house Comptroller. Maoni yangu nikaona kwamba State house Comptroller abaki ile ile kabila ya yule kiongozi. Hata tunaona hiyo ndio kama security ya mtu binafsi na hata hawa security bodyguard. Saa zingine huyo mtu ni Mbaluhyia halafu apewe security bodyguard labda Mjaluo. How are you sure that you are going to be secured?

Halafu natural resources zetu zirudi ziwe chini ya County Council of Taita Taveta na kila mahali katika Local Government. Na kuongezea iwekwe kwamba maji na umeme katika hospitals ziwe ni free of charge. Sio kwamba unaenda hospitali unasikia hospitali imekatiwa maji kwa hivyo operation haiwezi kufanywa. Hayo ni mambo yanatokea Taita hata wakati mwingine Voi hospital.

Walemavu ikiwezekana, kuna wale walemavu ambao wanaweza kusoma - labda ni mguu ama mkono uko na kasoro. They should be considered to be given free education hata ya colleges. Kuna wale wazee wamebahatika wameishi vizuri wakafika zaidi ya miaka sitini na tano. Inatakikana hata kama alikuwa ni mkulima na hakuwa kwa N.S.S.F na mengine, awe anatafutiwa pension at least kama 2,500 per month. Anaweza kuwa hana watoto ama watoto wake wote wamekufa. Sasa yeye atategemea wapi? Sasa wazee wengine watakufa na age yao haijafika.

Katika mambo ya Councillors, allowances na salaries tunapendelea since they are politicians na wenyewe walipwe na consolidated fund - Sio kulipwa na mabaraza. Katika hii post ya Assistant chiefs na Chiefs, nitaomba kama wengine walivyotangulia kusema ikiwezekana wachaguliwe waketi two terms, - kwangu nitaingilia upande wa salary. Tukitaka ku-avoid mambo mengi kuwalaumu pia salaries za Chiefs na Assistant chiefs ziwe katika zile kuwa considered.

Halafu na upande mwingine, law ya Chief isaidie. Nikichagua ni moja ni moja maana naona unataka kunionya …

**Com. Keriako Tobiko:** Maliza, sasa wakati wako umeisha.

Ninaenda katika hizi associations ambazo zinakuja. Tutaomba associations hizi zinatengezwa mara nyingi kama ni kutetea haki za watoto, za akina mama, ziende kulingana na mila. Usiniambie inaweza kuwa ni desturi labda mama amekosea na umempiga makofi mawili, kosa lake haliangaliwi sasa ni mimi kutafutwa. Na kwa watoto ikiwezekana, caning in primary schools and in Secondary kama sisi tulisoma na viboko virejeshwe kuamua watoto wanaosumbua.

Mwisho, kila mtu akimaliza form four itakuwa ni vizuri, ikiwezekana apelekwe kwa N.Y.S training ambapo inawatengeza watoto. Na majeshi yetu ya Kenya tumeona kama nchi nyingine wamekuwa, ukiambiwa ni mwanajeshi unaona ana kitambi na jersey. Ikiwezekana kuna courses kama za kutengeza barabara. Kama hizi zinazofanywa kama na China road. Badala ya watu kuketi kwa Barracks, Kenya ni nchi ya amani, wafundishwe courses kama hizo. Wakiwa wanatengeza mabarabara na wanashughulikia mambo mengine hata repairs kwa institutions, we will be saving for the Government. Hiyo itakuwa ndiyo kazi

maana huwa tunachagua watu wako strong na healthy. Asante.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Record. Ndugu yangu, Commissioner ana swali.

**Com. Kabira:** Umesema ukipiga mama makofi mawili tu na makosa yake iangaliwe ionekane kama ni makosa mabaya …

**Councillor Juma Sese:** Vile nataka kueleza naomba nifafanue, utakuta wewe mwanaume umefika labda ni saa kumi na mbili jioni, mama ameingia saa tatu, sasa unamuuliza ni vipi? Anaweza kuwa amekurushia maneno mengine ambayo yako-recorded mahali na discipline ya kiafrika, umemchapa makofi mawili na labda lingine likapita sasa inageuzwa anapata ushauri labda kwa akina mama wenzao ambao wanashindwa na nyumba zao. Wanapata ushauri na wanaangalia mwanaume peke yake kuonewa.

Pia kuwe na group ya kuangalia wanaume. Sio mama amevaa miniskirt, amekuonyesha mapaja umempatia haki yake, unaangaliwa kama mwanaume unalaumiwa. Pia kuwe na group ya kutetea wanaume. Na kama kunaingia group ya FIDA iambatane na mila zetu. Hata hiyo jana nafikiri ilikuwa katika Bunge.

**Laughter from the audience.**

**Com. Kabira:** Okay. Sijamaliza.

**Councillor Juma Sese:** Uliza niko tayari.

**Com. Wanjiku Kabira:** Na mwanaume akimkosea bibi, tufanye nini?

**Councillor Juma Sese:** Mwanaume vile sasa ndio umelileta vizuri. Kawaida katika mila tukiwa tunaoana ni family zinakutana zinaamua hawa watoto wetu waoane. Kama tukikoseana, ki-family mwanzo waanze kusahihisha na kuzungumza, shida yenyewe kukiwa haki imesimama, itapata ushauri kutoka pale kwa family. Lakini isiwe kwamba umegundua leo bibi yako hata ana mimba na labda sio yako, umeanza kumuadhibu sasa unaambiwa umepiga mwanamke akiwa mjamzito na wewe umejua hiyo mimba sio yako.

Ikiwa lakini imepangwa kwa family na wakazungumza na mtoto akatoka labda mimi niko mweupe kidogo na mtoto ametoka mweusi, inakuwa umekuwa katika haki, family mwanzo lishauriane kupeleka mtu kwa FIDA. Sio bibi ame-discipliniwa yeye mwenyewe ametulia halafu asubuhi unaona akina mama wawili watatu wa FIDA wanakuja na kibeti. Kwa sababu wanajua kufanya kazi wanapata commission mahali. Hiyo tutakuwa hatujengi.

**Com. Kabira:** Okay. Asante sana.

**Councillor Juma Sese:** Kuna lingine Commissioner naona unapenda kutetea haki za akina mama na mimi nataka za wanaume.

**Laughter from the audience.**

**Com. Kabira:** Hapana mimi najua akina mama wako hapa na watajitetea. Tutawapatia wakati. I wanted to recognize the presence of the Minister your MP Retired Major Marsden Madoka. Na tutamuuliza kama atawasalimia sasa au tuendelee kwanza.

**Honourable Marsden Madoka:** Endeleeni kwanza.

**Com. Kabira:** Okay. Thank you.

**Com. Keriako Tobiko:** Ngamarieni Mwangi.

**Ngamarieni Mwangi:** Commissioners hamjambo? Kwa majina ni Ngamarieni Mwangi. Nawakilisha sauti ya vijana wa(inaudible) sub-location. Lugha itakayotumika kuandika Katiba iwe ni Kiswahili ndipo iweleke kwa watu wote. Malipo ya (inaudible) kortini iondolewe. Kwani hiyo hufanya maskini azidi kuwa maskini na tajiri azidi kuwa tajiri. Serikali iwe inalinda watu wake kwa kulinda maisha na mali yao.

**Com. Keriako Tobiko:** Iko shida gani?

**Ngamarieni Mwangi:** Vituo vya matibabu viwe vikifanya kazi siku saba masaa ishirini na nne kwa wiki bila kujali holidays na iwe bila malipo. Mfanyikazi wa Serikali akifanya makosa akiwa kazini ashitakiwe kama mtu binafsi na asitetewe na wakili wa Serikali. Kwani hiyo inafanya wafanyikazi wafanye makosa makusudi. Wanyama wa pori wakisababisha madhara kwa binadamu au mimea wizara inayohusika ilipe fidia kwa wahusika. Walimu wa nursery walipwe na Serikali. Mwanafunzi akikosa ni lazima aadhibiwe na mwalimu kwani Biblia inasema 'spare the rod spoil the child'.

Barabara zote nchini zitengenezwe kwa usawa. Mkenya ana ruhusa ya kuishi popote Kenya lakini iwe mijini na sio mashambani kwani hiyo inachangia vita vya kikabila. Asilimia themanini ya uajiriwa itoke kwa wenyeji wa wilaya inayohusika ambapo labda kuna hiyo kampuni. Chief na naibu wake wawe wakipigiwa kura na wananchi na pia wawe na elimu ya kutosha. Na kura zipigwe baada ya miaka mitano.

Ikiwa mbunge au Councilor atapatikana na makosa wakati wa hatamu yake wananchi wawe na haki ya kuchagua mwingine.

PC atoke kwa mkoa, DC atoke kwa wilaya na DO atoke kwa tarafa zinazohusika. Na watakuwa wakichaguliwa kama wabunge. Tume ya kuajiri wafanyikazi wa Serikali ichaguliwe na wabunge. Mawaziri wachaguliwe na tume ya kuwaajiri wafanyikazi wa Serikali na sio Rais. Judge mkuu, police commissioner, Mkuu wa sheria na Jemedari mkuu wa majeshi wawe wakiajiriwa na Tume ya wafanyikazi wa Serikali wala sio Rais.

Rais asiwe mbunge na kama ni mzuri afanye kazi kwa vipindi viwili. Makamu wa Rais achaguliwe na Bunge pamoja na Speaker. Wakuu wa mashirika ya Serikali wachaguliwe na mawaziri wanaohusika. Ardhi ya national park ipunguzwe - naongea hapa kuhusu sehemu za Taita , ipunguzwe na kupewa wananchi wasio na ardhi. Consolidation Act iondolewe na badala yake ibaki Adjudication kwani hiyo huchangia vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Mashamba ni ya wananchi kwa hivyo hakuna Stateland Act - Mashamba yote ni ya wananchi. Rasilimali zote kama gemstones, parks, misitu na vinginevyo viwe vikifaidisha wananchi wa eneo hilo peke yake na sio watu kutoka wilaya zingine. Chairman wa County Council, Ma-mayors wa manisipaa wawe wakichaguliwa na wananchi baada ya kupigiwa kura.

Wafungwa wa makosa madogo madogo chini ya miaka miwili hivi wawe wakiruhusiwa wafanye kazi katika tarafa na location. Kila tarafa ijengwe---

**Com. Keriako Tobiko:** Na hilo liwe la mwisho. Liwe la mwisho hilo.

**Ngamarieni Mwangi:** Ngoja kidogo tu. Kila tarafa ijengewe na Serikali chuo cha watoto mayatima. Halafu ya mwisho, Kenya hii wanawake wasiwe wakivaa nguo ziwapasavyo wanaume kwani hiyo ndiyo huwa ina-encourage rape. Hata Biblia pia imesema mwanamke asivae nguo impasayo mwanaume.

**Com. Keriako Tobiko:** Sawa sawa. Asante. Jiandikishe hapo ndugu. Mwavasa Mwombo.

**Mwavasa Mwombo:** Waheshimiwa Ma-commissioner na wananchi wote kwa majina naitwa Philip Mwavasa Mwombo. Mimi ni mwenyekiti wa Ford Kenya katika Mwatate Constituency. Katika kuchangia mapendekezo ninawakilisha kijiji cha Kariobangi na Town, na tunasema hivi: Katiba iwe na utangulizi na uzalendo. Ya pili itoe uwezo na kanuni za kuweza kumfuta Rais akikiuka kama kufanya uhalifu fulani na kifungu nambari kumi na nne moja na mbili iondolewe ili aweze kushitakiwa mahakamani.

Tatu idumishe kikamilifu mila na desturi za makabila mbalimbali. Nne, iandikwe kwa lugha ya Kingereza na Kiswahili na baadaye itafsiriwe kwa lugha mbalimbali. Tano, iwe ikifundishwa shuleni na iwe rahisi kuipata kama kuuzwa katika maduka ya vitabu.

Namba mbili nazungumzia juu ya Rais. Rais achaguliwe kwa wingi wa kura apate asilimia hamsini na moja au zaidi na apate asilimia ishirini na tano katika ile mikoa mitano. Ya pili, Rais awe kati ya miaka arobaini na tano na sitini. Akifikisha sitini akae masaa.

**Laughter from the audience.**

Na anatumika hiyo miaka kumi peke yake, vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Ya nne, awe Rais wa nchi na isiwe ni kiongozi wa Serikali vile ilivyo sasa. Kwa sababu sasa huwezi kujua Rais Moi ni wakati gani anazungumza kama Rais, ni wakati gani anazungumza kama mbunge au ni wakati gani anazungumza kama mwenyekiti wa Kanu. Awe na kiwango cha elimu cha kidato cha nne na kwenda juu. Asiwe mbunge na asiwe mwenyekiti wa chama chochote. Hiyo ni kusema Katiba iruhusu independent candidates kusimama katika uchaguzi mkuu.

Wananchi wapewe uwezo wa kumfuta Rais kwa kupiga kura ya kutokuwa na imani na Rais. Vilevile hata mawaziri hata wabunge.

**Clapping from the audience.**

Makamu wa Rais ili awe na nguvu, asisukumwe sukumwe achaguliwe pamoja na Rais - awe running mate wake. Kwa hivyo atakuwa na nguvu hawezi kufutwa kwa Redio saa saba mchana. Kuwe na Waziri Mkuu ambaye ndiye atakuwa mkuu wa Serikali. Namba tatu, naingia Serikali. Kuwe na Waziri Mkuu ambaye atatoka katika chama kilichopata viti vingi zaidi bungeni. Kuwe na makamu wake ambaye atachaguliwa kutoka chama cha pili cha ukubwa ambaye kama sasa anaitwa 'Official leader of the opposition'. Yeye angekuwa makamu wa Waziri Mkuu.

Kuwe na mawaziri wasiozidi kumi na wanane na kila wizara iwe na Waziri mmoja na naibu mmoja na Permanent Secretary mmoja. Sio wizara moja ina mawaziri sita, huo ni uvunjaji wa pesa za umma. Tupunguze ghalama umaskini umezidi. Kuwe na Serikali ya mseto. Mkuu wa Sheria apendekezwe na chama cha wanasheria nchini na jina lake lipewe Waziri Mkuu na Waziri Mkuu vile vile apeleke kwa Bunge na aidhinishwe na Bunge. Sio kuwa appointed kwa sababu atafanya ile wakubwa wake wanataka.

Vile vile Makatibu wakuu hivyo hivyo waidhinishwe na bunge. Tunaipa Bunge mamlaka kamili. Utawala wa mikoa ufutiliwe mbali. Na badala yake kuchaguliwe wenyeviti kuanzia kwa vijiji hadi mahali kwingine. Kusiwe na DO, na DC, na Chief na nini, hiyo ni akili ya kikoloni ambayo wanatumiwa kutunyanyasa kwa sababu ni watu wa kusema 'yes sir'. Hawezi kusema 'no sir' - atafutwa kazi.

**Laughter from the audience.**

Vilevile kikosi cha Administration Police kivunjiliwe mbali na wote waende Kiganjo for retraining. Tusiwe na mamlaka ya polisi kawaida na polisi wa Administration - hawana kazi maalum akikushika bado atakupeleka kwa Police station ndio ushitakiwe.

Mahakama: Ili mahakama iweze kuwa huru, Judge mkuu ateuliwe au awe recommended na chama cha mawakili na achaguliwe na aidhinishwe na Bunge baada ya jina lake kupelekwa kwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu kupeleka kwa Rais ateuliwe na apewe tenure of office. Sio kufutwa ovyo ovyo. Vile vile kwa ma-judge na ma-judge wa rufani. Vile vile Mkuu wa sheria afutiliwe ule uwezo wake wa kuingilia kesi. Anaweza kuingiza moja aseme linaitwa 'nolle-prosequi" ambayo anaweza kuikatiza na mnyonge kuumia na kulinda hawa wengine.

Ardhi imezungumziwa zitazungumza juu ya hiyo nafikiri tumekubaliana na hayo mapendekezo. Lakini pia ningependa tueleze kwamba kuna ushahidi kwamba hizi shamba za mkonge za Mwatate, Taveta, Ziwani, Jipe zilitolewa pound millioni mbili na muingereza mwaka sitini na nne. Na hiyo pesa ilikuwa Wataita wakishalipa basi hii mashamba itakuwa ni ya Wataita. Na mpaka sasa hatujaelezwa na Serikali kikamilifu imekuwa vipi na mashamba ni ya akina nani na walipata kivipi na tungependa hiyo tufahamishwe.

**Clapping from the audience.**

Mapendekezo yetu kwa ardhi ni haya: Lease zote…….

**Com. Keriako Tobiko:** Na u-summarise ndugu yangu. Tutajisomea hiyo memorandum. Sawa sawa?

**Mwawasa Mwombo:** Asante sana. Hii imezungumza mambo ya lease na mambo ya mbuga ya wanyama wa porini, mambo ya madini imezungumzwa, mambo ya maji imezungumzwa. Bali tunasema kampuni yoyote ya madini au mtu binafsi akija kuchimba madini, iwe Katiba inaruhusu auze hamsini na moja kwa mia ya hisa zake kwa wenyeji.

**Clapping from the audience.**

Mahesabu ya madini yawe yakipelekwa kwa County Council ili kukagua na kuweza kuitoza ushuru kupunguza umaskini wa bwana chairman hapa. Maji ni mengi yametajwa, nitawaachia hapo. Mtasoma hiyo zaidi.

**Com. Keriako Tobiko:** Okay asante.

**Mwawasa Mwombo:** Kidogo tu. Mila na desturi hiyo imezungumziwa, hata ndio Madam alikuwa anauliza hapa Councillor juu ya mila na desturi zikizingatiwa na ziwekwe kwa Katiba ni kwamba mambo kadha wa kadha, pombe za kienyeji hiyo ni mila na

desturi kwa hivyo Katiba izingatie mila na desturi. Nadhani nitamaliza ingawa ni ndefu mtajisomea, lakini nitasema hivi: Ya kwamba polisi wapewe mshahara mzuri na nyumba nzuri. Pengine mambo ya "mlungula" utapungua. Na kikosi cha Administration nimesema ivunjwe na iwekwe kwa polisi. Asanteni sana.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe hapo. Davis Lemera.

**David Lemera:** Basi kwa majina ninaitwa David Lemera na haya ni maoni yangu ya kibinafsi. Kwa vile nina memorandum, nitataja tu kwa ufupi kwa sababu ya kuokoa wakati. Ningependelea vyama vya kisiasa viwe vitatu kwa sababu kwa wakati huu tuna zaidi ya vyama arobaini nchini Kenya ambazo zinaelekea ni za kikabila. Pili ningependelea kuwa tuwe na Serikali ya *majimbo*.

Tatu ni kwamba Mkenya yeyote asiwe juu ya sheria akiwemo President au Rais. Nne, President na msaidizi wake au Vice-President wachaguliwe na wananchi. Tano, tuwe na bunge mbili, Lower House na Upper House. Wengine wamezungumzia zaidi juu ya hiyo. Sita, Chiefs na Assistant Chiefs wawe-elected, wachaguliwe na wananchi badala ya kuwa appointed na Serikali. Saba, kuna kile kipengele ambacho tunakiita 'right of recall'. Wenzetu washatangulia kusema kwa mfano kama Councillor au Mbunge hafanyi kazi kulingana na vile anavyotazamiwa na wananchi, wananchi wapewe uwezo wa kumfuta ili wachague Councillor au Mbunge mwingine awawakilishe kwa huo wakati mwingine ambao umesalia.

Nane, kwamba wale wote ambao wanachaguliwa na Serikali wawe approved au wapitishwe na bunge. Na pia wawe professionals, - wawe wanazijua hizo kazi. Kwa mfano kama ni Waziri wa elimu, awe kwamba anajua mambo ya elimu kikamilifu au barabara. Sio kwamba awe mtu mwingine hajui mambo ya elimu vizuri halafu anaenda kuharibu hiyo wizara. Pamoja na wasaidizi wake kama PS, na Assistant ministers wachaguliwe kulingana na hiyo profession ya hiyo wizara. Halafu pia tuwe na ofisi ya huyu mtu anaitwa Ombudsman, sijui kwa Kiswahili anaitwaje. Huyu ni wa kuangalia checks and balances of the Government. Yaani katika idara zote za Serikali, awe akiangalia wakati mambo yanaendeshwa, aone kwamba mambo ya Serikali yanaendeshwa kisawasawa halafu baadaye ndiyo yule Auditor General aje kukagua mambo ya hesabu au mambo vile yanavyoendeshwa.

Halafu wale wote wanapigania viti vya kisiasa, wawe ni Ma-councillors, wawe ni Wabunge, wawe ni Rais, pia wa-declare their wealth. Watoe utajiri wao, waeleze waliupata vipi ili baadaye kama amekuja kuvunja mali ya umma ama mwenye kulipa kodi ijulikane na watu wajue vile watakavyo chukua hatua.

Na kumi na moja, ni kwamba hizi mbuga - hiyo ishatajwa ni kwamba, iwe chini ya miliki ya County Council, ili revenue kutoka kwa pengine watalii na mambo mengine, zile pesa ziingie kwa County Council halafu ndio baadaye Central Government ije kupewa percentage fulani ama asilimia fulani.

Halafu ingine ni kwamba, kuundwe kamati ya kusimamia welfare ama mambo ya wabunge pamoja na ma-councillors. Isiwe kwamba vile ilivyo sasa wabunge wakijiona kwamba hali zao za shida zimezidi wanaenda kujiongezea mishahara yao wenyewe. Lakini kuwe na kamati maalum ya kushughulikia mambo hayo ili pia na Councillors wasije wakaachwa nje. Sio vile tunaona Councillor ambaye ndio kama macho ya Mbunge lakini ukiangalia ule mshahara anapata halafu ukilinganisha na ule Mbunge anapata unaona hata it does not make sense. Kwa hivyo ningeomba hiyo iangaliwe pia. Halafu mwisho ni kwamba kura zote wakati wa uchaguzi zihesabiwe pale kituoni. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Bakari Mwanjoki.

**Bakari Mwanjoki:** Mimi najulikana kama Bakari Ngindu Mwanjoki. Maoni yangu ni kwamba kuwe Katiba hii ambayo tunaandikisha sasa, Serikali ijayo, Katiba yetu iseme ama napendekeza kwamba kuwe na majimbo. Sababu ya kusema hivyo ni kwamba jimbo la pwani limebaki nyuma kutoka mwaka wa sitini na tatu. Ukiangalia utaona pwani hakuna University lakini sehemu nyingine tunasikia kuna University. Mambo mengine yanaendeshwa hata ya barabara.

Na rasilimali nyingi zinatoka hapa ama ushuru mwingi unatoka hapa. Watoto wa sehemu ya wilaya ya Taita Taveta hawasomi sawa ikilinganishwa na wale wa kule juu. Hiyo ndiyo maana tunatetea majimbo kwanza hapa Pwani. Ama Kenya nzima pawe na majimbo nane - hiyo ndiyo Katiba. Tunataka rasilimali zote ambazo ziko katika Mkoa huu wa Pwani, zirejeshwe kwa sehemu ya Pwani.

Baraza la County Council linatakiwa kuchukua rasilimali ambazo ziko katika district ya Taita Taveta na ndio maana inaweza kujiendeleza na kutufanyia njia nzuri. Lakini kwa sasa, naona ajabu hata hii hii lami kwa hii barabara nimekuja nayo, baiskeli yangu ishapindika kwa sababu makorongo yamejaa hapo. Pesa hakuna, pesa zote zimepelekwa huko juu. Kupendekeza kwangu ni kwamba, sisi Wataita hatujaenda sana tunataka tuzae hapa tukutane na Kazigao ama tukutane na Ushambani.

Hizi mbuga za wanyama zipunguzwe na Katiba ijayo. Ili Mtaita azaane sio kurudishwa rudishwa ndani ya mawe ati 'waacheni hivyo hivyo, waacheni hivo hivo' kwa nini itakuwa hivo. Tunataka Katiba ijayo iwe Mtaita wanaenda hata wakikutana na wagiriama ni sawasawa kwa kuzaana ili tupate sehemu ya kulima mtu ajilimie chakula akipaka lori tatu, nne ndio kujiendeleza. Lakini wewe unalima chakula mwezi moja. Hiyo tunataka ipitwe na hii Serikali iliyopo. Tunataka Serikali ijao iwe imepunguza mbuga za wanyama kutoka sehemu ya Pwani.

**Com. Keriako Tobiko:** Endelea Mzee wangu.

**Bakari Mwanjoki:** Mengi yamezungumzwa kutoka madini kutoka rasilimali. Tunataka Custom, mimi nasema Custom iwe iko upande huu. Yaani hapo tutakuwa sehemu ya wilaya ya Taita Taveta imejiendeleza ikiwa Custom itakuwako. Asanteni sana.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mzee wangu. Jiandikishe hapo. Wacha tumsikize mama mmoja hapa sasa. Joyce Mwangoji.

**Joyce Mwangoji:** Asante Commissioners na viongozi. Yangu mengi yamezungumzwa na labda nitazungumza hasa yale yanayohusu akina mama. Ya kwanza ni kwamba Affirmative Action policy iwe adopted ili tupate akina mama wengi katika Parliament na Local Authorities na hata katika viwango vingine. Pia Constitution iangalie sana mambo ya gender equality.

Ikiwa kutakuwa na nominations za Members of Parliament ama katika Local Authority, basi hizo nominations, wanawake wawe nusu na wale ambao watakuwa nominated. Na nasema kwamba sheria pia ilinde watu iwapatie security kwa candidates wote wakati wa nominations, wakati wa campaign hata katika election period ili candidates wote wapate security ya kutosha.

Na tena napendekeza kwamba kuwe na electoral court ambayo ita-facilitate mambo ya kusikiza petitions za elections. Mayors na Council chairpersons na the deputies wachaguliwe na watu directly. Na nasema kwamba County councils wapewe uwezo zaidi ya shughuli za district. Na pia napendekeza kwamba President asiwe na constituency bali awe anaakilisha Kenya kwa ujumla. Na pia tunapendekeza kuwa President aongoze kwa kipindi cha miaka…awe na miaka mitano na kipindi cha miaka miwili I mean term mbili tu za miaka tano tano.

Tukiangalia upande wa uraia, tunasema kwamba mtu yeyote ambaye alizaliwa Kenya baada ya mwaka wa sitini na tatu na anaishi Kenya kwa miaka ambayo ni zaidi ya mitano, basi huyo apewe uraia. Tunasema pia mtu yeyote anayezaliwa na Mkenya nchini Kenya, nje ya Kenya, ikiwa ni mama ama ni baba huyo mtoto awe ni raia wa Kenya. Kwa sasa inabagua wanawake mama akizaa akija na mtoto hapewi uraia. Kwa hivyo tunasema kwamba akina mama akija na mtoto wake hata kama amezalia nje akiingia Kenya awe ni Mkenya.

Na tunasema pia mtu yeyote awe mama ama baba akiolewa au kuolewa na mtu ambaye si Mkenya, apatiwe uraia. Kwa sasa inabagua wanawake. Mwanamke akiolewa na mtu ambaye si wa Kenya kwa sasa- huyo mtu hapewi uraia. Ni mwanaume tu akioa mwanamke huyo mwanamke anapewa uraia. Tunataka hiyo ibadirishwe iwe kwamba wote wapewe uraia.

Pia akina mama singles, watoto wao wapate haki ya uraia kamili. Na kwamba katika passports tunaona akina mama wakiwa wanasafiri na watoto wao passports zao, jina la mtoto haliwezi kuingizwa kwa passport ya mama mpaka apewe kibali na bwana. Na hiyo imekuwa na shida nyingi. Tunataka akina mama wapewe uwezo wa kuweka majina ya watoto wao katika passport wasafiri bila shida yeyote.

Basic Rights: Tumesema kwamba tunataka Katiba izingatie basic rights ya kwamba tupate matibabu, maji, chakula, elimu na security. Na tena tunasema kwamba katika ngazi zozote za uamuzi kuwe na akina mama ili maamuzi yatakapofanyika kuwe

akina mama nao ni wengi. We should have 51% ili tuwe tunafanya uamuzi wa kutosha.

Pia tunasema akina mama wawe na haki ya kumiliki mashamba ama properties zozote zile. Na kwamba mama yeyote Mkenya asibaguliwe kwa kuwa ni mama na apewe heshima yake. Na pia tunasema Affiliation Act ile ambayo ilikuwa inaangalia watoto ambao wamezaliwa nje ya ndoa irudishwe katika Katiba. Iliondelewa mwaka wa sitini na saba na irudishwe iwe vile ilivyokuwako.

Katika vyama vya kisiasa nasema kwamba hivi vyama ikiwezekana vipatiwe pesa na Serikali lakini vipatiwe kulingana na wale members wao ambao wako katika Parliament. Na nasema parties sisiwe ni kama private party. Yaani isiwe ni ya mtu mmoja ama wale watu wenye uwezo sana. Ziwe ni parties ambazo zinazingatia masilahi ya watu wote.

Electoral system: Kura za Parliament na za Councillors ziwe kando na zile za President. Kura zihesabiwe mahali zimepigiwa - polling station, na matokeo yawe hapo hapo. Ballot boxes pia ziwe transparent kwa mtu yeyote aone. Siku hizi ni nyeusi na mtu hawezi kuona nini kiko ndani. Pia naomba kwamba kuwe na limit ya pesa ambazo zinatumiwa wakati wa campaign. Kwa kuwa hiyo itapunguza corruption na pia wale wanyonge pia wataweza kupigania. Electoral commission nayo iendelee kufundisha raia water education ili waelewe na hiyo ifanyike through political parties ama through NGO's. Na pia tunaomba akina mama kwamba the Constitution i-allow kwamba kuwe na mfuko fulani wa ku-support wanawake candidates and other marginalized persons ili wakati wa pigania Parliament na Civic elections wawe na nguvu za kupigania nafasi hizi.

Kwa upande wa mashamba na property tunasema mtoto mwanamke awe ameolewa ama hajaolewa awe na haki ya kuridhi kwa familia ya kwao mahali ametoka bila kubaguliwa. Kwa sasa tunaona watoto wa kike ndio wanabaguliwa na tunaona wengi ambao hawajabahatika kuolewa wakikaa nyumbani wakizaa watoto wanapata shida kwa kuwa hawana mahali pa kujenga ama pa kulima. Na pia tunasema wakati nafasi za mashamba zinapotokea kama hizi za settlement, wanawake pia wapewe nafasi ya kupata hizo shamba isiwe tu ni wanaume ambao wanapewa. Na tunasema kwamba Constitution iwe na uwezo zaidi………….

**Com. Keriako Tobiko:** Halafu mama u-summarise.

**Joyce Mwangoji:** Iwe na uwezo zaidi kuliko hizi mila zetu. Na nasema kwamba Stateland zote zipeanwe Local Community ama ziwe under Local Authority na National parks nasema ziangaliwe zirudi kwa Local Authority. Na nasema all leases ya Sisal Estate in Taita Taveta ziwe reverted to the locals. Na tena mbio, mbio napendekeza kwamba title deeds za family land ziwe na majina ya mama na baba. Na all public utility land ambazo zimechukuliwa zimenyakuliwa, zirudishwe ili zinufaishe wananchi kwa jumla. Na nikimalizia kwamba tuna marginalized and minority groups rights nasema kwamba kuwe na harsh sentences kwa watu ambao wamepatikana na hatia za ku-rape, defilement ama incest. Na tunasema minimum sentence iwe ten years na strokes ama life-imprisonment. Na ikiwezekana pia wawe castrated hawa wanaume.

Tunasema manyumba ambayo inajengwa na public transport na mambo mengine ya public yawe designed to cater for the needs of the disabled. Nasema kwamba customs na traditions that are harmful to women should be abolished. Kama F.G.M, wife inheritance na mengineyo. Na pia mambo ya domestic violence, tunasema hao ambao wanapiga wake zao watu hawa wapewe adhabu za kutosha. Na pia kuwe na special dock katika police station ya ku-deal na mambo kama hayo. Na pia kuwe na shelters for domestic violence victims.

**Com. Keriako Tobiko:** Mama tafadhali tutajisomea. Don't read it to us. We will read it ourselves.

**Joyce Mwangoji:** Asante sana. Mwisho nasema Katiba iwe rahisi kwa lugha rahisi na ifundishwe shuleni na vijijini. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Julius Mwangoo. Raymond Mwanzo. Milton Ngolo.

**Milton Ngolo:** Kwa Commissioners na wananchi wenzangu hamjambo? Mimi langu ni kuongeza tu kidogo kwa vile tunayo memorandum ambayo tumeandika lakini sasa nitaongeza kidogo kuhusu sheria ama mambo mengine ambayo yako ndani ya Katiba. Kitu ambacho ningeomba, ningeomba Katiba mpya sheria zitungwe na watu ambao wameelimika ama experts ambao watatengeneza sheria isiwe ati sheria imetengenezwa na watu wengine ambao itawafaa wenyewe bila watu wote kuwa wameakilishwa.

Tena kitu ya muhimu ambayo ningeomba, ningeomba hivi: Wazee wa kila kabila wahusishwe katika mijadala kidesturi na mila za kiafrika. Ili mila za kiafrika zilindwe, Afrika isije ikaharibika. Kwa sababu kitu ambacho nimeona, hata Katiba yenyewe ambayo ni ya Kenya, ambayo wananchi ndio wameishi nayo kwa miaka thelathini na tano, ni ajabu ya kwamba hiyo Katiba ilikuwa inafuatana mila na desturi za Kizungu. Lakini sasa kwa bahati nzuri wananchi sasa washagundua kwamba walikuwa wamepelekwa kwa meli ambayo ilikuwa haifai. Na hiyo ndio imefanya farakano nyingi zikawa katika Kenya. Watu hawapendani, wanakuwa ni kama nyang'au na majibwa wananyang'anyana mifupa huko misituni. Unakuta uchumi wenyewe umesahaulika, watu wanaangalia pesa peke yake, hawaangalii masilahi ya watu wenyewe ama kuangalia masilahi ya watu ambao wataishi kesho.

Watu wanaishi hawajui kwamba kesho kutwa watoto wataishi namna gani. Pesa zote za nchi zimenyakuliwa na zikafichwa. Sasa watu wanababaika ati uchumi umeharibika. Tunataka watu ambao wataandikwa katika kazi za Serikali wawe ni watu ambao watakuwa ni watu waaminifu. Tena wapewe discipline ya kutosha ili wasije wakaharibu Serikali. Ningeongea zaidi lakini kwa sababu nina memorandum nimeandika wacha niwasilishe.

**Com. Keriako Tobiko:** Okay, asante sana. Ignasi Mbele. Eric Maganga. Daudi Mwandawiro. Muhammed Ndambaso. Davidson Kasanu.

**Davidson Kasanu:** Asante sana bwana chairman. Yangu ni machache tu. Na kwanza ningalitaja moja moja na kueleza. Kuhusu pension ama malipo ya aina yeyote ile kwa watu wanaostaafu. Kuna ile inaitwa life gratuity na death gratuity. Hasa naongea kwa upande ule wa death gratuity. Unaona akina mama wengi wanateseka na hatimaye kuwa hawana matumaini ya kupata hayo malipo. Basi tungalipenda kusema ya kwamba malipo ya mtu aliyekufa ni vigumu kuyapata iangaliwe vizuri na hasa ikiwezekana yawekwe katika first priority badala ya kuwekwa pending.

Kwa upande wa pili naenda mambo ya elimu yaani education. Katika mambo ya elimu, hii 8-4-4 kusema ule ukweli ni maoni lakini sijui, huu mtindo wa elimu umeonekana kana kwamba umeleta shida nyingi hasa kwa wanafunzi ama shule na kuwa na syllabus nyingi hata ingawa zimejaribu kupunguzwa kupunguzwa. Lakini inaonekana kuwa ni matatizo ambazo zinaingiza kufanya wanafunzi kunywa madawa ya kulevya ati kwa kufikiria kwamba wanaweza kukabiliana na yale ma-syllabus. Lakini badala yake….

**Com. Keriako Tobiko:** Kwa hivyo pendekezo lako ni gani kwa hiyo?

**Davidson Kasalu:** Badala yake iwe pendekezo kama haingewezekana masomo kupunguzwa zaidi au hiyo 8-4-4 iweze kuondolewa na badala yake irudishwe mfumo uliokuwa zamani. Kwa upande wa tatu ni courts and laws. Courts and laws tumeona ya kwamba kwa hizi raping cases kwa akina mama zimezidi na utaona ya kwamba ni shida sana na kwa hivyo tungependelea iangaliwe maana imekuwa na vifungo tofauti tofauti. Unaona mwingine ameenda akahukumiwa mara kifungo cha mwaka mmoja, mwingine miaka miwili, sasa adhabu kamili haijatolewa na hasa inaleta matatanisho baina ya yule aliyetendewa ama kwa jamii kufikiria kwamba amekuwa under-rated kwa njia fulani ama nyingine. Kwa hivyo adhabu moja itolewe kwa kiwango kimoja.

Sasa naingia kwa upande wa commerce yaani biashara. Kwa kweli tangu Serikali ilipoondoa hii control price ya vitu, tumeona wafanyi biashara ndio wanaonufaika zaidi kwa mpango huu. Hali mwananchi wa kawaida anaendelea kuumia na vitu na kupandishwa huku ikidaiwa kwamba "hii ni transport, hii ni transport." Na hatujui mambo hayo ikiwa ni kweli. Kwa hivyo Serikali kuondoa ile control price imeleta mshikeni kwa wananchi wa kawaida. Kwa hivyo ningelipendelea hii control price iweze kurudishwa. Na hayo ndio niliokuwa nayo asante sana. Natoka katika Mwatate Constituency naitwa Davidson Kasalu katika Kishamba location.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante. Jiandikishe hapo nyuma. Jiandikishe hapo. Jared Mwagada. Fransisca Musua. Julius Gitonga. Hakuna. Magdalene Ngondo. Godwin Mwangoji. Sammy Kiwia. Dickson Babu had spoken? Dickson Babu. He is finished. Faith Mwadima.

**Faith Mwadima:** Wananchi wote nawasalimu hamjambo? Kwa majina mimi naitwa Faith Mwadima wa tarafa ya Mwatate.

Mimi yangu yale nilikuwa nataka kuzungumza yamezungumzwa kabisa lakini sisi watu wa Mwatate tuna shida na hospitali. Hospitali tunataka ziwe za bure, na shamba la mikonge lipunguzwe na pia za wanyama wa pori. Na kama chakula cha msaada kinaletwa kwa wale akina mama wasiojiweza halafu hawapatiwi, basi kisiletwe kabisa. Yangu ni hayo asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Okay asante sana. Benson. Jiandikishe pale. Benson Maganga. Joseph Mwakise.

**Joseph Mwakise:** Hamjambo nyote? Kulingana na Katiba iliyoko sasa nilikuwa nataka kuzungumzia juu ya marekebisho yenyewe. Marekebisho yenyewe ya Katiba ni kusema kwamba Katiba ya sasa, Serikali tunayoiomba itengenezwe sasa hivi ni ya majimbo. Kwa sababu Serikali iliyoko sasa imechukua mamlaka yote. Tulikuwa tunaomba Assistant Chief aondolewe kubaki chief. DO aondolewe kubaki na DC. Na DC awe anatoka humu humu.

Ya pili ni kuhusu mambo ya corruption. Pesa zote zimechukuliwa zimepelekwa nje, tulikuwa tunaomba kwamba Katiba ambayo inatengenezwa sasa, ikiwezekana wale watakaopatikana wamechukua hizo pesa wapelekwe mahakamani na wahukumiwe kwanzia kifungo cha miaka kumi kuendelea mbele. Halafu pesa zote zitakazopatikana huko zirudishwe nchini ili ziweze kusaidia uchumi ambao umezorota.

Ya tatu, tumesikia watu wengi wakilalamika kuhusu mambo ya watoto haramu. Watoto haramu wanatokana na njia moja. Kwa sababu utakuta mtoto wa kike amewekwa mimba na amemzaa mtoto nje. Yule mtoto kwa sababu mamake hawezi kumsaidia ingefaa mtu ambaye amemzaa yule mtoto, alazimishwe kulea yule mtoto mpaka afikishe umri wa miaka kumi na nane. Aweze pia kupatiwa nafasi ya kuridhi ile mali kwa yule bwana. Sio tu awe aking'ang'ania eti akae kwa wazazi wa bibi. Hicho ndicho kitu kinaleta kwamba lazima mtoto wa kike apatiwe shamba kwa wazazi wake - La. Mtoto ambaye amezaliwa apelekwe kwa baba yake na baba yake aweze kumlea na ampatie shamba yeye mwenyewe. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandijkishe ndugu yangu pale. Jiandikishe. Samwel Mwakungu. Leonard Mjomba. Emmanue Mwadoe. Emily Mwazinge. Clementina Asirena. Esther Mwombo. Mwachaje Kilelu. Esther Mwombo.

**Esther Mwombo**: Kwa majina ni Esther Mwombo, Chief Chavia Location. Nitatoa maoni yangu juu ya kazi nchini. Katika nchi hii ya Kenya ninapendekeza ikiwezekana wafanyikazi wale watakao ajiriwa na Serikali ama na kampuni yeyote ile wafanye kazi mpaka miaka arobaini na tano kisha wapishe vijana nao waendelee. Ninayo sababu. Ni kwa sababu mzazi atafanya kazi miaka sitini ama sabini huku watoto wake watano wana degree lakini wako nyumbani.

Kwa hivyo kazi ni miaka arobaini na tano ujiwekee akiba. Kwa sababu ya kufanya kazi miaka hamsini na tano wazee wanakaa kiholela na wale walioajiriwa hawajiwekei akiba haraka haraka. Wanafanya kazi wakijua niko bado na miaka kumi, miaka ishirini na huku vijana wanakaa nje. Kwa hivyo ninaomba miaka ya kufanya kazi ipunguzwe na vijana waweze kupata kazi wale ambao wako nje.

**Clapping from the audience.**

Ingine ni juu ya ardhi. Ninasema hivi: Ikiwezekana mali yote ya asili irudishwe kwa wilaya na wilaya isimamie na ilinde na ijue itatumika kivipi ili kufaidi mahali pale pale inapotoka. Na ikiwezekana basi kama Serikali itataka kitu kidogo, - sio ni kitu kidogo lakini rasilimali karibu ya 70 ibaki kwa wilaya.

**Clapping from the audience.**

Na nitatoa ombi lingine kwa watoto yatima. Watoto ambao ni yatima wanawapatia guardians ama walezi ngumu kwa sababu utakuta guardian, walezi kazi ngumu. Kwa sababu guardian ana watoto kumi, bado wengine wamefiliwa na baba zao na mama zao watano. Yule guardian ambaye ni relative anachukua jukumu kubwa ya kulea watoto ishirini ama kumi na nane. Ikiwezekana watoto wote yatima katika Serikali yetu ya Kenya waandikishwe kwanzia wilaya hata sub-location ili wapatiwe elimu ya bure. Na kama haitawezekana katika shule zote za kawaida, basi wajengewe shule zao zile ambazo zitahudumiwa na Serikali na kila elimu ya hali ya juu wapatiwe hapo. Kwanzia kiwango cha chini mpaka cha juu.

Na ikiwezekana pia kuna hao wazazi ambao hawajiwezi. Hao wazazi pia ambao hawajiwezi waandikishwe kuanzia viwango vya chini na wale watoto wapatiwe elimu za bure. Tunao watoto bright lakini tunawapoteza kwa sababu wazazi wao hawawezi kuwasomesha. Ninaomba elimu ya bure kwa wasiojiweza. Na nitataka nizungumzie juu ya matibabu. Matibabu yamekuwa ya hali ya juu, unakuta mtu ambaye hajiwezi anatakikana afanyiwe matibabu ya elfu mia. Elfu mia. Na hata maishani mwake hajapata kushika elfu moja, elfu mia atatoa wapi? Basi matibabu pia yaangaliwe yawe ya bure.

Nitataka nitoe habari yangu juu ya ujira. Kunao ujira wa hali ya juu sana ambako watu wanapata pengine elfu sabwini, elfu mia moja na hamsini na hapa kuna wengine wanapata elfu moja, elfu mbili, elfu tatu na wote wanafanya kazi katika Serikali. Hayo mambo ya ujira ambayo elfu sabini zinaweza kugawanywa zikaletewa watu wengine watano, ikiwezekana lipunguzwe kwa sababu sukari ni kilo moja shilingi hamsini kwa tajiri na hata kwa maskini. Je maskini hana haki ya kula? Je ya kuishi hana haki? Tafadhali Serikali yetu ya Kenya isifanye maskini akufe na tajiri aishi maradufu. Kila mtu ana haki ya kuishi.

Mwisho kabisa nitajitetea. Mimi kama Chief na mfanyikazi wa Serikali, nashangaa sana wananchi wakisema ati tuchaguliwe kwa kura. Nikichaguliwa kwa kura sitafanya kazi vile inavyotakikana maanake kila wakati nitakuwa nalinda kiti changu. Nikiwaambia huyu ana makosa na alikuwa campaigner wangu je hiyo kazi nitapata wakati mwingine? Kwa hivyo hiyo ingelikuwa sisi tuwe appointed kwa interview, kwa mtihani, kwa qualifications na criteria ili niweze kuifanya kazi sawasawa. Kweli ni kweli la uwongo ni la uwongo.

Makosa ni makosa nisiyapake rangi ya green. Maanake ninaweza kuchukua rangi ya green nikapaka makosa ili nibaki kwa kiti.

Ninalinda unga. Kwa hivyo haya mambo ya Provincial Adminstration, sikubaliani. Na kama wananchi mngelijua kweli vile mnavyofanywa - fanywa hivi na wale mnawachagua, mnakuwa patted at the back, hamngesema tuchaguliwe. Kazi itakuwa ngumu. Asanteni sana.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe. Chief jiandikishe. Kilelu.

**Mwachaje Kilelu:** Asante sana ndugu Commissioner na wananchi. Mapendekezo kwa ufupi ni kama ifuatavyo maanake najua wakati hatuko nao na watu ni wengi. Kwanza Katiba ningependa kulingana na maoni yangu, ningeonelea Katiba inafaa ikae na Kitangulizi, - It is important to have a preamble in the Constitution. Mamlaka yote ya nchi na Serikali yakae chini ya wananchi, - All state power should emanate from the people. That should be there in the preamble.

Halafu kuna jambo la Serikali itakuwa kazi yake ni gani? Kikatiba, Serikali inatakiwa ikae na wajibu mmoja tu, - kuendeleza maisha ya mwananchi peke yake. Na Serikali ikishindwa kutekeleza wajibu huo ifanywe nini? Kukawa na wananchi wana ruhusa ya kuwa na kura ya maoni kuondoa hiyo Serikali. Na watu wote licha ya kujali tabaka, rangi wala kabila wawe sawa mbele ya macho ya sheria, - all people should be equal before the law.

Haki za binadamu ni lazima zizingatiwe na kuimarishwa kabisa katika Katiba. Kwa mfano watoto Katiba iweze kutafsiri rika la mtoto, mtu yeyote chini ya miaka kumi na sita, atafsiriwe kama mtoto. Na mtoto akae na haki ya chakula, elimu na afya. Vijana wakae na haki ya uhuru wa elimu, wakae na haki ya kupata kitambulisho, kupata passport na kupata kadi ya uandikishaji wa kupiga kura. Na pia vijana waweze kupewa nafasi ya muhimu katika kuakilishwa bungeni. Tunaweza kutoa mfano kama Uganda, we have a special youth representation in Parliament and even in the Local Authorities, - that should also be instituted in the Kenyan Constitution.

Wale watu ambao ni walemavu, naona kwamba Katiba ingetakiwa iangalie kama wataalamu akina Keriako, wataangalia lugha gani ya kisheria itafaa. Walemavu wajulikane kama ni transport accessibility, communication, mambo ya afya, mambo ya uandikishaji kazi, mambo ya elimu. Na pia walemavu wakae na nafasi zao wametengewa kama sehemu maalum ya kuakilishwa Bungeni as a special sector.

Halafu akina mama pia nina pendekezo la kwamba akina mama musikae na lile "mama." - Let there be no lamentation. Akina mama kisheria waangaliwe sawa kama wanaume. Let us not use a lot of words – "gender" and so many words. Wawe sawa na wanaume. Isipokuwa kwa hali ya sasa kwamba akina mama wamelemewa na wamebaki nyuma kwa sababu tunazijua ni nyingi hatuwezi kumaliza kwa leo, wapewe nafasi at least - special also affirmative action iangaliwe.

Then kwa upande wa utawala. Nafikiri watu wengi sana tumesema majimbo, majimbo, lile jimbo ambalo mimi ningelionelea linafaa sana ni jimbo …..let us establish counties. Kukae na jimbo la wilaya. Na hilo jimbo la wilaya likae kwamba ukitoka

Central Government from Statehouse, usiingie Harambee house, the second institution of power ikae ni County council. Halafu iwe mali yote, ardhi yote ambayo iko chini ya ile area ikae under Local Authority. Na mambo ya ardhi, there should be a Land Commissioner who is from the district. Halafu wale viongozi - Civic leaders wakae kwamba wana bunge lao. Like in the County Council where we have all Councilors let us have a district assembly.

District chairman wa county council tubadirishe jina lake akae ni district governor. Na kukae na bunge mbili the current House of Representatives and the Senate. Kila District Governor akae ni member wa Senate na wakae wanakutana kama mara mbili kwa mwezi Nairobi.

Halafu yale mapato yote yanayopatikana katika kila wilaya, yakae kabla hayajaenda kwa hazina kuu ya Serikali yakae yanapitia hazina kuu ya wilaya. All revenue collected within the district.

Then Provincial Administration with due respect to Madam Chief vile alivyosema kwamba Provincial Administration isikae inachaguliwa, I also agree with her. Isikuwe inachaguliwa. Isipokuwa mamlaka, the office of the chief should be the office of the Council only that the Chief should be the Administrative Assistant of the Council.

The DO should be the Administrative Assistant of the Member Parliament and the office of the DO should be the office of the Member of Parliament. When Madoka is elected you don't have to bother him to hire an office. Let there be an office for him to serve. Halafu tunatakiwa kama kwa mfano District Commissioner, ile office isikae ni ya District Commissioner tena ikae ni ya District Governor anayechaguliwa na wananchi. Huyo Governor ndiye anachukua nafasi ya District Chairman. Yule District Commissioner anakuwa ni kama Administrative Assistant to the Governor.

Then, kwa upande wa elimu, kwa sababu ya mambo mengi uzalendo haujui elimu. Kuna watu ambao hawajaenda hata nursery lakini ni watu ambao wanapenda nchi, wanapenda maendeleo na ni watu wazuri sana. Lakini kwa sababu ya wakati, ukora umekuwa mwingi. Mataberi wamekuwa wengi, mawakili wengi are not truthful. Ukijua Chairman ama District Governor si mzuri, ukijua kuna diamond ya Taita, you will come and fradulently acquire some land in Taita.

Kwa hivyo kwa sababu vile maisha yamekaa District Commissioner pamoja na Councillor na Mbunge na Rais wote wakae ni watu wamefikia at least minimum O' level. Tusiseme Rais akae na degree. Hata Uingereza ilianza kuwa na madegree kutoka miaka mia tatu iliyopita and John Major was just a Prime Minister the other day is an O' level. So we cannot peg a University degree for leadership. Let it be just O'level as the minimum standard of education.

Kwa kumalizia malizia, ningependelea pia kukae na calendar ya elections. Isikae kwamba uchaguzi mimi nikiwa kama President nikae natumia nchi vile ninavyotaka. In future, hundred years from now, hatutakuwa hai lakini tungependa uchaguzi ukae wale watakao kuwa wakati huo wanajua uchaguzi ni baada ya miaka fulani na Tume ya uchaguzi ikae huru, kujiandikisha kwa kura

kuwe kunafanywa mara kwa mara, halafu kukawa na haki ya wananchi, kukawa na kura ya maoni – a provision for referendum should be there.

Rais achaguliwe directly na wananchi kwa mihula miwili peke yake. Only two terms and a term should be five years. Then Rais asikae kwamba anasimamia vyama vya kisiasa. The President should be above party politics.

Serikali iwe inaongozwa na Prime Minister kupitia Bunge. Na katika uchaguzi wa Urais, Rais mpaka apate 50% of the votes in addition na 25% katika mikao mitano. Kama sio hivyo, kunakuwa na run off between nambari moja na nambari mbili. Halafu Prime Minister awe anashirikiana na kamati za bunge mara kwa mara wakati wanapoendeleza Serikali.

Halafu mambo mengi yamesemwa hapa ya mishahara, ya maendeleo, we cannot contaminate the Constitution with everything. Lakini it is my proposal that: Kwa nchi kuendelea, kuna tume kadhaa ningependelea zikawekwe, zikawa zinatambulika kikatiba. Na hizi tume, - these commissions should be recognized by the Constitution and even bright lawyers like Tobiko should put the right language to get these commissions.

1. Electoral Commission: Tume ya Uchaguzi, tena itambulike Kikatiba.
2. Parliamentary Service Commission: Tume ya Huduma Katika Bunge iwe inatambulika Kikatiba.
3. Local Government Commission: Maanake we are talking of devolution na tunataka Serikali za mitaa ndio ziwe na mamlaka, tukawe na tume ya Serikali za mitaa.
4. Kukawe na Police Commission.
5. Kukawe na pia Armed Forces Commission.
6. Kukawe na pia Public Service Commission.
7. Kukawe na Judicial Service Commission. Prisons Commission.
8. Na kukawe na the Office of the Government Inspector together with Anti-corruption authority clauses. Hiyo tutaona kama Auditor and Controller-General ataingia hapo ndani. Kusudi nini? Malalamishi yote ya mwananchi kuhusu Serikali yawekwe hapo ndani. Asanteni sana na Mungu awabariki.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo ndugu yangu.

**Com. Kabira:** Sorry tutamuuliza Emmanuel Nzungu ako? Hayuko. Joseph Obondo. Joseph ako? Na mheshimiwa utatwambia wakati ule unataka kuzungumza. Okay.

**Joseph Obondo:** Asante kwa kunipa hii nafasi kuzungumza kuhusiana na maoni ya Katiba. Hii Katiba sisi tunafurahi sana Wakenya, nafikiri ninafurahi; Hii Katiba ilikuwa inasumbua Wakenya. Na hii Katiba kwangu mimi naunga mkono kufanywe Katiba ile ya kuunga Wakenya wote. Wakenya wawe huru bila kubagua ati huyu ni fulani huyu ni fulani. Tujenge Kenya yote,

kuinua Kenya yote kila pahali. Hiyo ndio mimi naunga mkono kuongezea tu. Hivyo ndivyo mimi naona.

**Com. Kabira:** Asante sana Mzee Obondo. Na tutamuliza Ronald Taabu. Amemaliza? Ako nje? Anakuja? Okey. Karibu Ronald.

**Ronald Taabu:** Asante sana kwa nafasi hii ambayo nimepewa. Nilikuwa nakimbia nimesikia kiu lakini nimekabwa vile. Ningejaribu kusema tu kwa kifupi, mimi nilikuwa napendekeza tuwe na nchi au Serikali ya Kenya ambayo haitakuwa na vyama vya kisiasa – "A no party State."

**Com. Kabira:** Tafadhali tumia microphone kwa sababu tuna-record.

**Ronald Taabu:** Okay. Basi ndio nilikuwa nasema ya kwamba tuwe na nchi ambayo haitakuwa na vyama vya kisiasa. Tuwe na "no party State." Hivi vyama vya kisiasa mara kwa mara ndivyo zimechangia kuleta ukabila sana katika nchi. Halafu tuwe na Rais ambaye atakuwa amechaguliwa na wananchi wote, na asiwe ni Mbunge. Awe ni kati ya umri wa miaka arobaini hadi akiwa mzee sana miaka sitini na tano. Serikali yenyewe iwe na Waziri Mkuu kwa sababu hapo juu nimesema haitakuwa na vyama vya kisiasa, Waziri Mkuu atakuwa akichaguliwa na wabunge wale ambao wamechaguliwa. Na ndiye atakuwa kiongozi wa Serikali. Kusiwe na wizara nyingi zikiwa nyingi kabisa ziwe kumi na saba.

Na muundo wa utawala, nilikuwa napendekeza kwamba utawala wa mikoa uondolewe mbali. Maanake wakati tunaposema chain of command, ikitoka huko juu mpaka kufikia kwa sub-chief ni kama mtu kujijenga kama kifalme, - inapitia katika hiyo chain of command, Halafu mpangilio huu wa utawala vile utakavyokuwa ni kama ifuatavyo:

Tukishatoka katika national level, hatutakuwa na ofisi ya mkoa. Tutakwenda moja kwa moja mpaka katika ofisi ya wilaya ambapo tutakuwa na mkuu wa wilaya wa kuchaguliwa kutokana na mahali anapotoka. Yaani tuseme kama ni Mtaita atakayekuwa kwa ofisi ya wilaya lazima atoke hapa Taita. Tukitoka katika ofisi ya wilaya, tunaenda ofisi ya Chief.

Hatutakuwa na ofisi ya DO. Ofisi ya Chief naye atakuwa akiitwa kama Mkuu wa tarafa ama wa location. Naye achaguliwe kwa kura. Ijapokuwa dada mmoja hapa amesema ya kwamba si vizuri kufanya hivyo lakini najua kwa sababu kutakuwa na sheria za kuongoza watu, huyo atakayechaguliwa ni lazima azingatie hizo sheria. Na asiwe chini ya miaka thelathini na tano na zaidi na vile wakati wa kumchagua ni ya kwamba wataandika applications zao na qualifications zao za elimu na sifa ndio waende kufanyiwa uchaguzi.

Na vile vile tuwe na uwezo raia wa kuweza kumtoa Chief, Assistant chief au Mbunge ama Councillor kama hatakuwa na nidhamu ama atakuwa amekuwa na utawala usiopendeza. Wananchi wawe na uwezo wa kumtoa hata kama muhula wake

haujaisha. Na kesi za mashamba ni mambo ambayo kidogo inatatiza wale ambao wana unyonge wa pesa.

Nasema ya kwamba tukirudisha utawala kwa hawa ambao tunasema kwa wazee wa nchi ama kwa wananchi, katika mahakama tuwe na watu wazee wa busara kuchaguliwa kuangalia mambo ya mashamba hapo hapo ndani. Kwa sababu kila jamii ina mila zake mbalimbali. Sasa sheria za kuandikwa zinazotumika sehemu za Ujaluoni, kwa Wakikuyu, kwa Wakamba si sawa na za Wataita. Kwa hivyo tuwe na wazee wanaolewa na wawe wakichaguliwa kutoka vijiji vijiji wa kuendesha hizo kesi za mashamba na kulingana na vile desturi na mila za hao watu ziko.

Jambo lingine ambalo naendelea kumaliza maliza ni katika kesi hizi za kuweka mimba. Zamani msichana akiwekwa mimba kuna wazee walikuwa wakishughulikia mambo hayo. Na zikirudishwa ni vizuri kwa sababu kila kesi iangaliwe kulingana na mambo yake. Ijapokuwa watu wanasema eti ni lazima msichana akiwekwa mimba mtoto alewe hatujui amepata mtoto kwa njia gani. Pengine alikuwa anafanya labda ni biashara mambo yakampata vibaya. Kwa hivyo naomba hali hiyo iwekewe wazee ambao watajua kuamua kulingana na hali ilivyo.

Halafu nikiingia katika umilikaji wa ardhi, kila wilaya inayo mila na desturi za umilikaji wa ardhi zake. Kwa hivyo kama ardhi ni ya Wataita, tusiambiwe kuna Stateland, kuna sijui nchi ya nani, lakini zote. Sehemu yeyote ya ardhi iliyoko Taita ni nchi ya Wataita. Kwa hivyo Wataita wawe na uwezo wa kuweza kuamua wataifanyia nini. Kama hizi national parks Wataita wakitaka kuzipunguza wawe na uwezo wa kuipunguza. Halafu kama tukipitia katika hii rasilimali, kila rasilimali ya nchi hii ambayo inaangukia katika mikono ya wilaya, asilimia sabini kwa mia, iwe ni mali itakayobaki katika hiyo wilaya. Na thelathini kwa mia ziende katika Central Government.

Na labda ninamalizia nikisema ya kwamba, askari tawala nilikuwa ninapendekeza ya kwamba hawa askari tawala ambao tunaita AP's wawe wakiwa chini ya Mkuu wa wilaya katika ngazi ya wilaya na katika location wawe chini ya Mkuu wa tarafa ama location. Na nilikuwa nimependekeza kwamba muda wa hawa watawala kuwa katika uongozi uwe miaka sita. Maanake mwaka mmoja kila mara huwa unaharibiwa katika mambo ya kufanya ma-campaign. Lakini miaka tano iwe ni ya kufanya kazi. Jambo la mwisho labda nikimalizia ni ya kwamba nilikuwa nimetaja ya kwamba kodi za mashamba na viwanda, kodi zozote zinazotokana na mashamba na viwanda vilivyoko katika wilaya, kodi zote ziende kwa mfuko wa wilaya. Kwa hayo machache Mungu awabariki.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Ronald, na Helen Salim ako? Hayuko. Sorry, sisikii. Jina lako. Why don't you get the names then you can check? You get his name then you can check how far he is. Nimekuita? Lile jina nilimuita Helen Salim. Na tukaona hayuko. Huyo alizungumza ni Ronald. Lakini nipatie jina lako nitaangalia. Umpatie jina nitaangalia. Thomas Tole ako? Hayuko. Preston Mwambela. Hayuko. Cornelius Muchalo. Hayuko. Christine Mwamudava. Amepeana? Mwakio Mwani. Walter Mwabogo. Ni wewe?

**Walter Mwabogo:** Mimi sina mengi sana. Katika hayo yaliyozungumzwa karibu yale nilikuwa nayo imekwisha semwa. Isipokuwa kidogo sikusikia mambo ya kuhusiana na hospitali. Hospitali watu wanaumia na magonjwa kwa sababu ya pesa. Maana ukiwa huna pesa utakaa na ugonjwa wako hivo hivo.

La pili, ni mortuary. Mtu wako amekufa, bila kupeleka pesa ataoza pale. Hilo ndilo nasema ni lingine ambalo halipendezi. Sasa kama sina pesa mtu wangu ataozea pale ama atazikwa na watu wengine hivi hivi. Hilo nasema liondolewe ikiwezekana. Sina mengi zaidi isipokuwa haya mawili tu.

**Com. Kabira:** Asante sana. Andika jina lako tafadhali. Boniface Mwamburi.

**Boniface Mwamburi:** Asante sana Commissioners wetu na wananchi wangu. Mimi nina machache kidogo ya kuongea. Jambo la kwanza ni Katiba yetu iwe na utangulizi na utangulizi wenyewe uonyeshe wazi kwamba Kenya ni nchi ya makabila mbalimbali na wanahitaji ama wako na different cultural beliefs. Hizo tamaduni zao ziwekwe katika hali ya kwamba hakuna mwananchi yeyote atakaye jisikia kwamba tamaduni zake zimekwepwa ama zimeenda zikawa zinalaliwa.

Jambo la pili katika huo huo utangulizi, uonyeshe kabisa kwamba kuwe na elimu ya bure, mambo ya afya yawe ya bure na mambo ya usalama hivyo hivyo yawe ni ya bure. Tuna uraia, uraia uwe ni jambo moja la kuangaliwa kwa dhati, hivyo basi kama kuna Mkenya yeyote ambaye amezaliwa Kenya, apewe uraia. Na kama kuna Mkenya yeyote amezaliwa nchi ya nje, pia huyo anastahili kupewa uraia. Lakini kama anataka kuwa na uraia mbili isikubaliwe kabisa. Asiwe Mjerumani halafu tena awe Mkenya kwa maana utakuta kuna mtu mwingine anaweza kuwa na uraia wa Italy, Ujerumani, na pia tena amepewa uraia wa Kenya. Sasa mtu kama huyo wakati mwingi kama kuna uvunjaji wa pesa anazivunja na kuzipeleka huko kwa haraka na anakimbilia upande ule mwingine wakati tumeachwa hapa katika hali ya janga.

Muundo na aina za Serikali: Kenya hii tunahitaji kuwa na muundo msingi wa Serikali yetu. Serikali yetu iwe na Rais na Rais asiwe anazingatia mambo ya chama. Hivyo basi Rais atakuwa anaangalia masilahi ya Wakenya wote bila kujali chama kipi ambacho kiko kwa uongozi. Na hawa Ministers wasiwe Wabunge, kama mtu anataka Ubunge asiende akapewa nyadhifa nyingine kama ya u-minister. Ministers wetu watolewe na nina amini hata sasa huwa wanachukua mawazo kutoka Permanent Secretaries ndio wazipeleke pale bungeni. Na wakati mwingi tunakuta kwamba hupotoshwa ama huwa hajabeba yale mambo ya kutosha pale Bungeni kwa sababu amepotoshwa na yule Permanent Secretary.

Hivyo basi kama kuna Permanent Secretary, achukue ule wadhifa maanake huyo ndiye atakuwa kama mkuu wa ile ministry na Minister asiwe Mbunge. Pia tuwe na Waziri Mkuu ambaye anatoka katika chama kile ambacho kimemsajili ndio aende tengeneza Serikali. Kama yeye ndiye yuko na majority votes katika bunge yeye ndiye ataweza kutengeneza Serikali ambayo itaweza kukizi mahitaji ya Wakenya wote.

Bunge lenyewe liwe na mambo mawili. Tuwe na Upper House na Lower House. Na hii Lower House tuwe tunawakilishwa kutoka district level ambao ni wale Ma-senator wetu ambao tutakuwa tumewachagua ama Ma-chairmen kutoka districts ili kuangalia ule mgawo wa rasilimali zile zinazokuja ama kile kikapu cha rasilimali vile kimekuja, kitufikie sisi wananchi katika district level.

Mahakama iwe ni huru na kuwa huru mahakama hiyo inapata usajili kutoka kwa Bunge baada ya majina ya lawyers yamependekezwa. Majina hayo yawe yamependekezwa kwa Waziri Mkuu ambaye ndiye atakuwa Mkuu wa Serikali ambaye ametengeneza Serikali na ayawasilishe kwa Bunge ili apate kusajiliwa na kupewa haki ya kuweza kufanya kazi.

Haki za kimsingi: Haki za kimsingi ni lazima tuangalie kwamba sisi tumepata haki zote. Tuna maji ambayo tunayajua ni haki yetu, lazima tupate, elimu ya kutosha ya bure kwa kila mtoto ambaye amezaliwa Kenya, pia kuwe na haki ya kumiliki shamba kwa kila mtu yeyote ambaye ameitwa ni raia wa Kenya - asikose chini ya acre kumi ya shamba - ni lazima apewe maanake Mkenya hawezi kuitwa squatter kwa vyovyote vile.

Haki ya ardhi na mali: Haki yetu ya ardhi na mali zetu ni lazima zilindwe katika Katiba hii. Kwa mfano vile tuko na migodi hapa ile migodi ni lazima tuone kwamba katika Katiba yetu tutengeneze “common market.” Badala ya mtu kutoka nje let’s say kutoka Nairobi aje achimbe madini, madini hayo yachimbwe hapa hata kama amepewa mamlaka ya kuchimba na ayauzie hapa hapa. Tukiwa tunajua kama rumbi ni shilingi elfu sita gram moja, basi iuziwe hapa Mwatate, tukisha ni elfu sita, aache fidia kidogo kwa County Council yetu na pia sisi wenyewe tutakuwa tumepata kujua kwamba kwa ile mali tumepata kitu kidogo.

Kuna hii private property, - si sawa kuwa na lease ya ninety-nine years kwa mtu mmoja ambaye alipewa enzi za ukoloni. Tukiangalia sana kama kwa mfano yule ambaye amemiliki Sisal Estate hapa hata saa hii ni mtu ambaye alipewa kabla hatujazaliwa - enzi za ukoloni. Zile treaties zote ambazo zilifanywa pre-independence ziwe revoked - they should be declared null and void. Kama wakati wa ukoloni tulikoloniwa na tukasema sisi tunaenda kupigania haki zetu, leo hii mkoloni huyo huyo tuko naye bado na anazidi kutunyanyasa na tunajikuta kwamba ile mali hatujapata na ukoloni bado unaendelea sasa unaitwa ukoloni mamboleo. Kwa hivyo katika hali yeyote ni lazima zile haki zetu, - na haki zetu ni mali kama hii sisal estate, ziwe ni za wananchi. Kama mkonge hautupi faida basi uondolewe tulime ili na sisi tupate.

**Clapping from the audience.**

Lakini kama unatupatia faida isiende pale Central Government bila Mtaita kufaidi chochote - apeleke 25% kwa Central Government na 75% ibaki hapa Taita tupate kukizi mahitaji ya County Council yetu. Electoral Commission: Katika hali ya kuwa na uchaguzi huru na wa haki, nilikuwa napendelea kwamba mahali popote kura zinapopigiwa, lihesabiwe hapo hapo, na kura zote ziwe ni za siri – zisiwe za mlolongo na baada ya hizo kura kupigwa pale zihesabiwe pale ijulikane mshindi ni nani na

mshindwa ni nani. Badala ya kubeba yale maboksi kutoka kituo hiki mpaka kituo kingine. Na maboksi hayo yatengenezwe kiasi cha kwamba ukiweka kura yako unajua boksi hili ndilo na kura zitakuwa zinaonekana ni ngapi zimeingia kule. Kwa hivyo kwa hayo nafikiri Katiba yetu ambayo inaenda kutengenezwa itakizi mahitaji yetu. Asante Commissioner.

**Com. Kabira:** Asante sana Boniface. Kioo Mwani. Amekuja? Hajakuja. Briton Kiriga. Hayuko. Joseph Mwangeka. Hayuko. Getrude Mugoi. (Hayuko). Hannah Kariuki. (Hayuko). Bildad Mugendi. (Hayuko). Beatrice Mwakunona. (Hayuko). Agnes Shayo. Agnes, she was representing a group. Hajaingia? Au ametoka? Lucas Mwanjama. Lucas Mwanjama hayuko. Hebel Mwakio. Can't read the name but it is Mwakamba. M. Mwakamba. Hayuko. Lillian Nzano. Alitoa? Ni sawa tu anataka kurudi.

**Lillian Nzano:** Kwa majina yangu ni kama vile mmesikia, naitwa Lillian Nzano na natoka hapa Mwatate kijiji ambacho kinaitwa Zingila. Nashukuru kwa nafasi hii ambayo kwa Kenya yetu imetoa kwa raia wa nchi ya Kenya asikie ya kwamba yuko huru na anaweza kutoa maoni yake. Sina mengi sana kwa sababu mengi nafikiri yametangulizwa na nimesikia kwa wenzangu, isipokuwa naweza kuongezea au kuchangia kwamba wakati viongozi wanapochaguliwa, achaguliwe kiongozi ambaye anaelewa na shida za mwananchi wa kawaida. Nikizungumza namna hiyo ni kwamba tunaona tunapochagua viongozi ni kuwa watusisimamie mambo yetu huko mbele. Lakini utakuta wakati mwingine tukileta mambo yetu kuwa, haya maneno hayaendi sawa sawa kwa sababu yule mtu hajui shida. Tunapoleta shida zetu tunataka mtu ambaye anamjua mwananchi wa kawaida. Kwa mfano mmoja wetu ametoa hoja ya jaa – kwa hivyo ni kweli niende nyumbani kwake nione analala vipi na watoto wake wanasoma vipi – huyo ndiye kiongozi wa sawasawa na akienda mbele atatoa hoja ya kweli.

Kwa sababu kuna viongozi wengine wanasema watu wake hawana shida. Tena unasikia watu sehemu hiyo wanakufa kwa njaa. Kwa hivyo jambo hilo natoa hoja ya kwamba kiongozi anapochaguliwa kweli ajulikane ni kiongozi wa matendo si kiongozi ambaye ni wa kuonekana pengine kwa gari hajui shida ile iko katikati ya wananchi.

Jambo la pili ningeweza kuongezea ni kwamba katika elimu tumeona watoto ni wengi sana ambao wana akili nzuri na tena ni watoto ambao wazazi wao hawajiwezi. Wanasoma, wengine wako Primary kunakuwa na michango midogo midogo ile mzazi wa kawaida anashindwa kutoa na yule mtoto wake anashindwa kusoma kumaliza hata darasa la nane. Tunaona hata kufikia Secondary, wengine wanafika pengine kama ni huu msaada unaotolewa kama bursary pengine anapatiwa kama elfu mbili tu - na mkiangalia kweli elfu mbili mtu ambaye anasoma Secondary school huyo mtoto hawezi kusoma. Unaweza kutoa hizo elfu mbili, na hizo elfu mbili bado hujamsaidia yule mtoto. Bado anahitaji pocket money, tumeshaona kuna mambo mengi ndani yake ili mtoto asome vizuri.

Unaona watoto wale ambao wanatoka katika nyumba sawasawa au pengine wanasoma na wale ambao pengine mishahara yao wazazi wao ni wazuri unaona watoto wengine hata wanaenda kuibia wengine. Wanakuwa wahalifu hapo katika mashule. Wengine wanaibiwa wenzao. Unasikia visa vimetokea namna hiyo.

Sasa nilikuwa naomba hivi, kwamba Katiba ipitishe ya kwamba mtoto ambaye anatoka katika mwananchi wa kawaida na ni mzuri katika masomo, - tunajua ni faida kwake na kwa mzazi, tena kwa nchi yetu hii ya Kenya, - kama anapatiwa msaada wa kusoma, hebu na ashikwe kwa mikono miwili, afundishwe, amalize shule na Serikali isimwache kulingana na akili yake na elimu ile ako nayo. Apatiwe ujuzi kulingana na vile anavyotaka, afundishwe na amalize. Nasema Serikali yenyewe ichukue jukumu ya kumpatia yule mtoto kazi ili tuweze kuwa na watu ambao wanaweza kujisimamia wenyewe pia na familia ya kwao pia hata na Serikali yetu kwa ujumla.

Kwa hivyo jambo hilo nasema kama ni Serikali kama ni shirika, ikichukua mtoto ihakikishe kama imemuchukua kutoka darasa la kwanza mpaka hata kama ni University amalize na tuone ya kwamba huyo tumepata raia mzuri katika Kenya yetu na atasaidia Kenya nzima hata kwa ulimwengu kwa ujumla. Hilo jambo likiwekwa katika hiyo Katiba, ikipitishwe katika Kenya nafikiri Kenya yetu itakuwa imebadilika.

Jambo lingine ni kwa upande wa wanawake, - katika usawa kati ya wanaume na wanawake. Nikizungumza hivi mimi nilikuwa nikifanya kazi katika ofisi ya utawala na nimestaafu. Baada ya kuacha kazi niko katika vikundi tofauti tofauti na nilitangulia katika wadhifa fulani katika hicho kikundi – lakini tunaposhughulika kwenda katika hizo ofisi za Serikali, unapowasilisha mambo yale yanatakikana. Unaweza kuona katika zile ofisi wanaanza kukuona wewe kama mwanamke na wasikuchukulie kukufanyia haraka kama yule mwanaume mwingine. Wewe unachukuliwa tu kama mwanamke - wewe kaa kando kwanza azungumze na mwanaume. Kwa hivyo ndio nataka kusema ya kwamba, wasahau ya kwamba huyu ni mwanamke aangalie ile hoja ameleta ni kitu gani ameleta pale. Kwa hivyo hapo natetea katika kusimamia katika shughuli zozote zile. Wanawake wasichukuliwe kama mwanamke lakini anaposimama pale ajue anasimamia katika kile kikundi na katika kila kusimamia ile sehemu na katika kufanikisha nchi yetu kwa ujumla.

Kwa hivyo nikimalizia nataka kusema ya kwamba mimi ni mstaafu nilikuwa nikifanya kazi na Serikali na nimeachia mwaka wa tisaini na sita na huu mwaka tuseme nimemaliza miaka sita. Na katika kufuatia ile haki za mtu au mapato ya mtu baada ya kustaafu, naona kuna unyonge sana. Katika maofisi wako na upole. Tunaomba Katiba hiii iangalie watu wanaostaafu kwa maana mtu akistaafu hana mapato mengine anatarajia kutoka ile ya kazi alikuwa anahudumia Serikali yake. Serikali imwangalie ajisikie ya kwamba 'ni mimi nilikuwa nikitumikia Serikali yangu nayo inanitunza.' Kwa hivyo zile haki za mtu angepata ziwe zinafuatiliziwa kwa njia inayofaa. Kwa sababu kuna wengine wanakufa hata kabla ya kupata haki zao na ni haki angepata kwa wakati unaofaa. Kwa hivyo kwa kifupi hayo ndiyo nilikuwa nayo machache kwa wakati huu. Asanteni sana.

**Com. Kabira:** Asante sana Mama Lillian. Nahason Msimba. (Hayuko). Alvis Kiungu. (He is outside). Salvo Nzae. (Hayuko). Walo Mwatalu. Hayuko. Mbogoli Tole. Mbogoli did he present? Okay. Jeniffer Milton. Jeniffer uko?

**Alvis Nyambu Ibrahim:** Kwa ma-commissioners wananchi mliofika kwa …….

**Com. Kabira:** Ngojea kidogo. Jeniffer unakuja? Hayuko. Na wewe ni nani? Ulikuwa nje?

**Alvis Nyambu Ibrahim:** Jina langu naitwa Alvis Nyambu Ibrahim nawakilisha waislamu wa Mwatate na haya ndio maoni yao waliyoyatoa - Mwatate Jamia Mosque, na walianza na mahakama. Kazi ya Kadhi na Kadhi mkuu ihusike na mambo ya mahakama kama maofisa wengine wa mahakama zile zingine. Pia walipendekeza kuweko na mufti - hicho ni cheo katika mojawapo ya vyeo vya kiislamu, atakaye wakilisha masilahi ya waislamu nje ya mahakama kama vile Bungeni. Lazima watimize masharti kama wengine kama kwa mfano awe na elimu ya sheria kikamilifu kulingana na dini ya kiislamu, awe na elimu kikamilifu ya dini ya kiislamu, awe mtu wa kuheshimika na mwenye hekima na busara. Kadhi ateuliwe na aidhinishwe na tume ya maulama. Kadhi ateuliwe na aidhinishwe na tume ya Maulama na Masheikh kwa kutumia usaidizi wa Serikali. Halafu wakipatikana wa kiwango kimojawapo wapigiwe kura na waislamu wenyewe nchini. Mahakama ya Kadhi yashughulikie maswala yote ya waislamu kikatiba mahakamani.

**Honourable Marsden Madoka:** Commissioners na wananchi kwa ujumla nawasalimu nyote. Mengi yametajwa lakini nitaongezea machache. Kuhusu Local Authority zipewe uwezo - kama vile chairman ameeleza, - ipewe uwezo wa vile tutaweza kutumia hizo pesa. Lakini tukifanya hivyo lazima pia katika Katiba tuweke kiwango fulani cha wale watu ambao tunajua kweli wakipata hizo pesa zitaweza kutumika sawasawa. Kwa sababu wajua zikija pesa nyingi hapa Local Authority, mnaona Chairman hapa Zacheus Augu labda sasa atataka kupeleka Mercedes badala ya kupeleka hii 504 halafu pesa zinatumika vibaya. Kwa hivyo tunataka kuweko na taratibu ambazo pesa hizo zikija katika wilaya zitatumiwa sawasawa na hapo ndio ninashirikiana na wenzangu kwamba katika wilaya kama ni ma-chairman wachaguliwe direct na wananchi.

**Clapping from the audience.**

Halafu hapo ndio kweli watajiona wana wajibu wa kutumikia hao wananchi. Yaani kwa kizungu tutasema watakuwa "accountable" kwetu sisi ambao tumewachagua wao. Na kweli wakifanya makosa tuwe na uwezo pia wa kusema huyu ameenda vibaya hatumtaki. Wananchi wa wilaya wapewe huo uwezo. Lakini kusema nasema majimbo sitaki, pesa zipelekwe kama ni Pwani, ati sisi twende kung'anga'na, - tunajua mahitaji yetu hapa Taita. Au namna gani? Sisi ndio tunajua, tunajua njia ipi mbaya ni wapi tunataka maji, ni wapi tunataka kunyunyisia mashamba yetu maji na kadhalika. Kwa hivyo tusigusiwe na hiyo njia ndefu ati pesa ziende katika Central au katika Regional Government.

Jambo lingine ni kwamba watu wa hapa wameongea juu ya Upper House, Lower House lakini hawakueleza kazi gani itafanywa na hiyo Upper House na Lower House. Hawajasema kwamba tukiwa ndio na Upper House na Lower House hizo ni ghalama. Kwa sababu kama mapato pia yanapatikana ya Serikali yataenda kama ni kulipa hao wengine wa Upper House, wengine wa Lower House, kwa nini tuwe na ghalama kama hizo? Vitasaidia nini? Mimi naunga kuwa na jumba moja peke yake katika utawala wa Serikali.

Ninaunga jambo ambalo limesemwa hapa kwamba katika Katiba inafaa isemekane kuwe vyama viwili, vitatu, vinne peke yake vya kisiasa. Kwa sababu sasa kuna vyama arobaini na mbili na vimekuwa ni vyama vya kikabila na tunajua ukabila ndio umezidi kuharibu nchi hii. Na hata ukiangalia Katiba za hizi vyama vyote, utaona Katiba ni kama sawa tu. Lakini kwa sababu ya watu binafsi wanataka uongozi ndio wanaanza kuanzisha vyama vyao. Basi ni vyema katika Katiba tuseme kutakuwako vyama viwili, vitatu, vine- ikiende juu kabisa. Halafu tuwe na hakika kwamba vyama ni hivyo peke yao kama mtu anataka kuingia amepewa nafasi, - iko democracia ya kweli anaweza kuchagua kati ya hizo vinne hawezi kukosa ambacho kinamfaa. Kwa hivyo mimi naunga sana jambo la kusema kuweko na limited number of political parties.

Mambo ya akina mama. Akina mama kweli ni lazima tuangalie haki zao. Ni haki kabisa lakini kila mara pia tunasikia akina mama wanasema tunataka usawa au namna gani? Tunataka usawa. (kitaita). Unataka usawa. Basi kama unataka usawa, kama ni kiti cha Bunge si upigane na mimi Kisawa? Kwa nini basi nikupe kiti?

**Clapping from the audience.**

Unataka usawa na kuna akina mama hatari sana ambao wakisimama kwa jukwaa hivi - hata Bi. Commissioner ukimwona hivi yeye hatari sana najua akitaka kiti pahali atanyakua upesi. Kwa hivyo tunasema kuwe ule usawa. Ni kweli hapo mbeleni labda waliachwa nyuma kidogo lakini sasa wanazidi kuendelea. Kwa mfano mnajua Mkubwa wa Serikali ni mama. Mzee kila mara hutuchekesha anasema 'mwanamke ndiye anakalia nyinyi nyote wanaume'. Tunasema ni sawa Mzee kwa sababu ana ujuzi ana nini, tunamkubali.

Kwa hivyo mambo ya akina mama ni kweli inafaa iangaliwe lakini sio eti kwa mfano katika Uganda, iko viti vya akina mama special. Tena ikija kwa viti vingine pia wanaruhusiwa kupigania. Sasa nikuonyesha hata tusipochunga Katiba kama hiyo, labda Bunge itatawalwa na akina mama. Tunasema akina mama wapigane na sisi kisawasawa.

Wakitushinda we will respect you - tutawaheshimu kwa sababu hata wewe mama why are you……kwa nini tayari unaanza kusema wewe ni mnyonge? Mkianza kusema eti 'mimi ni mnyonge niangalieni'- yes, if you are weak you are weak. Lakini tunasema fight your rights kama binadamu kama sisi wengine. Kwa hivyo akina mama nyinyi tunawaunga mkono katika juhudu zenu. Kuna haki kama yale ya mashamba na nini tunasema akina mama lazima kweli wapewe haki zao - wasinyanyaswe kwa upande huo.

Mambo mengine yamesemwa hapa eti ni Serikali ya mseto. Yaani labda National Government au Coalition Government, mimi ninapinga hiyo. Kwa sababu ukiangalia kama hata tukienda hapa Zambia juzi juzi wakati walitaka kutoa Kaunda vyama viliungana pamoja ndio wakaweza kushida lakini baada ya hapo, wakaanza kutawanyika, wakaanza kuleta taabu hata uchumi wa nchi ukazidi kuzoroteka.

Ukienda kama ni India, mara nyingi kwa sababu chama kimoja labda hakina nguvu zaidi kinachukua chama kingine halafu hapo katikati wanaanza kukosana tena, wanaanza kufanya uchaguzi tena. Ukienda hata Israel ambapo kuna mambo mengi hata wao mara nyingi wakiwa wanafanya kama hiyo Coalition Government kwa sababu hawana watu wa kutosha katikati ya ile wakati wao pia wamekosana wanaanza tena kufanya uchaguzi, - ni ghalama na kupoteza wakati.

Ninataka kuweko na chama ambacho ni kimoja na kinaweza kuunda Serikali. Lakini ati ilazimishe, - kama wakati tulipopata uhuru wetu,- kama walivyofanya South Africa. Labda ni kweli wakati huo kwa kujaribu kuleta watu pamoja, hiyo mambo ya National Government au nini labda ingekuwa sawa. Sisi Kenya tumepita kiwango hicho tumeenda mbali na sasa tuweze kusimama kama watu ambao tunajua tunafanya nini. Hilo ni jambo ambalo mimi nafikiria linafaa lifikiriwe sana tusije tukaanza kurudi nyuma.

Mambo ya utawala. Katika nchi yeyote lazima kuwekwe na ile tunasema law and order. Sheria ziweze kudumishwa na amani iwekwe. Bi. Chief hapa aliongea jambo la kweli, - kwamba tukisema machiefs wachaguliwe, kuweka ile sheria itakuwa ngumu. Kwa sababu hata Diwani hapa Kiliga anajua, ukienda kwake atakubembeleza sana, - hata kama hana kosa anaogopa kukuambia kwa sababu anafikiri litakuudhi na hawezi kuchukua hatua zile ambazo angechukua ili mambo yawe sawa. Kwa hivyo sisi tunasema, au mimi ninasema utawala wa Serikali lazima uweko.

Tunajua kwamba mwananchi akitaka jambo la Serikali anakimbia kwa Chief na tunajua machiefs wengine labda huenda wakatumia uwezo wao vibaya lakini hilo ni jambo ambalo linaweza kutengenezwa. Lakini Serikali inataka iwe na watu wake kule chini ambao watahakikisha kwamba usalama unaweza kudumishwa na mwananchi akiwa na taabu kuna mtu ambaye anaweza kumkimbilia na akahakikisha kwamba mambo yake yamefanyika.

Kuna jambo ambalo pia labda tungefikiria kama idara ya polisi. Labda badala ya kuwa na Commissioner of Police huko juu labda hapa Pwani tuwe na regional police. Au hata kama iwe ya hapa wilaya tuwe na polisi wetu na mkubwa wetu ambaye anaweza kuangalia mambo yetu.

**Clapping from the audience.**

Kwa sababu pia tunafikiria tukiwa na watu wetu, yale mambo mnasema ya ufisadi, mtoto wako hawezi kuja kukuomba kitu ati akupitishie kitu au namna gani. Kwa hivyo labda hiyo tunaweza kupunguza tukiwa na watu wetu ambao wanatufanyia kazi sisi na wanajua usalama ni nini. Kwa hivyo hilo ni jambo ambalo ingefaa pia tuweze kulifikiria. Mwingine hapa alisema kwamba hataki Waziri awe mbunge - Sio eti ninajitetea.

Maswali ambayo mjumbe wako analeta na Serikali inafaa ielezwe. Kama Waziri hayuko katika Bunge hayo maswali yenu

mkipeleka bunge ni nani atajibu kwa niaba ya Serikali? Kwa hivyo haya ni mambo ambayo watu wafikirie. Katiba ikisema - kama America kwa mfano wale wanaitwa ma-cabinet hivi kweli hawako katika ile Senate na nini - taratibu yao ni nyingine. Lakini Serikali nyingi katika Afrika au zile ambazo tutasema zilichukua Katiba zao au utawala wa kutoka kwa West Minister wajumbe huwa ndio mawaziri.

Lakini tunataka katika Katiba pia kuwekwe sheria kwamba wale ambao watakuwa nominated, - na hii nominated wanaoteuliwa wabunge, nia yake ni kwamba; Labda watu wakichaguliwa, labda kati ya wale waliochaguliwa labda hakuna mtu wa dini, au hakuna mlemavu, au hakuna muislamu, au hakuna mtu wa aina fulani. Iwe ina hakikisho ya kwamba kweli wale ambao wanateuliwa wawe kweli wanawakilisha watu labda ambao ule ujuzi wao hauko katikati ya wale ambao walichaguliwa.

Kwa mfano kama tumeona kati ya wale waliochaguliwa hakuna mtu kweli anafaa kuwa Waziri wa fedha, basi wateuwe mtu ambaye kweli anajua mambo ya wanaohusika na wizara kama hiyo. Hiyo tunataka iwe katika Katiba clearly kwamba sio eti uchague tu kwa sababu eti ni mtu wa Kanu, au mtu wa DP au mtu wa nini, tuchague kulingana na yale mahitaji tumeona labda yamekosekana katikati ya wale ambao walichaguliwa.

Kwa hivyo hayo ndio maoni yangu, nasema mengi mumesema nimesema yale ambayo ningetaka kusisitiza hapa katikati lakini nawashukuru kwa sababu kweli mmejitolea kuhakikisha kwamba Katiba hii itakayofanywa ni Katiba yenu nyinyi. Na tunataka Katiba ambayo ni rahisi kueleweka. Sio Katiba iko na mambo mengi mtu akisoma hata hawezi kuelewa, - we want a Constitution ambayo wananchi wanaweza kuelewa kwa urahisi na ile haki ya kibinadamu inadumishwa. Asanteni sana.

**Clapping from the audience.**

**Com. Kabira:** Asante sana Mheshimiwa kwa hayo yote maoni yako. Thank you for being with us this afternoon. Okay. Now we move on to Elizabeth Madoka.

**Elizabeth Madoka:** Asante sana pengine naongeza tu vile umesema kwa hivyo usiwe na wasiwasi. Ninashukuru sana wakati huu, mengi yamesemwa na nimeisikiliza na ninaunga mkono zaidi vile mume wangu amesema kwa sababu tulikuwa pamoja na ninajua vile amesema. Lakini kuna kitu kimoja tu ningeomba, - sijui kama itaingia kwa Katiba au kwa file. Wabunge wale tumechagua, wacouncillors wale tunachagua, tunatakikana tujue kabisa kazi yao ni nini. Shauri mwingine anasema anapita tu na gari hazungumzi na sisi. Atawezaje kwenda kufika kwa watu wote kama hana gari?

Na vile vile kunao wengine wale wako chini yake wanafanya kazi pamoja, na wanajua mahitaji ya wale wananchi. Wananchi tunapenda sana waangaliwe kwa shida zao. Nimeona vile wamekuja wakati wa huu tuko …..yeye yuko kwa Bunge - shida ni nyingi na zaidi kwa akina mama, za masomo ya watoto wao, wagonjwa - hata ndio unasikia wakitaja habari ya mahospitali.

**Clapping from the audience.**

Tungeomba kama hiyo Katiba inatengenezwa, iwe pesa zile zinagawanyiwa wenye Local Authority, wawe na pesa kama inapewa hapa Taita, ndio inapewa Kiambu ndio inapewa kila mahali ili wakikosa hiyo pesa na wao ndio wanajua zile shida za wananchi wa area hii, waweze kuwasaidia. Kama ni hiyo masomo, kama ni hiyo magonjwa na mahospitali. Hiyo ndio ninazidi kuongeza kwa sababu nimesikia kilio sana na nimeona hiyo kilio shauri inafika mpaka kwangu nyumbani - ili wananchi wasaidiwe kwa shida zao. Nashukuru tu na nasema asante. Nataka kurudi juu kidogo nifike kwa Rais, niseme vile wamesema kweli Rais awe ni term mbili tu na naona hakuna haja ya Prime Minister lakini naona iko haja ya Vice-President akiwa amechaguliwa ili waweze kufanya kazi pamoja na President. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Madoka na hata sisi tumefurahi kuona uko pamoja na yeye, kwa hivyo mambo yote ya wanawake tukitaka a-support tutakuja kwako. Asante. Josephine Mshimba. Josephine ako? Hayuko. Monicah Mwadime. Ameenda? Okay. Na mwingine ni Boniface Mwamburi. Amemaliza. Na Joseph Mande. Hayuko. Elias Mwasi. Ametoka? Okay. Mwashegwa Mwatalu. Walter Mwambogo. Asante. Kidodi F.M.C. (Ametoka.) Josephat Mwanguo. Hayuko. Mwawasi Njomo. Hayuko. Robert Msafari. Michael Kiuu. Pastor James Kivunike.

**Pastor James Kivunike:** Wapendwa nyote nawasalimu kwa jina la Yesu? Mimi naitwa Pastor James Kivunike, nakaa hapa Mwatate na hii ni bahati kubwa tueleze mazingira yetu, kuishi kwetu na kukaa kwetu kwa leo na kwa watoto wetu wajao zaidi kwa ajili ya Katiba hii inatengenezwa. Nimesikia mengi na wapendwa wamesema yote na hasa yale yanahusu uchumi, ile inahusu human rights ingawa iko imebaki kidogo kwa human rights haraka nizungumze hiyo.

La kwanza wacha nianzie pale jambo la kuhukumu watu kifo. Katika nia yangu na kamati ile tumeketi nayo hiyo ya kikanisa, sisi twaona kuhukumu kifo - death penalty, kuondolewa. Na nchi hii yetu i-negotiate na nchi zingine kama Comoro, Namibia, Seychelles, mtu akiwa amefanya jambo mbaya, amehukumiwa kifo achukuliwe nchi ingine inaitwa kwa Kizungu banishing - mumtoe akae nje atakuwa anafanya kazi kushinda kwenda kumkata shingo.

Lingine tunasema ni kuhusu freedom of worship au uhuru wa kuabudu. Katika Kenya yetu kwa sasa hivi kunahitaji mabadiliko haraka sana tena ya kweli tena ya msisimko. Tumekuwa wajumbe wengi, dini ni nyingi zahubiriwa kukakuja kama fujo badala ya haki. Mimi nimeona Katiba twaitengeneza tuwe na dini tatu zikubaliwe kwa kuwa watu wengi wa Kenya tuko katika dini hizo - Ya Ukristiano, dini ya Kiislamu na Hindu. Zingine zile hazijulikani kwangu nilikuwa nimesema na hiyo committee tumeketi nao, ziwekwe ndio ikakuwa twaruhusu fujo. Hata kwa Ukristiano wakati huu Katiba angeliweka discipline ya kushirikiana – yaani kwa mfano kwamba kanisa zijengwe mbali ya kilomita tatu kutoka kwa ingine - sio kujengwa kama viosk karibu karibu mwisho watu wakaanza kutoa farakana, watu wakaanza kuzozana, watu wakaanza hata kuchafua Injili yenyewe. Kwa hivyo hii kupanga panga tunataka Katiba iweke kwamba Msikiti au Kanisa au Temple isijengwe kupita kilomita tatu - Iwe kilomita tatu kutoka kwa ingine - ubali wa kutosha kusikuweko vita. Hiyo kufungia nje dini zingine itatuwezesha kufunga nje devil

worshippers.

Nchi yetu miaka hizi kwanzia miaka elfu tisaini devil worshipper wamechukua, wamesitawi, hata imekuwa shida. Sasa tunaona ajali nyingi kama Mtongwe, kama Bombolulu, kama huko Ukambani hiyo maskuli ilichomwa, tumeanza kumaka kumaka tu lakini hii yote imeletwa zaidi kwa kuwa devil worshippers wamekuwa wengi. Uhuru wa ku-worship usiruhusu hata vile vitu si vya faida kwa mwananchi ila ni vya hatari. Kwa hivyo kuongezea vile wengine wamesema, uhuru wa kuabudu uweko kwa Katiba, tukuwe na vitu vya haki na discipline ya kuhubiri Injili kwa haki kwa njia ile iliyoko - Si fujo tu, si kuweka kuweka tu.

La mwisho ninasema vile wengine wamesema ingawa wametoka nje, ati vyama vikuwe viwili vitatu. Vyama Kenya kwetu kama tunafanya ukweli kwa Katiba, vyama vyatakikana vinane. Kwa nini? Kuna watu wa mafikira ya kifanyakazi (trade unions), wanaweza kutaka kuunda chama kina mafikiria yale yamejaa kufanya kazi, tusiwafungie. Kuna watu wana mafikira ya Human Rights - akina Professor Kibwana, - ana timu sasa imekomaa ni kubwa, hao wanazungumza mchana usiku "Human Rights." Na hao wanaweza kuunda chama kinaosisitiza nguzo yao ya human rights.

Kuna watu wana mafikira ya culture, wale mumewasikia eti tufanye vyama vyetu utamaduni. Sasa huyo ukimfungia kwa chama umemuumiza roho, wacha chama kinachosisitiza utamaduni kiinuke. Hivyo ni vitatu. Nne, industrialists wale wa biashara biashara na hao wanahitaji chama chao kama hicho kimejaa biashara ingawa kutakuwa na vitu vingine.

Cha tano ni cha wakulima. Kuna watu wa mafikira yao inclined to farming. Kwa hivyo ukisema tufanye vitatu peke yake, umefunga watu dhamili zao zingine. Tena kuna Religionists sisi twataka hata Injili ihubiriwe mpaka Parliament mpaka Councils. Hao nao wanaenda kuunda chama tuseme twataka Injili ikuwe na uhuru tosha kwa kila area. Kwa hivyo vyama vinane, ni hayo mafikira nane yaliyoko Kenya - the thinking strands in a society now. Hicho nilikuwa nagusa kifikiriwe.

Cha mwisho hii Katiba kweli tumekuwa nayo haikuwa na preamble kama wengine wamesema; kwa hivyo hatukuelewa inaelekea nini ni kama sheria tu ilitungwa peace-meal. Twataka preamble ama ule utangulizi unaoeleza philosophia, mafikira yetu ya leo na kesho - yaani inayotutia moyo kwamba tuna future. Si Katiba imeandika sheria peke yake. Nafikiri ni hayo, mengine yamewekwa kwa karatasi zetu. Mimi nawakilisha kanisa na michunjo ikaandikwa na karatasi nafikiri nitaweka huko. Mungu awabariki.

**Com. Kabira:** Asante sana Pastor James Kivunike. Nitauliza kama Omar Athmani ako? Hayuko. Kuna mwingine anataka kutupatia maoni lakini hajaitwa? Ni wewe tu peke yako? Tutaanza na huyu. Utasema jina lako kwa sababu tuna-record. Umekuwa registered? Ukaitwa lakini ulikuwa nje? Ni sawa tu. Utataja jina lako kwa sababu uko kwa register uitaje huko halafu uzungumze. Okay. Asante. Kuna mwingine? Na wewe? Kwa hivyo wewe ndio utakuwa wa mwisho. Na wewe?

**Suleimani:** Mapendekezo yangu ya Katiba ambayo nimeleta mbele yenu ni kuhusu mashamba yetu. Ningependekeza ya

kwamba ………..

**Com. Keriako Tobiko:** Ngoja kidogo. Nauliza kuna watu wengine wanataka kuzungumza baada ya yeye? Wangapi wanataka kuzungumza? Fatuma, are the other people registering? So, ni watu wangapi sasa wamengapi? Wawili, watatu. Okey. Na ufupishe.

**Suleimani:** Mapendekezo yangu mbele ya Katiba yetu ya Kenya ambayo tunaisubiri kwa hamu sana ni kuhusu mashamba yetu. Kwa hakika, kuna watu wachache sana ambao wanamiliki maelfu ya mahectare ya mashamba huku wazalendo ambao ndio wengi sana wanakosa hata nukta moja ya shamba angalao ya kuzikiwa. Mashamba hayo ambayo yanachukuliwa ya mahectare nyingi zao huwa hazilimwi. Ziko kama mapori na huku wananchi wanataabika hapa na kukosa mashamba angalao ya kulima kupata sima ama hata ya kuzikwa.

La pili,

**Com. Keriako Tobiko:** Pendekezo lako kwa hiyo ni gani? What is your recommendation on the big parcels of land?

**Suleimani:** Pendekezo langu katika mambo hayo, ningependekeza kama wamechukua ma-hectare mingi ya mashamba ambayo hayalimwi, mashamba hayo yapokonywe watu hao yakabidhiwe wananchi wale ambao hawana mashamba kabisa.

La pili, ni kuhusu wanyama wa porini. Kwa hakika tunazo National parks hapa - areas kama hii yetu ya Mwatate, asilimia kubwa ya ardhi hapa imechukuliwa na wanyama wa porini - robo tatu ya ardhi yetu hapa imechukuliwa na wanyama wa porin huku wananchi wa hapa Taita Taveta wakibakia na thuluthi moja ya ardhi. Kwa hivyo unakuta kwamba sisi hapa tumezingirwa na wanyama wa porini na hao wanyama wa porini wanaingia mashambani kwetu, wakishaingia mashambani kwetu hatulipwi fidia yetu.

Lakini unakuta ng'ombe wetu wale ambao tuko nao wakiingia shambani kuna Agricultural officer ambaye amewekwa tayari wa kukabilia nini? Wakukabilia mimea ile ambayo imeharibiwa na wanyama wetu. Agricultural officer huyo anakupeleka mbele anakuchagulia mimea iliyoko hapo, unalipishwa pesa. Kama haujalipa hizo pesa ambazo agricultural officer amesema, sasa unapelekwa kortini.

Ningependelea, ningeomba ya kwamba ikiwezekana Serikali yetu hii iweke agricultural officer wa kukadiria mimea yetu ambayo imeharibiwa na wanyama kama ndovu, swala, ndege wa porini hata nyani. Iwe na agricultural officer ambaye huangalia mimea zetu zikiharibiwa na wanyama kama hawa.

Pendekezo la tatu ni kuhusu mahakama ndogo. Kuna watu ambao wanaenda kortini na kwa kweli huwa wananyanyaswa sana.

Unakuta ya kwamba mtu amepelekwa kortini, akishapelekwa kortini hapo kuna Serikali ina mtu wake-ina kiongozi wa mashtaka. Huyo kiongozi wa mashtaka yuko na yule mlalamishi pia yuko. Yule mshitakiwa huwa hana hata wakili. Mara ingine hana mtu wa kumsaidia na pengine hajui kuongea mbele ya korti. Unakuta anadhulumiwa na mashtaka ya uongo na kweli ambayo yanamtokezea hapo kwa vile hajui kuzungumza. Ningeomba ikiwezekana Serikali iajiri mawakili wa kutetea watu ambao hawajui kuongea na pia ambao huwa wanalaliwa sana na upande wa mashtaka.

La tatu ni rasilimali zetu. Ningeomba ya kwamba Serikali yetu iangalie rasilimali zetu za wilaya yetu hapo kabisa. Rasilimali zetu kwanzia mashamba hii ya mikonge, madini, maduka yetu yote hapa tunatoa pesa zote zinapelekwa huko Nairobi, City huko – zinakwenda kutumiwa huko na watu sisi hapa huwa hatuwajui. Unakuta pia hapa tunalalamika shule zetu zinakosa vifaa hata choki hatuna, pesa zote zinapelekwa kule. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba asilimia sabini na tano ya rasilimali zetu zibakie hapa hapo hiyo Serikali kuu ipelekewe asilimia ishirini na tano peke yake iwe ni yao ya kuchezea huko na kujenga viwanda vya silaha.

Pendekezo langu la tano ni utawala. Utawala ningesema Chifu na Naibu wake kwa kweli wamepewa mamlaka zaidi hata ya kuchukua ardhi ya mtu ama kuingilia mambo ya mtu ya nyumbani. Ningependekeza mamlaka hayo kwanza yapunguzwe, pili Chifu huyo na Naibu wake ikiwezekana tuwachague moja kwa moja kwa kura.

Ya sita ambayo ni ya mwisho ni kuhusu mashirika. Hapa kwetu Coast Province tuna mashirika mengi sana. Kenya Ports Authority, nini nini ziko hapo zote lakini unakuta katika mashirika hayo, viongozi walioko hapa wanatolewa pande zingine - wanatolewa sehemu zingine huko. Mkongo wa kuanzia juu mpaka wa katikati ndio unakuta "Kamtaita" ketu kamewekwa hapo. Ama "kamtu" ka pwani kanawekwa chini hapo. Ningependekeza mashirika kama hayo yaliyoko hapa kwetu katika Coast Province yawe yakisimamiwa na mtu wa hapa hapa Coast Province ikiwezekana, kwanzia wa kwanza na wa pili hata na wa tatu. Kwa mpango wa kazi asilimia tisaini iwe vijana wa hapa hapa Coast Province. Nafikiri hapo ni mwisho wangu.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe hapo na upeane karatasi. Nani mwingine? Kwa ufupi sana ndugu yangu.

**Alfred Mwadama:** Kwa majina mimi ni Alfred Mwadama na natoka hapa Mwatate. Ma-commissioners wetu nashukuru sana vile mlivyokuja, na Katiba yetu sisi tungependa mambo mengine machache - mengi yashazungumzwa na wananchi wenzangu. Sisi ijapokuwa tumekuwa ni watu wa mwisho mwisho, lakini kusikiza hayo yote ndio uzuri kupata flavour. Kunayo mengine machache labda yamesahaulika na labda tungependa turekebishe na iingie kwa Katiba yetu.

Kuna hii hali ya hawa madereva wetu. Madereva utakuta dereva ameshawahi kuua karibu mara tatu nne - ana gari yuko njiani kila wakati. Dereva ashasababisha vifo vya watu wengi sana. Badala ya Serikali vile inajua huyu mtu ana licence hiyo, sheria iundwe sasa ikiwezekana mtu kama huyo ametoa uhai wa watu kadha, anyimwe kabisa hii licence - Ifutiliwe mbali, asiweze tena

kurudi barabarani.

Maisha ya watu wengi sana wetu yameisha kwa sababu ya haya magari. Dereva amegonga safari ya kwanza, safari ya pili, safari ya tatu. Lakini utakuta bado tena anaenda anafungwa kidogo, pesa nyingi zatoka kwa tajiri, anatetea dereva anarudishwa tena kwa gari. Yule mtu unamwona kesho yuko barabarani. Kwa hivyo hiyo iingie kwa Katiba iweze kabisa, itilie mkazo, dereva yote atakaye fanya zaidi makosa kama hayo, apatikane makosa si ya yule aliyekufa, ni dereva, afutiliwe mbali ile licence yake. Nafikiri hilo likiingia itakuwa uzuri sana.

Vile vile kwa upande wa hawa waizi, washinzi, Katiba hii yetu tungependa mambo yote yarejeshwe kwa wazee vijijini vile tunavyotaka. Atakapopatikana ni mwizi hukumu itoke kwa wanavijiji wenyewe ya kumhukumu yule mwizi. Kwa sababu mwizi atakuwa kila mara anajulikana yu aiba, anajulikana na watu wote lakini anaenda anafungwa yeye ndiye mmoja anajua kula na wale maaskari zaidi. Akirudishwa vijijini mnamwona siku mbili tatu ndiyo huyu tena - ametaipisha mali nyingi za watu. Kwa hivyo kuweko na uwezo Katiba hii yetu, sheria itoke, maamuzi yatoke kwa wanavijiji wenyewe watoe uamuzi wa kuhukumu yule mtu. Asante sana.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe hapo kabla haujaenda. Wewe ndio utakuwa wa mwisho sasa.

**Omar Athmani:** Mimi ni Omar Athmani kutoka msikiti wa waislamu wa Ndembwa. Nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii kueleza machache ambayo yanahusu Katiba kwa jamii ya kiislamu. Hapa tulipendekeza kwamba Chief Kadhi lazima achaguliwe na waislamu wenyewe na awe na elimu ambayo kwa upande wa kizungu, awe ni mtu wa form four na tena awe na elimu ya kiislamu ambayo inahitajika kwa kutekeleza jukumu. Kwa sababu akiwa mtu haelewi kiislamu au kizungu itakuwa ni vigumu sana kujua matatizo yote ya mwananchi maana elimu pia ni msingi wa uongozi.

Chief kadhi pia awe na mambo ambayo anaongoza inalingana na sheria za kiislamu kwa sababu wakati mwingi unaona ya kwamba waislamu huwa na matatizo kwa sababu unakuta jambo fulani linatokea la kiislamu halafu unakuta halitangazwi kulingana na sheria za kiislamu. Kwa hivyo ni lazima mambo ya kiislamu, Chief kadhi atangaze mambo kulingana na sheria za kiislamu.

Kuhusu mavazi. Tunaomba ikiwezekana mavazi hasa kwa jamii ya kiislamu au watoto wa kiislamu, wawe wanaruhusiwa katika Katiba ikiwezekana wawe wanafaa mavazi ya kiislamu kwa sababu hiyo iko katika sheria kiislamu hawaruhusiwi kuvaa mavazi ambayo inaleta aibu katika jamii. Siku ya ijumaa kwawaislamu huwa ni siku yao kubwa sana kama vile inavyokuwa jumapili kwa wakristu.

Tunaomba ikiwezekana wawe wanapatiwa nafasi ya kuabudu Mwenyezi Mungu kwa siku hiyo ikiwezekana - ifanywe kama jumapili vile wakristu wanavyopewa likizo ya jumapili. Kwa sababu mara nyingi huwa wanapatiwa shida - mtu wakati unataka

kwenda msikitini inakuwa ni vigumu hata saa zingine kupatiwa nafasi ya kwenda kwa msikiti. Kwa hivyo wakati mwingi huwa tunataabika sana sisi waislamu.

Pia tunaomba katika Katiba kama itawezekana wale wanaopata mishahara ya juu, wale wanaopata mapato ya juu ikiwezekana, kodi ya mapato iwe juu kwa sababu tunatarajia mapato kama hayo ikiwa inatoka namna hiyo tutapata shule za msingi za bure na pia tutapata matibabu ya bure. Maanake tutapatiwa pesa kutoka hapo.

Kwa upande mwingine tunaomba ya kwamba ikiwezekana Rais awe chini ya sheria - sio kama kwa wakati huu Rais yuko juu ya sheria unakuta sheria zingine haziendi sambamba kwa sababu anaweza kuingilia kwa mfano, mtu ameshtakiwa kortini pengine ni mkubwa au waziri ameshtakiwa kortini, anapiga simu au anawakilisha kitu chochote, unakuta hiyo kesi inafutwa, maana kwa hivi sasa yuko juu ya sheria. Tunaomba ikiwezekana katika Katiba ijao awe chini ya sheria. Mtu akifanya makosa ashitakiwe vile inavyotakikana na ahukumiwe kulingana na wajibu wa sheria.

Upande mwingine naomba kwamba ikiwezekana Rais achaguliwe na wananchi kwa kupitia asilimia ishirini na tano kwa Kenya nzima. Pendekezo lingine tulipendekeza ikiwezekana ma-DO katika division wapunguzwe kwa sababu tuko na ma-chief na ma-sub-chief na huko juu tuko na DC. Ikiwezekana ma DO wapunguzwe kwa sababu ya kupunguza ghalama za Serikali kulingana na hali tunavyoiona.

Kwa upande mwingine tulipendekeza bunge isiwe na mamlaka ya kuvunja sheria yeyote katika Katiba – Ikiwa kuna sheria yeyote ya kurekebishwa irudishwe kwa wananchi kwa sababu mara nyingi tumeona wabunge wanakutana na wanagongana gongana mara wanavunja kipengele kingine cha sheria. Hiyo tumeona imekuwa shida kabisa kwa wananchi na wanataabika na wengine wanapata shida.

Kuhusu wanyama wa pori, tumependekeza kwamba ikiwezekana zile pesa zote zinazopatikana katika wilaya ile inahusika, iwe inapatiwa kiwango kikubwa cha pesa kuliko zote zitatoka kwa Central Government halafu hao wametoka hapa ndio wanapewa kitu kidogo - ikiwezekana wapewe nafasi ya kwanza au pesa hii kubwa kwa kujitimizia katika sehemu yao.

Kuna jambo lingine ambalo tumependekeza la mwisho - Mkenya yeyote - kwa hivi sasa inasemekana kwamba Mkenya yeyote anaweza kuishi mahali popote bila kupatiwa shida - lakini kwa upande wetu tulipendekeza Mkenya yeyote anaweza kuishi mahali popote bila kutatizwa lakini ikiwa anaishi katika ardhi au amenunua plot lakini aishi kulingana na sheria za wananchi wa pale. Kwa sababu mara nyingi watu kama wale wanavuruga sheria za kimila.

Kwa upande wa mwisho tutapendekeza ikiwezekana, kwa sababu mara nyingi mambo mengi tumeona yanafanywa kutoka huko juu au kupitia Serikali kuu au waliochaguliwa, katika sehemu zile tusiwe na reserve au za wilaya au za Province, zinapata shida kulingana na mapato. Yaani kwa mfano mapato mengine kama pesa hizi za kutoka Coast au katika Provinces zote

zinapelekwa katika Central Government. Unakuta mambo mengine katika sehemu hizi za chini zimelaliwa. Basi tukapendekeza kuwe na Serikali ya *majimbo* - lakini sio kusema eti Serikali ya *majimbo* eti tunabagua mtu hivi - mtu anaishi kulingana na sheria vile wananchi wa pale wako. Mimi sina mengi ya kusema lakini naomba kwamba Mungu atubariki kwa Katiba hii ambayo tunaunda, ikiwezekana Katiba iwe inaangalia masilahi kamili ya wananchi bila kubagua jambo lolote au kubagua mtu yeyote.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante ndugu yangu. Jiandikishe. Kuna mtu mwingine? Na iwe kwa ufupi sana ndugu.

**Emmanuel Mzungu:** Mimi naitwa Emmanuel Mzungu, natoka hapa Mwatate. Mengi yameongewa lakini pia ningependa kusisitiza kwa kusoma, kwa sababu yangu nafikiria itawafaa wote. Kwa hivyo ningependa niyasome na kama pia Tume ya urekebishaji wa Katiba ingeniruhusu nisome, niko na page tisa tu peke yake. Asante.

Kwanza ningeanza na Katiba. Katiba iwe na utangulizi na uzalendo, itoe uwezo na kanuni za kuweza kumfuta Rais akiwa amefanya uhalifu fulani na kufuju au kuhalifu Serikali, idumishe pia Katiba kikamilifu mila na desturi za makabila mbali mbali, iandikwe kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na baadaye ifuatiliwe kwa lugha mbali mbali. Iwe ikifundishwa shuleni na iwe rahisi kupatikana kama kuuzwa kwa maduka ya vitabu.

Halafu ningependa kuongea juu ya Rais. “Rais achaguliwe kwa wingi wa kura - asilimia hamsini au zaidi na apate asilimia ishirini na tano kwa mikoa mitano. Awe kati ya miaka arobaini na tano hadi sitini na atumike kwa miaka kumi pekee au vipindi viwili vya miaka kumi. Awe Rais wa nchi mwenye mamlaka ya kadiri na asiwe kiongozi wa Serikali. Awe na kiwango cha elimu cha kidato cha nne au zaidi. Rais asiwe mbunge wala mwenyekiti au mwanachama wa chama chochote cha kisiasa. Mwananchi au wananchi wapewe uwezo wa kumuondoa Rais kwa kura ya maoni ambako itajumulisha makamu wake pamoja na wabunge. Kuwe na makamu wa Rais atakayechaguliwa kwa wingi ya kura ,yaani running mate asilimia hamsini na moja au zaidi.”

Kuwe na Waziri Mkuu pia. Hii itatuwezesha kusimamia rasilimali za nchi maana Rais amekuwa na mamlaka makubwa. Amesimamia dollar na akasimamia Serikali. Kwa hivyo mtu atakayesimamia Serikali na atakaye simamia dollar ambaye ni Waziri Mkuu. Akiwa kutoka chama kilichopata viti vingi bungeni. Halafu kwa Serikali kuwe na Waziri Mkuu atakayekuwa na chama kilichopata wabunge wengi uchaguzini na aliye chaguliwa na bunge. Kuwe na makamu wake atakaye pia chaguliwa na bunge na atoke kwa chama cha pili kutokana na viti vya wabunge.

Kuwe na mawaziri ambao hawatakuwa wabunge kwa sababu, tunachagua Mbunge hapa anakwenda kulishwa Waziri na kumbe hana ujuzi wa uaziri. Kwa mfano tunaweza kuwa tumechagua kwa mfano kama mbunge wetu hapa Major Marsden Madoka ambaye tunamjua saa hii ni Waziri wa nchi za nje. Na ujuzi na taaluma yake tunajua alikuwa ni mwanajeshi, - mtu wa kupiga bunduki, halafu aanze kuchaguliwa katika wizara ya afya - hata ukimweleza mambo ya ‘typhoid’ hajui. Achaguliwe katika Wizara ya Ulinzi na wizara ya Afya ipewe mtu ambaye ana taaluma ya udaktari.

**Clapping from the audience.**

Halafu kuwe na mawaziri ambao hawatakuwa wabunge, wateuliwe na Rais, waidhinishwe na bunge na wapendekezwe na Waziri Mkuu, tuwe na Serikali ya mseto. Kila chama kipendekeze kwa Waziri Mkuu, majina ya mawaziri na manaibu wao, kila wizara iwe na waziri mmoja na naibu mmoja na wachaguliwe kulingana na taaluma zao. Waziri awe na elimu ya kidato cha nne ama zaidi. Mkuu wa sheria apendekezwe na Chama Cha Wanasheria cha Kenya kwa Waziri Mkuu na ateuliwe na Rais, na aidhinishwe na Bunge na uwezo wa kumfuta kazi au kumuondolea mamlaka upewe wananchi.

Makatibu wakuu wateuliwe na Waziri Mkuu na waidhinishwe na wabunge. Utawala wa mkoa, yaani Provincial Administration ufutiliwe mbali na badala yake wachaguliwe wenyeviti yaani Chairmen kwa kijiji hadi mikoa - na wawe wenyeji wa sehemu zao na watumike kwa vipindi viwili vya miaka mitano. Sababu ya kusema hivi ni kwamba tumekuwa na watawala kama ma DC na ma DO ambao hata (kitaita). Sasa tunataka watu ama watawala wachaguliwe kama machairmen wa hapa na wahusishwe kuwa wenyeji.

Halafu tukiingia kwa Bunge. Ningesema Bunge liwe na uhuru wa kujipangia calendar yake lenyewe. Rais asiwe na uwezo wa kusimamisha au kuvunja Bunge na asiwe na uwezo wowote wa kuingilia Bunge. Hii tumeiona saa hii kwa sababu tukichagua mbunge, akipelekwa pale mbele anakuwa kwamba hatuangalii sisi anaangalia Rais na Serikali kuu. Kwa hivyo tunataka mbunge akichaguliwa awe huru na akienda pale, Bunge liwe huru liwe linasimamia maswala ya wenyeji - maana Mbunge tukimchagua anatakikana kusimamia sisi. Wabunge wawe na elimu ya kidato cha nne au apitwe ile inaitwa "Proficiency test" ya Kiingereza au Kiswahili. Awe kati ya miaka ishirini na nne hadi sitini. Wananchi wapewe uwezo wa kuondoa Mbunge wao kwa kura ya maoni hata kabla hajamaliza miaka tano.

Pia Bunge liwe na uwezo wa kupanga na kuidhinisha Mapato na Matumizi ya Umma. Kwa sababu tumeiona imekuwa wazi kwamba hata tukichagua Mbunge, hawezi kwenda pale na kusema kwamba mapato ya Wataita yatumiwe kwa hivi na hivi - kama kwa hospitali, mashule, barabara na mambo kama hayo. Akienda pale anasikia vile Serikali inasema, ikisema mapato ya Wataita ipelekwe kwa upande huu, anakubali kwa sababu ameingizwa katika Serikali na hiyo hatutaki.

Pia Bunge liwe na uwezo wa kumfuta mtumishi yeyote wa umma au mshirika wa umma na kumlazimisha kulipa au kama amefanya tatizo lolote la kuhusu uvunjaji wa pesa za umma, kulingana na ripoti ya mkaguzi mkuu, au kutumia ofisi vibaya, au kosa lolote, basi Bunge hilo liwe na uwezo wa kumfuta kazi.

Pia Bunge liruhusu kwamba Mbunge atakaye patikana na hatia, asishikilie cheo chochote cha umma maishani mwake - maana wengine wanarudishwa na wamefanya makosa - wanakula pesa za watu tena anarudishwa. Hatutaki hiyo. Katiba mpya isimamie hiyo mambo. Bunge liweke kiwango cha safari za Rais na matumizi ya afisi hiyo yakaguliwe kwani safari za Rais ni

ghali mno na manufaa yake wananchi hayawafai. Utakuta Rais anaenda na safari zake zinaandikwa katika mzururu wa mipango za Serikali na hazifaidi mwananchi wa Kenya. Utakuta Rais ameenda kutibiwa mambo yake huko. Utakuta Rais ameenda kuchekia mali zake huko na inabidi aje wabunge wamuekee sahihi na pesa zitoke katika mfuko wa umma. Hayo mambo yafutiliwe mbali na Bunge liwe na uwezo wa kukataa hayo mambo. Halafu pia ofisi ya Bunge, ikitumiwa vibaya pesa za umma,Rais asilipe na kuondolewa mamlaka - vile vile Waziri au naibu wake kuondolewa kwa kutumia vibaya pesa za umma.

Halafu mahakama. Ili kuwezekana ama kuwezesha mahakama kuwa huru, Judge mkuu apendekezwe na Chama Cha Wanasheria nchin Na aungwe mkono na makundi ya kidini na wanaohusika kama vile majudge wa mahakama kuu na ya rufani. Wapewe ulinzi wa ofisi na Bunge peke yake na liwe na uwezo wa kufuta majudge hawa kwa kura asilimia sitini na tano. Rais au Waziri Mkuu au mkuu wa sheria asiyaingilie mahakama.

Maprosecutor wawe mawakili na si mapolisi. Kwa sababu utakuta askari amefika darasa la nne, hajui chochote anakwenda pelekwa pale kortini Voi. Hajui hata kutetea mtu na kuwa awekwe mtu ambaye yuko na taaluma ya sheria kama vile wakili. Kwa hivyo polisi waondolewe katika prosecution. Pia Bunge ipewe uwezo wa kushtaki Serikali, Rais, Waziri Mkuu kama itakuwa na ukiukaji wa Katiba. Hii ni kwa sababu tumeona malimbikizo ya mamlaka imekuwa kwa Rais kwa hivyo ikiwezekana Rais apokonywe hayo mamlaka.

Halafu tuingie katika ardhi hapa Taita maana Tume imekuja Taita naongelea mambo ya Taita. Hati za kumiliki mashamba zitolewe wilayani na wenyekiti wa vikao vya ardhi wawe wenyeji. (kitaita).

**Clapping from the audience.**

Halafu tena ---

**Com. Keriako Tobiko:** Ndugu kuna jambo moja ambalo limeniruka hiyo umeongea kwa lugha yenu nataka kuelewa pia na mimi.

**Emmanuel Mzungu:** Nitaongea Kiswahili sasa. Haki za kumiliki mashamba zitolewe wilayani na wenyekiti wa vikao vya ardhi awe mwenyeji. Haki hizi zisitolewe Nairobi - Nikisema hivyo ni kwamba, nilisema Kitaita narudia Kiswahili ni hivyo, - Hati za kumiliki mashamba zitolewe hapa hapa. Kwa mfano hapa Wundanyi katika history yetu ipewe huo uwezo na ndio zitatolewa na wenyekiti ambao tumechagua sisi wananchi sio watu wa kutolewa huko kwa ma DC na ma DO- hatutaki hayo mambo na wakati ardhi inatolewa kibali iko hapa Taita. Na iwe ni ardhi ya Serikali au trust land na habari zozote kuhusu ardhi zichapishwe kwa magazeti ya kawaida yaani kama vile *Taifa* ama *Nation* – wala Kenya Gazette kwani gazeti hili la Kenya Gazette limetumiwa vibaya na Serikali, kunyanyasa wananchi haki zao na ni wazi kwamba, gazeti hilo halipatikani kwa urahisi - lapatikana huko hatuelewi ni wapi.

Hii mambo ya ardhi, Katiba ile iliyoko iruhusu unyakuzi wa ardhi kama haki ya Wataita kumiliki mashamba ya mkonge. Mwatate sisal estate, Taveta, Ziwani, Jipe, Kidai na kadhalika. Nikisema hivyo ni kwa sababu mashamba haya toka tupate uhuru na wakati ule tulikuwa tunatakiwa tupate uhuru ---

**Com. Keriako Tobiko:** Ndugu hebu rudia tena hizo majina za Sisal Estates.

**Emmanuel Mzungu:** Okay. Zile estates zilizoko Taita estate Mwatate, Taveta estate, Ziwani, Jipe, Nakitai, Kidai - ile iko pale inamilikiwa na Wakamba, pamoja na Voi ile iko na Vishram na kadhalika, hizi zirudishwe kwa wananchi. Nikisema hivyo ni kwa sababu shamba hizi wakati tulikuwa tunapigania uhuru ijapokuwa hatuweko sisi ni watoto, lakini kuna wazazi wetu walipigania uhuru, Serikali ya Uingereza ilikuwa na uwezo wa kukopesha nchi yetu pesa ili kwamba mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na mkoloni yarudishwe kwa wenyeji. Ilivyofikia wakati huo, wenye mamlaka waliokuwako wakati huo kama vile Rais Kenyatta, wakachukua nafasi hii kutunyang'anya mashamba yetu kwa kuyachukua na kuyanunua na kupeana familia zao.

Kwa hivyo kwa hivi sasa lease zilizoko za kumiliki haya mashamba yetu tuliyoyataja, zifutiliwe mbali na zirudishwe kwa wenyeji - hata Uhuru pia hatumtaki. Kuna ushahidi katika mashamba haya. Ngonja niseme sawasawa kwamba Serikali ya Uingereza kupitia kwa Sir Isaac Walton waliwakopesha Wataita shilingi milioni mbili tarehe thelathini mwezi wa kumi na mbili mwaka wa sitini na nne na ili hali tulinyang'anywa mashamba haya kwa njia ya lease na familia ya Kenyatta. (kitaita). Tunataka yarudishiwe Wataita. Mapendekezo yetu sasa kuhusu haya mashamba.

Lease zote za mashamba ya makonge zifutiliwe mbali maana ikiwa huyu Mu-Greek anayefanya kazi hapa kwa shamba la Beth Mugo ambalo linaitwa Taita estate, atapewa lease ya miaka mia tisa na tisaini na tisa, Wataita hawatakula chochote. (kitaita). Hiyo iondolewe - lease zifutiliwe mbali. Wenye shamba hizi walipe Wataita fidia kwa muda waliotumia mashamba haya. Pia waeleze walizipata kivipi. (kitaita). Na kama itakuwa imepewa Kikuyu ama Wa-Greek, je wao walizaliwa na Mwangeka wa Maloba?

Tano, mbuga za wanyama wa pori - yaani Tsavo east, Tsavo west, Taita hills, Game sanctuary zigeuzwe ziwe game reserves ili zitumike kwa wenyeji ama zinufaishe wenyeji kama vile Meru na Masai mara. Mbuga za Tsavo east na west zitunzwe na pia zipunguzwe kwa asilimia hamsini - 50% yaani kutoka 62% ya ardhi ya Wataita hadi 31%, na ingine igawie wenyeji ambao kwa sasa wana asilimia 11.9% pekee na wengi ni ma-squatter. Kwa nini?

Uchumi na mali asili yaani rasilimali: Kwanza nitaanzia madini ambayo ndio "kahawa" ya Wataita. Hakuna mmea utakao ota chini ya miaba na Taita tumebarikiwa na miaba iliyo na madini. Vibali vya utafutaji na uchimbaji madini vitolewe kwa wilaya inayohusika kama Taita taveta wala si Nairobi ama Nairobi ni Taita? Maana tumeona watu wanatoka juu na vibali vyao vya Prospecting rights, wanakuja hapa wananyakua shamba la Mzee Mwaewa wakisema "nimepewa title deed" ama kibali cha

Prospecting rights na huyo mzee anaondoka ni mwenyeji. Vibali hivi vitolewe katika wilaya zinazohusika kama nilivyosema Taita taveta ama Wundanyi.

**Com. Keriako Tobiko:** Nani atoe kwa district, kwa wilaya?

**Emmanuel Mzungu:** Nataka tuwe na Governor ambaye atakuwa anasimamia rasilimali na utekelezaji, utumiaji pia ya wa rasilimali kwa ajili ya uboreshaji wa maisha ya wenyeji. Nikiendelea; kampuni yeyote au mtu binafsi atakaye chimba madini sharti auzie wenyeji hisa ya asilimia hamsini na moja - yaani kama vile Bara Arabu. Ukichimba mafuta geleni mbili, geleni moja iingie kwa wenyeji, geleni moja uende nayo - hii itatuwezesha kupunguza vita na kunungunika kwa ajili ya mali asili. Itaondoa pia vita kama vile Osama alivyofanya America.

Nikiendelea, mahesabu ya mapato kutoka kwa madini yawe yakipelekwa kwa County Council ili yatozwe ushuru. Kwa mfano nikieleza kwa ufafanusi: Utakuta mtu anauza mawe katika barabara hii ya Mwatate, amekutana na tajiri anauza mawe ya laki tano, na kuna mtu anakuja kutoka Mwadabogo, ametunda mboga zinaitwa *mtangu* analeta sokoni za shilingi arobaini, akifika sokoni anaambiwa na wale walioajiriwa na County Council atoe shilingi kumi kabla hajauza. Na kuna mtu hapa ameuza madini ametoka Taita ya laki tano, County Council haijajua, chairman wa County Council hajajua na hizo pesa zinapita moja kwa moja hata County Council haipati ushuru. Kwa hivyo ni lazima mapato yote ya madini na kila kitu kinachotoka katika rasilimali ya Taita Taveta yahusishwe kando na hii mambo ya "mnyunya mnyunya."

Halafu maji: Maji ni mengi hapa Taita sana wilayani Taita taveta. Ikiwezekana iwekwe shindikizo la kutumiwa kikamilifu - kama kunyunyisa mashamba na matumizi ya nyumbani. Kenya mzima juzi mambo ya *typhoid* yamezuka hapa Taita taveta kwa sababu watu wanatumia maji yasiowekwa dawa, maji yasiyo masafi na tumegundua maji ambayo yanawekwa kwa chupa kama hizi zilizo hapa mbele ya meza yanatoka hapa *Njota*. Yanatumiwa na mabwenyenye fulani, wanayauza na Mtaita hana uwezo wa kuyanywa.

**Com. Keriako Tobiko:** Unapendekeza nini kwa hiyo?

**Emmanuel Mzungu:** Napendekeza hivi; maji haya yaachiwe Wataita wayatumie kikamilifu na pato lolote lile litakalopatikana katika maji ya Taita, yawanufaishe Wataita. Kama vile Mzima springs. Si itoke hapa ikauzwe Mombasa na wakati Mtaita hata Kibwezi, hata Voi hana uwezo wa kuyanufaika. Unaona?

Halafu naingia kwa misitu: Misitu ihifadhiwe vizuri na isiporwe na wahalifu kwa manufaa yao wenyewe. Maana utakuta kwa mfano; chini chini ya mlima watu wenye pesa zao wanakwenda wanachukua mashamba pale halafu wale ambao hawana uwezo wa kuchukua mashamba pale hawajanufaika kwa njia yeyote ile. Kwa hivyo misitu iwe ni ya Wataita na iwe inawanufaisha Wataita. (kitaita). Wenyeji wetu hata (kitaita) msiduni.

Biashara: Mabenki yaregeze masharti magumu yaliyoko sasa ili kuwezesha wenyeji kuchukua mikopo kwa kustawisha biashara zao na ukulima bora. Kodi ndogo ndogo kama vile nilivyotangulia kusema za County Council - mama analeta mnyunya anaambiwa atoe shilingi kumi, na Maina Mbuta anauza mawe ya shilingi mia tano elfu hajatoa hata sumuni, ziondolewe mbali.

Mila na desturi: Katika Katiba ijayo ikiwezekana iwekwe wazi kwamba mambo yanayohusu mila yazingatiwe. Kwa mfano: Kesi za kifamilia au kijamii zitatuliwe kulingana na mila na desturi za Wataita. Nikitoa mfano ni kwa ule mfano ya wajaluo. Wakati Omweri alikufa – yule nyoka mkubwa, madaktari wa kijaluo waliomba ruhusa wakaenda kumtibu na alipokufa Serikali iliamua impeleke kwa museum na wajaluo wakakataa wakasema ni lazima azikwe kulingana na mila na desturi za kijaluo. Kwa hivyo sasa Wataita na wenyewe mila zao zizingatiwe sawasawa katika Katiba. Nikaomba kwamba, ama nasema hivi mwananamke yeyote wa kitaita asivae long, iandikwe kwamba "asivae." Maana inaleta madhara na matatizo katika nchi - Haya ni mambo ya western culture.

Halafu katika mila na desturi za Wataita, utumiaji na utengenezaji wa pombe za kienyeji zihalalishwe. Hii ni kusema ya kwamba hapa tunauziwa pombe zinaitwa *Gachungwa,* tunauziwa pombe zinaitwa C*hairman*, tunauziwa pombe zinaitwa *Katapingu*, zingine zinaitwa M*arios,* zingine zinaitwa C*hibuku*, zingine zinaitwa *Miti dawa,* zingine zinaitwa S*orghum*, zingine *Ranger*. Na *mbangala* pombe ambayo imekuwa ikikunyiwa tangu jadi, ukishikwa nayo kwanza unashikwa suruali hapa na unatembea kwa "storeys." (kitaita). Kwa nini? Hizi pombe za kienyeji zihalalishwe hata Nairobi pombe ile inaitangwa Njohi muratina iko wazi. Kwa nini twawekea Mnazi aibu (kitaita) ziko huru.

Naingia kwa uchaguzi ambapo Tume iko hapa na ningeomba masikio yenu. Bi. Mwanatume na Bwana mwanatume mlioko hapa, hapa nimefika kwenu. Macommissioners wa uchaguzi kwanzia ngazi ya kitaifa hadi wilaya wachaguliwe na wananchi. Hii itatuwezesha kuondoa kuingiliwa kati na mamlaka yaliyoko. Pia Tume hii wawe kati ya miaka thelathini na tano hadi sitini, wazee waliostaafu wasiruhusiwe kuomba kura au kazi katika Tume hii - Maana utakuta mzee mwingine alikuwa anafanya kazi na Cargo, amemaliza kazi na Cargo anakuja kuomba kazi katika Commission - Mtu ame-retire asiruhusiwe. Mwingine alikuwa na Serikali pia anafanya na Serikali anachaguliwa kwa sababu yule aliyo katika Serikali ni rafiki yake - nitamweka hapa ili kwa sababu akiwa pale ataniwezesha nini? - Kuingia ndani. Hatutaki hayo mambo. Tume ya Uchaguzi ichaguliwe na wananchi kuanzia ngazi za kitaifa hadi mashinani. Tume ya Uchaguzi ipewe uwezo wa kuondoa au kufutilia mbali uchaguzi wa Rais, Makamu wa Rais, Wabunge, Madiwani watakaopatikana wakitoa hongo au kosa la uchaguzi. Hii ni kwa sababu…….

**Com. Keriako Tobiko:** Tunaelewa sababu sasa enda pendekezo lingine.

**Emmanuel Mzungu:** Ningependa kusisitiza, lakini ngoja niendelee. Pia Bunge likivunjwa, hapo ni katika uchaguzi sasa, Rais akabidhi mamlaka kwa Speaker wa Bunge. Vile vile mawaziri na manaibu wao wakabidhi mamlaka yao kwa Speaker wa Bunge. Hii itazuia utumiaji mbaya wa mali na pesa za umma wakati wa uchaguzi. Wananchi wapewe uwezo wa kumuondoa

Mbunge au Diwani kabla ya muda wa miaka mitano kwa kupitia kura ya maoni ikiwa wana sababu za kutosha. Kwa mfano Mbunge au Diwani akishindwa kutekeleza kazi yake.

Siku ya kupiga kura ziwekwe tofauti, siku ya uchaguzi wa Rais iwe kando, siku ya wabunge iwe kando, siku ya diwani iwe kando. Na kura zote zihesabiwe katika polling station. Na polisi wa utawala ama polisi wasiingilie katikati. Hii itasaidia kule kuibiwa kwa kura.

Tume ya Uchaguzi pia ipewe uwezo wa kufuta na kushtaki hawa maofisa kukiwa na ushahidi wa kutosha - ikiwa amefanya makosa, Tume kama ya hawa waliokuja mbele zetu wawe na uwezo wa kuwaondolea mbali. Uteuzi wa wabunge na madiwani maalum ufutiliwe mbali kwani hawana manufaa yeyote kwa wananchi. Kwa mfano ningependa kueleza kwa ufupi: Nachaguliwa …

**Com. Keriako Tobiko:** Ndugu tuachane na mifano, umetoa mapendekezo. Move on.

**Emmanuel Mzungu:** Naendelea kumaliza sasa. Mengineyo: Katiba izingatie mambo ya kijinsia na watoto. Tungetaka nchini Kenya, Katiba itakayokuja - kulingana na Katiba iliyoko haielezi mtoto ni kuanzia umri wa miaka gani - tungetaka Katiba inayokuja iseme mtoto ikiwa ni kuanzia siku moja mpaka miaka kumi na nane iandikwe tujue na kijinsia pia akina mama wawe na uwezo wa kulea watoto kwanzia mwaka moja ama siku mmoja mpaka miaka kumi na nane hata akiwa ametengana na bwanake. Lakini --- watoto wawe ni wa baba. Mama naye apewe uwezo wa kulea kwanzia siku moja mpaka miaka kumi na nane maana wamama wengi wanatupa watoto chooni kwa sababu ya kuona ya kwamba wanashindwa kulea.

Serikali itoe elimu ya lazima ya shule za msingi bure. Pia Serikali itoe matibabu ya bure. Sheria za wafanyikazi ziangaliwe ili kuwe na hali nzuri na mishahara bora. Kwa mfano polisi, walimu, madaktari. Ukianzia kwa polisi, utakuta polisi anabeba bunduki kwanzia asubuhi mpaka jioni na tena kwanzia jioni anaambiwa”uwe alert.”

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa ndugu tunajua kazi ya polisi bwana.

**Emmanuel Mzungu:** Ngoja niendelee - nikiendelea kumaliza. Halafu hapa Taita Taveta kama nilivyotangulia kusema kuna mbuga za wanyama. Wako watu wanauliwa na wanyama wa pori hapa. Malipo au fidia ya mtu yeyote atakayeuawa na mnyama pori iwe wala isipungue chini ya shilingi milioni moja na nusu na isichukue zaidi ya miezi mitatu - maana watu wanauliwa hapa hawalipwi, inazungumziwa tu inazungumziwa tu. Serikali za wilaya zipewe uwezo wa kukusanya pesa zote za ushuru wilayani na pia ziwe zinalipa asilimia thelathini na tano kwa Serikali kuu na wala sio Serikali kuu ikusanye pesa hapa ipeleke huko juu. Maana tuko na watoto wanaopita mitihani, wanatakikana kwenda University- Serikali za wilaya zisimamie mambo kama hayo na miradi kama vile unyunyisaji wa maji, na mambo kurekebisha barabara za vijiji au kununua ma-tractors kama zamani ili yawe yanakodishwa na wakulima, wawe wanalipa na walimie mashamba yao na mbolea, wawe wanapewa kwa

ghalama za chini pamoja na mikopo---

**Com. Keriako Tobiko:** Mzungu, sasa unajua umechukua dakika arobaini na tano.

**Emmanuel Mzungu:** Namaliza niko na namba moja peke yake tafadhali bwana Commissioner wa Tume ya kurekebisha Katiba - namba moja peke yake. Halafu mwisho kuwe na hii ofisi ya Ombudsman kila wilaya. Halafu katika hiyo namba moja:

(a) Polisi wapewe mshahara mzuri wasiwe wanaende kupita kupita wakiomba pesa kwa wanawake wa kukoroga pombe ama kushika shika watu viuno.

(b) Halafu kikosi cha Administration kivunjiliwe mbali - kiunganishwe na polisi wa kawaida. Asanteni. Mimi ni Emmanuel Mzungu.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Bwana Mzungu. Jiandikishe na upeane memorandum yako hapo. Baada ya kusikiza Mzungu, kuna mwingine ako na maoni tofauti na yake?

**Hezron Mwachalo:** Nasema asanteni Ma-commissioners kutoka Nairobi halafu na makarani wanaohusika na wananchi kwa ujumla. Mimi kwa jina ni Hezron Mwachalo. Jambo ningelipendekeza Katiba yetu angalao kama itawezekana wafuatilie ni kwamba Rais achaguliwe na wananchi. Pili Rais kama atatoka Mkoa wa Kati, basi mdogo wake ama naibu wake atoke jimbo la Pwani. Halafu ningependekeza tena kwa upande wa Machifu na Ma-assistant chiefs. Wawe wanachaguliwa na wananchi kwa sababu mamlaka waliyoko nayo, wakati mwingine wanafinya wananchi kwa sababu wale ambao hawajui sheria basi wanafinywa kwa kulingana na udhaifu wao ama unyonge walioko nao.

Pia ningependekeza kwa upande wa ardhi - ardhi tusema kwa ujumla hapa sehemu yetu ya pwani, sehemu kubwa sana ambapo imekaliwa na wanyama. Sehemu nyingine imekaliwa na mashamba ya mikonge, sehemu nyingine pia inakaliwa na ranches na sehemu ambayo imekaliwa na wananchi ni ndogo mno. Tunaomba kama Katiba itatuwezesha ama itawezekana, basi mashamba mengine kama ‘Estates’, mashamba ya mikonge, wananchi angalao wagawie kidogo.

Mashamba mengine ya ranches kidogo yagawanywe ili wananchi wapate msaada - maana kuna wazazi ambao tunaokuwa na maisha yetu yanapita. Lakini wale ambao tumewazaa - hii young generation inahitaji sehemu kubwa ambapo sasa labda kuna mtu anaweza kuwa analima acres mia moja ama mia mbili. Mwingine naye hapo hapo analima labda acres tano. Kwa hivyo sasa tunaomba kama ni kuwagawanywa, igawanywe kulingana na vipengele ama sehemu sehemu za acres kumi kwa kila mmoja ama kama ni hamsini ipatikane hamsini kwa kila mmoja.

Halafu pia sehemu hii yetu ya jimbo la Pwani, kuna hawa ambao ni wezi na ni wauaji. Unakuta mtu ameiba leo, kesho anapelekwa kortini, baada ya muda unamkuta tena yuko nje. Inasemekana kwamba sheria haimruhusu mtu kukaa pale, ama

kuhukumiwa kwa haraka kulingana na sheria ya Kenya ile ilioko - kwamba wakati mtu ameshikwa, inabidi akae mpaka wakati ule wameamua vile sheria inavyosema. Sasa Katiba hii ninaomba kama mtu ameshikwa ni leo, kesho tumwone umwoni amepelekwa kortini badala ya kuwekwa muda mrefu ambapo watu wengine ambao wana watu wenye pesa wanaenda wanahongana ili kusudi mtu wao akifika pale anaachiliwa haraka. Kwa hivyo kwa hayo machache nawashukuru nasema asanteni.- Mbarikiwe.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo ndugu yangu.

**Com. Kabira:** Thank you very much and we want to thank all of you who have waited until this minute, and I hand over to the distict co-ordinator for any information she wants to give, and also to wind up the session.

**Fridah Mwadime:** Shukrani sana Macommissioners kwa kazi ambayo mmeifanya hapa na wananchi pia nawashukuru nyote.Wengi wameondoka lakini wale wamebaki ni kwa imani hiyo hiyo ya kurekebisha Katiba yetu. Sina mengi nikuomba tu kwamba pengine mwalimu Shalasha aje atufungie kwa maombi ya kiislamu maana tulianza kwaa maombi ya kikristu. Kwa hivyo mwalimu njoo utufungie ili tuweze kutawanyika na nafikiri wale waliobaki hapa ni watu wa karibu lakini, kwa niaba ya wilaya yote nzima nawashukuru nyote kwa kuweza kufika, na hata wafanyikazi wa Tume ambao wako pamoja nasi kwa kuweza kukaa nasi mahali hapa. Na kwa shule, naona bursar yuko pale, tafadhali peleka shukrani zetu kwa Principal wa shule hii, tunashukuru kwa kutuwezesha kuwepo mahali hapa siku ya leo. Asante sana.

**Mwalimu Shalasha:** (Prayer in Islam.) Ewe Allah tunakuomba kwa shukrani zote, tumekurejeshea wewe na tunakuomba utuongoze katika njia zetu, katika safari zetu sote tuliokuja hapa turudi salama salimini na tutakapofika huko tunakokwenda, Inshallah Allah tutakushukuru na tutakuhimidi. Allah tunakuomba uzidi kutulinda katika nchi hii, utupe baraka, utupe jaza , utupe mwongozo mzuri na uiongoze hii Tume ambayo iko hapa mbele yetu ili iweze kuhifadhi maoni yetu - iweze kuchukua maoni yetu kama tulivyoyatoa, na iweze kuyatumikia kisawa ili tupate Katiba itakayotufaa sisi zote kama Wakenya.

**Meeting ended at 6.00 p.m.**

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**